¹ Ndugu na laba, musikiye kujiteteya kwangu. ² Wakati makutano balisikiya Paulo kusema kwa luga ya kibrania, balinyamaza nakusema: ³ Mimi ni muyuda muzaliwa wa Tarse pale Silisia, niligfundishiwa pale, ku mikulu ya Gamalieli. Nilifundishiwa katika njia nzuri ya sheriya ya ba baba yetu. Niko na juhudi juu ya Mungu kama vile benye. ⁴ Nilisumbua hadi kufa benye balifata mafundisho ya Yesu. ⁵ Tena bakuhaui wakubwa na wazee batashuhudiya, kama nili pata bana kutoka kwabo juu ya wandugu wa Daniasi. Nirudiye ku Yerusalema nafunga watu kamba na kuhazzibu batu ba njia ya Yesu. ⁶ Alifika wakati niko kusafari, karibu na DAmasi, mana moya, na saa sita muchana, mwangaza mukubwa taka mbinguni ukanizaunguluka. ⁷ Nikaanguka kubulongo, nikasikia sauti moya, inasema: Saulo, Saulo! juu ya nini unanitesa? ⁸ Nikajibu: ninani bwana? akasema: Mimi ni Yesu wa Nazareti anaye tesa. ⁹ Bnegi balikuwa pamoja na miye baliona ule niwangaza, lakini habakusikiya sauti ya mutu anayesema na miye. ¹⁰ Nikasema: nifanye nini Bwana? Bwana akaniambiya: Simama na wende DAmasi, kule batakua mbiya benye utafanya. ¹¹ Sikuona tena juu ya mwangaza ule, na nikaenda Damasi nikiongozwa na batu tulikuwa nabo. ¹² Nilikutana na mutu jina yake Anania, anayeogopa Mungu kupitiya sheriya ya Musa, na batu bote bana mushuhudia muzuri. ¹³ Alikuya pembeni yangu, nakusema: Ndugu Saulo, fungua macho. Mara moya nikaona. ¹⁴ Na akasema: Mungu wa ba baba yetu anakuchakule juu utambue mapenzi yake, juu uone mema na juu usikiye sauti ino yotoka ku kinywa chake. ¹⁵ Sababu uta mushuhudiya mbele ya batu juu ya yote uliyoona na kusikiya. ¹⁶ Unachunga nini tena leo? Simama na ubatizwe nini na Zambi yako itakaswe uite jina lake. ¹⁷ Kisha kurudiya Yerusalema, na wakati nilikuwa naomba ndani ya hekale, nikaanguka nikaona maonyo. ¹⁸ Ondoka mbiyo Yerusalema kwa sababu habata amini ushu huda wako kuhusu mini. ¹⁹ Nikasema, bwana, banajua nili funga na kupiga fimbo batu baliyokua mini ndani ya makanisa. ²⁰ Wakati damu ya shahidi wako sitefana ilimwangika, nili kuwa pale, nikikubali na kuchunga manguo ya benye balimuwa. ²¹ LAkini aliniambiya: kwenda kwa sababu nakutuma mbali kwa bapagano. ²² Batu bali muru husu aseme mpaka pale. Kisha bakalalamika tena: Mumutoshe mutu wa hivi duniani, kwa sababu siyo vizuri aendeleye na kuishi. ²³ Wakati beko na lalamika, kuttupa manguo na majiwe angau. ²⁴ Kyongozi mukubwa wa waskari akaamuru Paulo aingiziwe ku nyumba ya wafungwa sababu asambishwe kwa kupiya fimbo juu atambue juu ya nini watu wanalalamika sababu yake. ²⁵ Wakati balimufunga kamba, Paulo akasema na kiongizi wa baskari: inaru husiwa kwenu humupiga fimbo Muruni ambaye hayasambishiwa? ²⁶ Wakati kiongozi wa baaskari alisikiya nvile, akaenda kwa kyongozi mukubwa wa baskari na kumuambia: unapenda kufanya nini? kwa maana huyu mutu ni mwanainchi wa kirumi. ²⁷ Kyongozi mukubwa wa baaskari akakuya na kusema: unisemeye, uko muruni? Akajibu: ndiyo. ²⁸ Kyongozi mukubwa wa waaskari akajibu : Ni kwa beyi kubwa nilipata ruhusa ya kuwa murumi. Na Paulo akasema mini nilizaliwa murunii. ²⁹ Batu lenye balikuwa naenda kumuuliza, balitoka pale haraka. Kyongozi wa waaskari nayeye akaogopa wakati alisikiya kama Paulo ni muruni, na yeye aliamuru afungiwe kanisa. ³⁰ Kesho yake, kyongozi wa baaskari alipenda kuya uhakika juu ya mastaki ya bayuda kuhusu Paulo balimufungula kamba, na kuleta oda kwa makuhani na kwa baraza ya bazee bakutane. Nguma alishusha Paulo na kumuweka mbele yabo.

Chapter 23

¹ Paulo akawakazia macho wale washauri wa Baraza Kubwa na kusema: «Wandugu zangu, mpaka leo zamiri yangu hainihukumu juu ya kitu chochote kinachoelekea mwenendo wangu mbele ya Mungu. ² Paulo aliposema maneno hayo, Kuhani Mkubwa Anania akawaamuru wale waliosimama karibu naye wamupige kofi kwenye kinywa. ³ Halafu Paulo akamwambia: “Mungu yeye mwenyewe atakupiga kofi, wewe unayeonekana kwa inje kama ukuta uliopakaliwa chokaa! Wewe unaikaa pale kwa kunihukumu kufuatana na Sheria. Lakini wewe mwenyewe unaivunja kwa kuamuru wanipige!” ⁴ Watu waliokuwa wakisimama karibu na Paulo wakamwambia: “Wewe unamutukana Kuhani Mkubwa wa Mungu!” ⁵ Paulo akasema: “Wandugu zangu, sikujua kwamba yeye ni Kuhani Mkubwa. Kwa maana imeandikwa katika Maandiko Matakatifu: Usimulaani mkubwa wa taifa lako.” ⁶ Halafu Paulo alikuwa akijua kwamba watu wamoja katika Baraza Kubwa walikuwa Wasadukayo na wengine Wafarisayo. Kwa hiyo akasema kwa sauti katika baraza: “Wandugu zangu, mimi ni Mufarisayo, mwana wa Mufarisayo. Mimi ninahukumiwa kwa sababu ninatumaini kwamba wafu watafufuka.” ⁷ Alipokwisha kusema maneno hayo, kukatokea ugomvi kati ya Wafarisayo na Wasadukayo, nao mkutano ukagawanyika. ⁸ (Ilitokea vile kwa maana Wasadukayo wanasema kwamba wafu hawatafufuka na kwamba hakuna wamalaika, wala roho; lakini Wafarisayo wanakubali mambo hayo yote.) ⁹ Basi kukakuwa makelele mengi, na walimu wamoja wa Sheria waliokuwa wa chama cha Wafarisayo wakasimama na kubishana kwa nguvu, wakisema: “Hatuoni ubaya wowote juu ya mtu huyu. Labda roho au malaika wamesema naye!” ¹⁰ Ugomvi ulipozidi sana, jemadari akaogopa kwamba watu wale watamururu Paulo. Kwa hiyo akaamuru waaskari waende katikati ya mkutano ule na kumwondosha Paulo kwa kinguvu katikati yao na kumrudisha ndani ya upango wa waaskari. ¹¹ Usiku ule ule Bwana akamutokea Paulo, akamwambia: “Ujipe moyo! Sawa vile ulivyotoa ushuhuda juu yangu hapa Yerusalema, ni vile vile utakavyopaswa kuutoa katika Roma.” ¹² Kesho yake kulipokucha, Wayuda wakafanya shauri; wakafanya kiapo kwamba hawatakula wala kunywa mpaka wamuue Paulo kwanza. ¹³ Na wale waliofanya shauri lile walikuwa zaidi ya watu makumi ine. ¹⁴ Wakaenda kuwaona Makuhani Wakubwa na wasimamizi wa watu na kuwaambia: «Sisi tumefanya kiapo; hatutasubutu kula kitu chochote mpaka tumuue Paulo kwanza. ¹⁵ Basi sasa, ninyi pamoja na Baraza Kubwa mumwombe jemadari awalettee Paulo, mukimwambia tu kwamba munataka kuchunguza vizuri zaidi maneno yake. Na sisi tuko tayari kumwua mbele hajafika hapa. ¹⁶ Lakini mupwa wa Paulo akapata habari ya vile watu wale wanavyovizia kumwua Paulo. Halafu akaenda katika upango wa waaskari na kumjulisha Paulo habari ile. ¹⁷ Basi Paulo akaita mmoja wa wakubwa wa waaskari na kumwambia: “Umupeleke kijana huyu kwa jemadari kwa maana yuko na neno la kumwambia.” ¹⁸ Yule mkubwa akaenda pamoja naye kwa jemadari na kumwambia: “Yule mufungwa Paulo aliniita, akaniomba nikuletee kijana huyu kwa sababu yuko na neno la kukuambia.” ¹⁹ Jemadari akamushika yule kijana mukono akaenda naye pembeni na kumwuliza: “Uko na habari gani ya kuniambia?” ²⁰ Kijana akasema: «Wayuda wamepatana kukuomba umulete Paulo kesho katika Baraza Kubwa. Nao watakuambia tu kwamba wakubwa wa baraza wanataka kuchunguza vizuri zaidi maneno yake. ²¹ Lakini wewe usikubali ombi lao, kwa sababu kuna watu zaidi ya makumi ine wanaovizia kumwua. Watu hawa wamefanya kiapo kwamba hawatakula wala kunywa mpaka wamuue Paulo kwanza.» ²² Yule jemadari akamwagiza yule kijana kwamba asimwambie mtu yeyote kwamba amemupasha habari hiyo, kisha akaagana naye. ²³ Kisha jemadari akawaita wakubwa wawili wa waaskari wake, akawaambia: «Mutayarishe waaskari mia mbili, waaskari wapanda-farasi makumi saba, na waaskari wapiga mikuki mia mbili kwa kwenda Kaisaria saa tatu ya usiku. ²⁴ Mutayarishe vilevile farasi wa kumubeba Paulo kusudi afike salama kwa liwali Feliki. ²⁵ Naye akaandika barua hii: ²⁶ “Mimi Klaudio Lusina, ninakuandikia wewe muheshimiwa Liwali Feliki, pokea salamu zangu. ²⁷ Wayuda walikuwa wamemukamata mtu huyu na kutaka kumwua. Nami nilipopata habari kwamba yeye ni mwanainchi wa Roma, nikaenda na kundi la waaskari na kumwokoa. ²⁸ Na kwa kuwa nilitaka kujua sababu gani Wayuda walimushitaki, nikamufikisha mbele ya Baraza yao Kubwa. ²⁹ Nikatambua kwamba wamemushitaki juu ya ubishi wenye kuelekea Sheria yao, lakini hakutenda kosa lolote linalomupasa kuuawa wala kufungwa. ³⁰ Na wakati nilipopata habari kwamba Wayuda wanafanya shauri la kumwua, mara moja nikakusudia kumutuma kwako, nami nimewaagiza watu wanaomushitaki walete mashitaki yao kwako.” ³¹ Basi wale waaskari wakafanya kama vile walivyoamuriwa. Wakamutwaa Paulo, na usiku ule ule wakamufikisha mpaka Antipatiri. ³² Kesho yake waaskari waliotembea kwa miguu wakarudi Yerusalema kwenye upango wa waaskari. Wakawaacha waaskari wapanda-farasi waendeleo pamoja na Paulo. ³³ Nao walipofika Kaisaria, wakamupa liwali ile barua na kumuleta Paulo kwake. ³⁴ Liwali akasoma barua ile na kumwuliza Paulo: “Wewe ni mtu wa jimbo gani?” Aliposikia kwamba yeye ni mtu wa jimbo la Kilikia, ³⁵ akamwambia: «Nitakusambisha wakati wale wanaokushitaki watakapofika.» Kisha akaamuru Paulo alindwe katika nyumba ya kifalme ya Herode.

Chapter 24

¹ Kisha siku tano, Anania, kiongozi mukubwa ya makuhanina waze kidogo, na musemayi moya anaitena Tertulo, waka enda pale, ku mustaki Paulo mbele ya liwali. ² Wakati Paulo ilisimama bele ya liwali Tertula akamustaki na kusema kwa liwali: "juu yako tu naishi amani, na kuona mbali kwako kunatuletea matengenezo mazuri ndani ya Taifa yetu". ³ Ni kwa shukurani sana tu na pokeyaka mambo yote uko na fanya muheshimiwa Feliski. ⁴ Nisi ponde muda wako, na kuomba unisikilize muzuri sana. ⁵ Uyu mutu tuna mukuta kuwa ugonya ya kotombokesha wayuda. Ni kiongozi ya zehebu ya watu wa Nazareti. ⁶ Tena alipenda ku ingiza hekalu yetu mu zehebu yake tu na mushika. ⁷ Lisiasi, afande ya waskari alikuya kutunyanganya Paulo ku mikano yetu na kuubeba. ⁸ Wakati utamuuliza maneno hiyi, uta yuwa weye mwenye sababu kani tuna mustaki. ⁹ Bayuda bote vile vile baka mustaki Paulo na ku hakikisha kama maneno ile ilikuwa ya kweli. ¹⁰ Lakini wakati liwali alifanya alama ya kumupa Paulo maneno aseme. Paulo akajibu: "na sikiya kusema kama oko muhamzi toka myaka mingi, na niko na futaha ni fasiliye miye mwenyewe". ¹¹ Unaweza ku uliza hakuya pita masiku kumi na mbili na lipanda kuabudu Yelusalema. ¹² Na wanani kuta ndani ya hekalu, sikwanza kubishana na mutu, wala kutombokesha kundi la watu; ikiwa mu shirika wala mu muguni. ¹³ Na hawa wezi kuhakikisha maneno bana nistaki sasa hivi. ¹⁴ Lakini naitika kama niko na mutumikiya Mungu kwa ile njiya wa naita zehemu. Niko mwaminifu kwa maandiko ya sheria na wa nabii. ¹⁵ Miye nabo pamoya tunaa tumaini kwa Mungu kama kuvo kufufuka wafu ya watu ya uhaki na wasiyo kuwa ndani ya uhaki. ¹⁶ Sababu nime mefanya nguvu yangu yote ni sikuwe na kitu kibaya mbele ya Mungu wala mbele ya watu. ¹⁷ Kisha myaka mingi, nali kuya na usaidizi wa franga na kutoa sadaka mu taifa langu. ¹⁸ Wakati nali fanya vile, wayuda wengine wa Asia walinikuta wakati ya kujitakasa ndani ya hekalu, bila kuwa na kikundi kya watu wala na wa ghasia. ¹⁹ Sasa batu aba kama beko na maneno kwangu banistaki. ²⁰ Watu hawa waseme kibaya kani walikuta ndani yangu, wakati nali samba mbele ya washauri. ²¹ Isipokuwa kitu moya nalisema kwa sauti nguvu, wakati nalikuwa ndani yabo: "Ni sababu ya kufufuka kwa wafu na sambishiwa kwenu". ²² Feliks alijuwa luzuri ile nyiya hivi akasikiliza bayuda akasema: "wakati kamanda Lesia atarudi Yerusaleme, nita amuwa maneno yenu". ²³ Kisha akatowa oda kwa kapitene alinde Paulo, wa mwatiyi uhuru kidogo bila kukataza wenzake kumu saidiya wala wasimutembeleya. ²⁴ Kisha mmasiku kidogo, Feliski akarudiya na Drusila bibi yake, muyuda, aka mu itisha Paulo na kumusikiya kuhusu nimani ndani ya Yesu Kristo. ²⁵ Gisi Paulo alikuwa na angeya naye kuhusu uhaki, uvumilivu, na ngisi Mungu ata sambisha wote, Feliski aka ogopa na ku sema: 'ondoka mbele yangu, nita kuitisha wakati nitapata muda'. ²⁶ Alikuwa natumaini asema Paulo ata mupa franga: ni kwa maana alikuwa namwitisha sana kuangeya naye. ²⁷ Lakini kisha myaka mbili, Porkiusi akakuwa liwli pa fasi ya Feliks. Kwa kupenda kufuraisha wayuda aka muacha Paulo gerezani.

Chapter 25

¹ Festo akafika ndani ya fimbo na kiisha siku akapanda Kaisaria pale Yelusalema. ² Koani mkuu na wayuda wengi vio ya juu wakamustaki Paulo mbele ya Festo na wakamuwambia kwa kinguvu. ³ Wakamuomba Festo na wanyekevu juu ya Paulo kusudi amuridishe Yelusalema kusudi ba muwe njiani. ⁴ Lakini Festo akawajibu Paulo yupo Genezani kule kaizaria, wakati nitarudia kule. ⁵ Akasema wanyi wanaweza kuenda pamoja na sisi. Kukuwa kitu moja ya ubaya juu ya mtu ule wamstaki. ⁶ Kiisha kukaa kule mdo wa siku Nane ao kumi na zaidi, akarudia kaisaria. Kesho yake akaka ku kitu cha kusambisha na akapana uusha ba mulete Paulo. ⁷ Wakati Paulo alipofika, wayuda wa Isalade wakakazibia pembeni naye (Paulo), wakasema maneno mingi ya ukweli juu ustakia ayo hawezi kujitosha ema. ⁸ Paulo akajitetea akasema: sikufanya hata kitu kibaya kwajina la wayuda, wala juu ya Ekalu wala juu Kaisara. ⁹ Lakini Festo alitoka kuwapendelea wa yaudi, akamwambia Paulo: unataka kwenda Yelusalema mkusambishe juu ya maneno aya? ¹⁰ Paulo akajibu mnasema kati kiti cha uamzi ya Sezaa, wapi tena naweza kuenda kusambishua. Sikufanya moavu kwa wayuda, ginsi unaifua vizuri sana. ¹¹ Kama sikufanya kosa na kama nilifanya kosa yenyi mtu anaweza kufa, sikatae fufa, lakini kama mastaki yao ni ya uwongo, hakuna mtu mwenye hanaweza kunipana kwao. Namuomba kwa kaisari. ¹² Festo akaongea na wabaraza yake kiisha akajibu: unaomba kusambishiwa kwa kaisari utaenda utaenda kwa Kaisari. ¹³ Kiisha siku chache mfalme Aripa na Berenise wakafika kaisaria kwa kumtembelia Festo. Kusha kuputisha siku mingi, Festo. ¹⁴ Kusha kupitisha situ minge, Festo akaonyesha maneno ya Paulo kwa mfalem. Akasema: Mtu fulani aliacwhua apa na Feliki kama vile mfungwa. ¹⁵ Wakati mlikuwa Yelusalema wakoani wa kuu na wazu wa wayauda walistaki mtu uyu kwangu na waliomba afungwe. ¹⁶ Nikajibu haiko dsturi wa Roma, kutoa mtu juu ya kufurahisha; mustakuwa anapashua kupata wa kati wa kujitetea mbele ya wenyi walimustari na kuonyesha makingo zabe mbele mastaki. ¹⁷ Ndio maana wakati walifika pamoja hapa, sikuongojea, kesho yake mkakaa chumba cha kusambisha, nikapana ruusa ya kumuita mtu ule. ¹⁸ Wakati watu wenyi walimustaki walifika kusamba sikuona hata neno juu yake yenyi ilikua sawa. ¹⁹ Walikuwa na mabishano kati yoana yey juu ya madini yao yenye kuangalia Yesu mwenyi alikufa na Paulo akiwambia yuko mzima. ²⁰ Akili ikanizunguka namma gani naweza kukata neno hii. Nikamualiza kama anaweza kwenda Yelusalema kusambisha maneno ayo. ²¹ Lakini Paulo akaomba achungwe kati ya nyumba ya gereza kwa kuongojea mpango mufalme. Nikapana ruusa wamchunge pale mpaka wakati nitamtuma Kaisari. ²² Agripa akasema na Festo: napenda pia kumusikia mtu ule". Fisto akamjibu, kesho utamusikia. ²³ Kesho yake, Ahgripa na Berenisa wakasindikizwa kwa ukubwa na wakubwa ya wakari na wakubwa wa ngi. Kwa uwezo wa Festo, Paulo bakamtosha inze. ²⁴ Festo akasema Mfalme Agripa na nginyi wote wenyi kuwa apa pamoja na sisi, Munaona mtu uyu; watu wengi wa wayuda walimambia pale Yelusalema na hata apa wanalalamika akufue. ²⁵ Najua kama hakufanya hata neno yenyi anastaili kufa, vile alifanya kumuita Mufalme, nilikasirisha kumtuma. ²⁶ Lakini sina neno la hakika kwa kwandisha kwa mufalme. Ndio maana nilimuleta mbele yenu, mbele ya mufalme Agripa, kusudinijue namma naweza kwandika juu ya neno hii. ²⁷ Kwani inanifania haina ukweli kwangu kumtuma ntu gerezari bila sababu na kujulisha osa lenyi alifanya.

Chapter 26

¹ Hivi, Agripa aka ambia Paulo: «ujiteteye peke yako.» Paul aka nyarosha mkono wake na kuji teteya. ² Niko na furaha, mufalme agripa, ku sambamba mambo yangu mbele yako leo kwa mastaki ya wa yuda kwangu. ³ Hasa juu kamili ku husu ma swali ya ki asiliya wa yuda. Hivi na kuomba uni sikilize vizuri. ⁴ Ba yuda bali juu vile nili komala tangu ujana wangu ndani ya inchi yangu na mu Yerusalema. ⁵ Bali ni juu tokeya mwanzo na balipaswa kuitika kama nili ishi saw mu Farissayo, dimi yenyi msimamo nguvu kwetu. ⁶ Hapa sasa na simama ku sambishwa juu nilitafuta ahadi Mungu alipatiya ba baba yetu. ⁷ Juu hii na ahadi ya ma kabila zetu kumi na mbili zili tumaini kupata wakati balikuwa baki abudu busiku na mehana. Ni kwa tumaini, mufalme Agripa, njoo ba yuda bananishitaki. ⁸ Ju ya nini lakuna mutu ndani yenu ana itika kama Mungu ana waza ku fufuka wafu? ⁹ Kwa wakati moja nili waza kama naweza kufanya mambo mingi kuzuwiya jina ya Yesu wa Nazareti. Nili bifanya mu Yerusalemu. ¹⁰ Nili tupa baminifu mingi ndani ya gereza, kwa oda ya ma kuhani wakubwa, na wakati bana ba uwa siku kuwa ngambo yabo. ¹¹ Nili ba azibu mara mingi ndani ya ma shirika na nili pima ku bakaza ba mu kufiru mungu nili basirikiya sana na ku ba tesa mpaka mitaa ya sio yetu. ¹² Wakati nilikuwa na fanya libi nili kuwa na enda Damasiko niki ruhusiwa na kuhani mkubwa. ¹³ Ku jiya, saa sita, mufalme niliona mwangaza kutoka mbinguni ili angaza kupita juu na ika waka iki ni zingira samoja na benzangu ya safari. ¹⁴ Wakati tuli anguka chini nika sikiya sauti kuni semeya mu ki hebrania : «Saulo, Saulo kwa nini una nitesa ni nguvu. kwako ku pinga teke mechokoo.» ¹⁵ Nika sema: weye ni nani Bwana? Bwana aka jibu: niko Yesu mwenyi una tesa. ¹⁶ Sasa simama juu sababu nili kutokeya ni kuku fanya mtumishi na mushuda wa mambo yenyi una juu sasa juu yangu na yingine niya ku oneshana tena. ¹⁷ Na nita ku okowa kwa taifa na wa pangono benyi nita kutuma kwabo. ¹⁸ Juu ya kufungula macho yabo na kuba tosha mu njiya ya giza baone mwangaza batoke kwenyi nguvu ya shetani ba mujuwe Mungu, juu Mungu aba urumiye zambi na wa pate urizi yenyi na wa patiya kwa wale na weka pembeni kwa imani yangu. ¹⁹ Kwa ile mufalme Agripa sita katala ku heshimiya ma ona ya mbingu. ²⁰ Lakini kwa wale wa Damasi ko kwanza, na kisha Yerusalemu mpaka mu Yudeya yote na wa pagano nao nili hubiri ili wa tubu na ku geukiya Mungu, kufanya maendo sawa ya wenyi wana okoka. ²¹ Njo sababu ba Yuda bali nifunga ndani ya hekalu na kujaribu ku ni uwa. ²² Mpaka sasa Mungu alini saidiya, juu na simama kushudiya kwa watoto na waku bwa wa matauja kwa ile ma nabii na musa wali sema ita fika. ²³ Ya kama Kristo ata tsekaka, na ata fufuka wa kwanza katika wafu na kutangaza mwangaza kwa mataifa wa Yuda na wa pagano. ²⁴ Wakati Paulo ali ongeza ku jiteya, Festo aka tomboka. «Paulo uko na bazima, ku juu kwako ina ku fanya bazimu.» ²⁵ Lakini Paulo aka sema sina bazimu muheshimiwa Festo; likini ni kwa uwezo nina sema hii maneno ya kweli kabisa. ²⁶ Juu mufalme ana juu kuhusu yale maneno na njo mana nayisema kwa uhuru, kwa juu hakuna kitu chochote yenyi inayo mufichwa; sababu hau ku fanyikwa kwa uficho. ²⁷ Una amini ma nabai, mufalme Agripa? «Na juu kama una iamani.» ²⁸ Agripa aka mjibu Paulo: unataka kuni vuta muda kidogo na unifanya niwe mu Kristo. ²⁹ Paulo akasema: na omba Mungu iwe kwa muda kidogo wala murefu, isiwe wewe tu lakini kwa wote wanao ni sikiya leo, baki wekama miye lakini bila minyororo ya gereza. ³⁰ kisha mufalme aka simama, liwali na Benike na bale bote baliyikala pamoja nabo. ³¹ Wakati bali toka mu nyumba ba ka anza ku sema ba moja kwa bengine na baka sema : «Huyu mutu haku fanya kitu yenyi anastahili kufa wala ku funguwa.» ³² Agripa aka mwambia Festo: « Huyu mutu angeli fungu liwa kama haku omba msaada kwa kaisara.»

Chapter 27

¹ Walipokwisha kukamata mupango wa kutusafirisha kwa njia ya chombo mpaka Italia, wakamuweka Paulo na wafungwa wengine chini ya uangalizi wa mkubwa mmoja wa waaskari aliyeitwa Yulio. Yeye alikuwa wa kundi la waaskari lililoitwa Kundi la waaskari wa mfalme. ² Tukapanda ndani ya chombo kilichotoka Adramiti, kilichokuwa tayari kupitia kwenye vivuko vya jimbo la Azia. Halafu tukaondoka tukiwa pamoja na mwanainchi mmoja wa Makedonia aliyeitwa Aristarko, wa Tesalonika. ³ Kesho yake tukatua Sidona. Yulio aliyemutendea Paulo mema, akamupa ruhusa ya kwenda kuonana na warafiki zake, wapate kumupa vitu alivyohitaji. ⁴ Kutoka kule, tukapita pembenipembeni ya kisanga cha Kipuro kwa kuepuka upepo uliokuwa ukivuma tokea mbele yetu. ⁵ Tukavuka bahari upande wa jimbo la Kilikia na Pamfilia, na kufika katika mji Mira, wa jimbo la Likia. ⁶ Kule yule mkubwa wa waaskari akakuta chombo kilichotoka Alesandria kwa kwenda Italia, naye akatupandisha ndani yake. ⁷ Tukasafiri polepole muda wa siku nyingi na kwa shida sana tukafika karibu na mji Kinido. Na kwa sababu upepo ulituzuiza kuendelea mbali ngambo ile, tukapita upande wa kusini wa kisanga cha Krete, kuelekea Salmone. ⁸ Tuliendelea pembenipembeni yake kwa shida sana hata tukafika pahali panapoitwa Vivuko Vizuri, karibu na mji Lasea. ⁹ Kisha kupitisha siku nyingi, tukafikia katika nyakati za hatari za safari ya bahari, kwa maana siku ya kufunga kula ilikuwa imekwisha kupita. Halafu Paulo akatupatia shauri hili: ¹⁰ «Wanaume, ninaona kwamba safari yetu itakuwa ya hatari na hasara nyingi, si kwa chombo na mizigo tu, lakini kwa maisha yetu vilevile.» ¹¹ Lakini yule mkubwa wa waaskari akasadiki zaidi maneno ya kapiteni na ya mwenye chombo kuliko kufuata shauri la Paulo. ¹² Na kwa sababu kivuko kile hakikukuwa na nafasi zuri ya kukaa wakati wa baridi kali, watu wengi kati yetu wakakubaliana kuondoka kule, kusudi ikiwezekana wafike Foinike, na kupitishia wakati wa baridi kali kule. Foinike ni kivuko kimoja kinachokuwa katika kisanga cha Krete, kinachoelekea upande wa kaskazini-magaribi na wa kusini-magaribi. ¹³ Upepo usiokuwa mukali ulipoanza kuvuma tokea kusini, wakazani kwamba wataweza tu kutimiza sawa walivyokuwa wamekusudia. Wakapandisha nanga na kuendelea pembenipembeni karibu sana na Krete. ¹⁴ Lakini nyuma kidogo, upepo mukali sana wa zoruba unaotokea upande wa mashariki-kaskazini ukavuma ukishuka tokea kwenye kisanga. ¹⁵ Upepo ukapeleka chombo, nacho hakikuweza kushindana nao. Halafu tukakiacha tu kipelekwe na upepo. ¹⁶ Tulipokuwa tukipita upande wa kusini wa kisanga kidogo kinachoitwa Kauda, tuliweza kwa shida sana kuopoa mutumbwi unaokokotwa na chombo. ¹⁷ Watumishi wa chombo walipokwisha kunyanyulia mutumbwi ule ndani ya chombo, wakakaza chombo kwa kukifungafunga na kamba kwa kukikingia na nguvu ya upepo. Na kwa kuwa waliogopa kwamba wasikwame kwenye lundo la muchanga wa ngambo ya Sirti, wakashusha tanga na kuachilia chombo kipelekwe na upepo. ¹⁸ Kesho yake kwa kuona jinsi zoruba ilivyoendelea kutusukumasukuma kwa nguvu, wakaanza kutupa mizigo katika bahari. ¹⁹ Na siku iliyofuata wakaamua kutupa hata vifaa vya chombo. ²⁰ Kwa muda wa siku nyingi hatukuweza kuona tena jua wala nyota, nayo zoruba ikaendelea kuvuma kwa nguvu. Kwa mwisho tukakata kitumaini chote cha kupona. ²¹ Watu walikuwa wamepitisha siku nyingi bila kula kitu. Halafu Paulo akasimama mbele yao na kusema: «Warafiki zangu, mungefuata shauri langu na kutoondoka Krete, hamungepata hasara hii na kupoteza vitu kama hivi. ²² Sasa ninawaomba mujipe moyo, kwa maana hakuna hata mmoja kati yenu atakayekufa, chombo tu ndicho kitakachoharibika. ²³ Kwa maana usiku malaika wa Mungu, ninayekuwa mtu wake na ninayemwabudu, alinitokea ²⁴ na kuniambia: Paulo, usiogope! Sherti usambe mbele ya Mfalme wa Roma. Na tena kwa kuwa inamupendeza Mungu kukutendea mema, yeye ataokoa maisha ya watu hawa wote wanaosafiri pamoja nawe. ²⁵ Basi mujipe moyo, kwa sababu ninamutumainia Mungu kwamba itatendeka sawasawa nilivyoambiwa. ²⁶ Lakini ni sherti tutupwe kwenye kisanga kimoja. ²⁷ Tulieneza majuma mawili tukipelekwa huku na huko na zoruba katika bahari ya Adria. Katikati ya usiku watumishi wa chombo waliwazia kwamba tumekaribia inchi kavu. ²⁸ Wakashusha kipimo ndani ya maji nao wakapata metre makumi ine kwenda chini. Mbali kidogo wakatupa tena kipimo na kupata metre makumi tatu. ²⁹ Kwa kuogopa kwamba chombo kisikwame kwenye mawe, wakashusha nanga ine za upande wa nyuma wa chombo na kungojea usiku ukuche. ³⁰ Wabaharia walitafuta kukimbia toka ndani ya chombo, wakashusha mutumbwi katika bahari, wakisema kwamba wanataka kufunga nanga tokea upande wa mbele. ³¹ Lakini Paulo akamwambia yule mkubwa wa jeshi pamoja na waaskari wengine: “Watu hawa wasipobakia ndani ya chombo hamutaokolewa.” ³² Halafu waaskari wakakata kamba zilizofunga ule mutumbwi na kuachilia uanguke katika bahari. ³³ Usiku ulipokaribia kucha, Paulo akawasihi watu wote kula chakula, akisema: “Sasa leo ni siku ya kumi na ine tangu mulipobaki bila kula kitu chochote. ³⁴ Basi ninawasihi ninyi mukule chakula, kwa sababu kitawafalia kusudi musikufe. Kwa maana hakuna mmoja kati yenu atakayepatwa na hasara yoyote hata kidogo.”» ³⁵ Kisha kusema maneno hayo, Paulo akatwaa mukate, akamushukuru Mungu mbele yao wote,

akaumega, na akaanza kula. ³⁶ Halafu wote wakatiwa moyo tena, nao vilevile wakakula chakula. ³⁷ Kwa jumla tulikuwa watu mia mbili na makumi saba na sita ndani ya chombo. ³⁸ Walipokwisha kushiba, wakatupa mizigo ya ngano katika bahari kwa kupunguza uzito wa chombo. ³⁹ Kulipokucha wabaharia hawakutambua inchi ile lakini wakaona nafasi bahari inapoingia ndani ya inchi kavu na kwenye kivuko. Basi wakakusudia kwenda kukwamisha chombo kule, kama ikiwezekana. ⁴⁰ Wakafungua nanga na kuziachilia zizame ndani ya bahari. Vilevile waliregeza kamba za makasia ya kuongoza chombo. Kisha wakafunga tanga ndogo mbele ya chombo kusudi kipelekwe na upepo, nao wakaelekea kwenye kile kivuko. ⁴¹ Lakini wakakwama kwenye lundo ya muchanga na chombo kikakwama pale. Sehemu ya mbele ya chombo ikazama kabisa pasipo kutikisika, lakini sehemu ya nyuma ikavunjikavunjika kwa kupigwa na zoruba kwa nguvu. ⁴² Halafu waaskari wapakata wazo la kuwaua wafungwa, kusudi hata mtu mmoja kati yao asitoroke kwa kuogelea. ⁴³ Lakini kwa kuwa mkubwa wa jeshi alitaka kumuponyesha Paulo, yeye akawazuiza wasitimize kusudi lao. Akaamuru wale waliojua kuogelea wajitupe wa kwanza ndani ya maji na kuvuka mpaka inchi kavu. ⁴⁴ Nao wengine wawafuate wakikamatilia kwenye mbao au kwenye vipande vya chombo. Ni vile watu wote walivyofika inchi kavu salama.

Chapter 28

¹ Tunapofika kwa kimia kati ya kisanga inahita malta . ² Watu wapale , walitukupo keya na upenda kutusaidiye, na kuwaki samotu juu tulilo bana na vula baridikali. ³ Na paulo alikuya nakifulushi ya kuni na kutiya kumoto, nyoka moya anaitua kipukusa anatoka juu ya kifuku na ili funga kumukono. ⁴ Wakatu ya mungini wana mona ile nyama anamufunga kwamuno, wanasemama moyana mwingine , uyu mutu ni muwaji kweli nana atamusaidia na imabaya, namuzi ya Mungu inatuma a ishi tena. ⁵ Na alitikisa mukono nyoka ananguka kumoto na neno ya mubaya a imukamate. ⁶ Balitishu nga agoje wala akufe na muna ya gafula, na bakatshunga saa mulefu, akuna mubuya yayote, na bikonaye muziri wana badilisamasemi kusema alikuwa mutu ya Mungu. ⁷ Basinamazingila pale ilikawa tajili mukubwa jina lake pablo alipokeye naga lama ya siku tatu. ⁸ Na akafika baba yake na pablo aligonza oma . ⁹ Natangu Paulo a naenda kwake anamuombeya na kumutiya mukono na akepona pale, nanyo mayaku ona mamba aya, wakanzi walikua na magonza wa mekuya na wamepona ¹⁰ Wakanzi wana mwisimu sana, na tangu tulingiya nasi tunamupatiya ya mana . ¹¹ Nyuma ya miezi tatu, tuna panda masua na iskanda ili kuwa baridi sana nakisanga, alikuwa nafundisa bamapacha. ¹² Na nyumu tunakwenda sirikusa na tunahikala pale siku tatu. ¹³ Tulipana na kufuka na mutaa ya regio nyuma yasiko moya, na mupepe ya kusuni, inakuya tuna fanya siku mbili, na tunai ika mutaa waputoli. ¹⁴ Kule tuna kuta banduku, balituta tuhisi nabo siku saba, na namuna tulifika roma. ¹⁵ Wanduku wakati walisikia tunasema, walifika kukamata kule limanga ya apias, tatu, Paulo anabaona wapendua anarudisasifa kwa Mungu nakutiya ujasir. ¹⁶ Tunafika roma, Paulo alilusiwa kuhisi ye peke na asari ya kumu tshunga. ¹⁷ Na nyuma ya masiko tatu, Paulo kusanya watu walikuwa viongozi yakati ya wayuda alialika mukutano, alisema bandaku atasifana vizuri mbele ya taifa na destruri ya baba yetu, sijali fungwa a yelusaleme ku kumikono ya waroma. ¹⁸ Wana iluza muzuri wamuru kiniatsha nituke niende juu abanikute na mabaya ata moya bani ukumu nikufe. ¹⁹ Laki wayohuda walikatalu ile mupango, nilikuwa na ngufu ya kuyita Cesar, tata siko kama nilikuwa kubeba mahukumu juu ya taifa Yesu. ²⁰ Juu yayo kuko nalomba nani museme, kwa sababu yake ikona israela niko kufunga nakamba ile. ²¹ Na alisema, atuko nambaruwa ya yunani, ju yako na akana akuya kusema mabaya yako. ²² Tunataka kusikiya mawazo yako kamuna juya ilezeebu inatembe kinyume ya kila mamali. ²³ Alikuwa ana tangaza siku juu yake, batu mingi wataifika wata kuwa kasi kusikiya maneno atayaseme mbele ya ufame ya Mungu, alilimba juu ya Yesu na seria ya musa na wanabi kuhaza asubuy tongo mangai libi. ²⁴ Bingina balikubali juu mambo alisema na bingine balekata wali, zalayu ²⁵ Walikosa banaza kubisana waona wao na yanatoka ka juu ya Baba na yisaya. ²⁶ Anasema wenda mbele kizazi nasema naowasikiye kumasikio na basidjuwe mana, bahone matsho basiona kitu. ²⁷ Basi mioyo ya taifa inakuwa mugumu, masiki yabo isitume kusikiliza, na basizwe mioyo kubali kupona. ²⁸ Yuwa kwaza ukovu ya MUngu, inatokana nakusikiya na anapele kakwa mataifa. ²⁹ Wakati wayudea walisiki ya wame toka na kweda, wana ona kupoteya mbele yao ³⁰ Paulo alisi katika makao yake miaka miwili alipokeya wote walikika kumuona na kumufarizi kwake. ³¹ Na alikuwa kufundisa juu ya ufalme ya Mungu na mambo ya bwa Yesu kristo ku uzasiri yote alifa nya

Book: Romans

Romans

Chapter 1

¹ Barua hii inatoka kwangu mimi Paulo, mutume wa Kristo Yesu, niliyeitwa na Mungu kuwa mutume na niliyewekwa kwa kazi ya kutangaza Habari Njema yake. ² Habari Njema hiyo iliahidiwa na Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake katika Maandiko Matakatifu. ³ Habari hiyo inaelekea Mwana wake ndiye Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye alizaliwa kimwili katika uzao wa mfalme Daudi. ⁴ Lakini kwa namna ya Roho Mtakatifu, alihakikishwa kwa uwezo kuwa yeye ni Mwana wa Mungu kwa njia ya kufufuka kwake. ⁵ Kwa njia yake Mungu amenipa neema ya kuwa mutume kusudi niongoze mataifa yote yapate kumwamini na kumutii. Na kwa tendo hilo jina lake lipate kusifiwa. ⁶ Nanyi vilevile munakuwa kati ya watu wale; mumeitwa na Mungu mukuwe watu wa Yesu Kristo. ⁷ Ninawaandikia ninyi wote wapenzi wa Mungu munaokaa Roma, mulioitwa kuwa watu wake watakatifu. Ninawatakia neema na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. ⁸ Kwanza ninamushukuru Mungu wangu kwa njia ya Yesu Kristo kwa ajili yenu ninyi wote, kwa sababu habari za imani yenu zinasambaa katika dunia nzima. ⁹ Mungu ambaye ninamwabudu kwa roho yangu yote kwa njia ya kutangaza Habari Njema ya Mwana wake, ni mushuhuda wangu kwamba ninawakumbuka siku zote ¹⁰ katika maombi yangu. Ninaomba kwamba Mungu akitaka, anifungulie njia ya kuwatembelea siku hizi. ¹¹ Kwa maana ninatamani sana kuonana nanyi, kusudi nigawanye pamoja nanyi zawadi ya kiroho, mupate kusimama imara. ¹² Ni kusema kwamba nipate kutiwa moyo kwa njia ya imani yenu na ninyi kwa njia ya imani yangu. ¹³ Wandugu zangu, ninataka mujue kwamba mara nyingi nilikusudia kuwatembelea, lakini mpaka sasa ninapata vizuizo. Ningetamani kupata matunda ya kazi yangu katikati yenu vilevile, kama inavyokuwa katikati ya watu wa mataifa mengine. ¹⁴ Kwa sababu ninapaswa kwanza kuwaendea watu wote: Wagriki na wasiokuwa Wagriki, wenye elimu na wasiokuwa na elimu. ¹⁵ Ni kwa sababu hii ninatamani sana kuhubiri vilevile Habari Njema kwenu ninyi munaokaa Roma. ¹⁶ Mimi sisikii haya juu ya Habari Njema, kwa sababu huo ndio uwezo wa Mungu unaowaokoa wote wanaoamini, kwanza Wayuda na kisha Wagriki vilevile. ¹⁷ Kwa maana Habari Njema inaonyesha namna Mungu anavyowahesabia watu haki mbele yake. Jambo hilo haliwezekani isipokuwa kwa njia ya kuamini tu. Ni sawa vile inavyoandikwa katika Maandiko Matakatifu yanayosema: «Mwenye haki ataishi kwa njia ya imani.» ¹⁸ Tokea mbinguni Mungu anaonyesha kwamba anawakasirikia wote wanaofanya zambi na maovu, wanaowazuiza watu wasitambue ukweli kwa njia ya matendo yao mabaya. ¹⁹ Kwa maana mambo yanayoweza kujulikana juu ya Mungu ni wazi kwao, kwa kuwa Mungu mwenyewe ameyaoonyesha kwao waziwazi. ²⁰ Tangu Mungu alipoumba dunia, hali zake zisizoonekana, ni kusema uwezo wake wa milele na umungu wake, vinaonekana kupitia viumbe vyake. Kwa sababu hii watu wale hawatapata namna yoyote ya kujitetea. ²¹ Ijapokuwa wanamujua Mungu, hawamutukuzi wala kumushukuru kama vile anavyostahili. Lakini mawazo yao yaligeukia mambo ya ovyo ovyo, na mioyo yao isiyokuwa na ufahamu ilibaki katika giza. ²² Wanajidai kwamba wao ni wenye hekima, lakini wako wapumbafu. ²³ Kwa pahali pa kumwabudu Mungu anayeishi milele, wakaabudu sanamu zilizochongwa kwa mufano wa mtu anayekufa, wa ndege, wa nyama na hata viumbe vyenye kutambaa. ²⁴ Kwa sababu hii Mungu aliwaacha wajichafue wenyewe kwa kufuata tamaa ya mioyo yao na kutendeanza mambo ya haya wao kwa wao. ²⁵ Wanabadilisha ukweli juu ya Mungu kuwa uongo; wanaabudu na kutumikia vitu vilivyoubwa kuliko Muumba mwenyewe, anayestahili kutukuzwa milele! Amina. ²⁶ Kwa hiyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za haya. Wanawake wao wanabadilisha matumizi ya kawaida na matumizi isiyokuwa ya kawaida. ²⁷ Na wanaume nao vilevile wanabadilisha matumizi ya kawaida ya mume na muke, wakiwakiana tamaa wanaume kwa wanaume. Kwa ajili ya hiyo, wanajipatia wenyewe azabu wanayoistahili kufuatana na huo upotevu wao. ²⁸ Hivi kufuatana na vile walivyokataa kumutambua Mungu, Mungu akawaacha wafuate akili yao ya upotevu, kusudi wafanye mambo wasiyopaswa kufanya. ²⁹ Wamejaa kila namna ya uovu, ubaya, tamaa na upotovu. Wamejaa wivu, uuaji, ugomvi, udanganyifu na ukorofi. Wao ni wenye kuchongeana, ³⁰ wasingizaji, wenye kumuchukia Mungu, wenye kasirani, wenye kiburi na wenye kujivuna. Wao ni werevu kwa kutenda mabaya, hawatii wazazi wao, ³¹ hawana zamiri, hawawezi kuaminiwa, hawana upendo wala huruma. ³² Nao wanajua kwamba Sheria ya Mungu inasema kwamba watu wanaotenda maneno haya wanastahili kufa. Lakini hata hivi wanaendelea, si kuyafanya tu, lakini kukubaliana na wale wanaoyatenda.

Chapter 2

¹ Wewe unayemuhukumu mwingine hauna namna yoyote ya kujitetea, haizuru wewe ni nani. Kwa maana wakati unapohukumu mwingine, unajikatia hukumu wewe mwenyewe, kwa sababu wewe unayehukumu unatenda mambo yale yale. ² Tunajua kwamba Mungu anahukumu kwa haki watu wanaofanya mambo ya namna hiyo. ³ Basi wewe unawahukumu wale wanaofanya mambo yale, lakini wewe mwenyewe unayafanya! Unafikiri kwamba utaponyoka hukumu ya Mungu? ⁴ Au haujali na uwingi wa wema, utulivu na uvumilivu wa Mungu? Haujui kwamba wema wake ungeweza kukuongoza hata upate kugeuka toka zambi? ⁵ Lakini wewe ni mugumu na mwenye moyo usiotaka kugeuka. Kwa hiyo unajiwekea azabu kubwa siku Mungu atakapoonyesha kasirani yake na hukumu yake ya haki. ⁶ Kwa maana Mungu atamulipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. ⁷ Wale wanaofanya matendo mema bila kuchoka na kutafuta toka kwa Mungu utukufu, heshima na uzima usiokuwa na mwisho, Mungu atawapa uzima wa milele. ⁸ Lakini wapingaji na wale wanaokataa kufuata ukweli, wakifuata uovu, wataangukiwa na kasirani na hasira ya Mungu. ⁹ Mateso na taabu zitamupata kila mtu anayefanya mabaya: kwanza Wayuda, kisha Wagriki vilevile. ¹⁰ Lakini kila mtu anayefanya mema atapata utukufu, heshima na amani; kwanza Wayuda, kisha Wagriki vilevile. ¹¹ Kwa maana Mungu hana upendeleo. ¹² Wote wanaofanya zambi pasipo kujua Sheria ya Musa watapotea pasipo kuhukumiwa na Sheria ile. Lakini wote wanaofanya zambi wakijua Sheria watahukumiwa kufuatana na Sheria. ¹³ Ni vile kwa sababu si wale wanaosikia Sheria ndio wanaohesabiwa haki mbele ya Mungu, lakini ni wale wanaotii Sheria. ¹⁴ Watu wa mataifa hawana Sheria ya Musa. Lakini wanapofanya sawa inavyoamuriwa na Sheria ile kutokana na zamiri yao, wao ni Sheria kwa ajili yao wenyewe, ijapokuwa hawana Sheria ile. ¹⁵ Kwa maana wanaonyesha kwamba maagizo ya Sheria yameandikwa ndani ya mioyo yao. Zamiri yao vilevile inawahukumu, na mawazo yao yenyewe yanawashitaki au yanawatetea. ¹⁶ Hiyo ndiyo itakayotokea siku ile Mungu atakapohukumu mambo ya siri ya watu kwa njia ya Yesu Kristo, kama vile Habari Njema yangu inavyosema. ¹⁸¹⁷ Sasa wewe unaitwa Muyuda, unategemea Sheria na kujivunia Mungu. ¹⁸ Unajidai kwamba unajua mapenzi yake na kutambua mambo yanayofaa zaidi kwa sababu umefundishwa na Sheria. ¹⁹ Unajiaminia kwamba wewe ni mwongozi wa vipofu na mwangaza kwa wale wanaokuwa katika giza, ²⁰ mufundisha wajinga na mwalimu wa watoto, kwa sababu kutokana na Sheria unajua uhakika juu ya mambo ya elimu na ya kweli. ²¹ Basi wewe unayewafundisha watu wengine, kwa sababu gani haujifundishi wewe mwenyewe? Wewe unayehubiri kwamba haifai kuiba, kwa nini unaiba? ²² Wewe unayesema kwamba haifai kuzini, kwa nini unazini? Wewe unayechukia sanamu za miungu, kwa nini unaiba vitu ndani ya hekalu zao? ²³ Unajisifu kwamba unajua Sheria, lakini unamuzarau Mungu kwa kuvunja Sheria! ²⁴ Kwa maana kama ilivyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Kwa sababu yenu, jina la Mungu linatukaniwa katikati ya watu wa mataifa mengine.» ²⁵ Kutahiriwa kuna mafaa kama ukitii Sheria. Lakini usipotii Sheria, wewe unahesabiwa kama mtu asiyetahiriwa. ²⁶ Na kama mtu asiyetahiriwa akitii maagizo ya Sheria, Mungu hatamuhesabu kuwa ametahiriwa? ²⁷ Mtu asiyetahiriwa kimwili, lakini anatii Sheria, atakuhukumu wewe unayevunja Sheria ijapokuwa unajua maandiko ya Sheria na umetahiriwa. ²⁸ Kwa maana kuonekana kwa inje kwa Muyuda si kuwa Muyuda wa kweli, wala kutahiriwa kimwili tu si kutahiriwa kwa kweli. ²⁹ Lakini Muyuda wa kweli ni yule anayekuwa Muyuda kwa ndani, nako kutahiriwa kwa kweli ni kule Roho Mtakatifu anakofanya ndani ya moyo wa mtu, wala si kule kunakofanyika kwa njia ya maandiko ya Sheria. Mtu wa namna hii hapati sifa kutoka kwa watu lakini ku

Chapter 3

¹ Basi kuna faida gani kuwa Muyuda? Na kutahiriwa kuna mafaa gani? ² Kuna faida kubwa sana kila upande. Kwanza, Mungu alifunua Neno lake kwa Wayuda kusudi walishike. ³ Tuseme nini basi? Ikiwa wamoja kati yao hawakukuwa waaminifu, jambo hilo litaweza kuonyesha kwamba Mungu ataacha kuwa mwaminifu? ⁴ Hapana hata kidogo! Sherti Mungu ajulikane kuwa mwenye ukweli, na kila mtu kuwa mwongo, kama inavyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Ee Mungu, sherti ujulikane kuwa mwenye haki katika masemi yako. Nawe ushinde wakati unaposhitakiwa.» ⁵ Lakini ikiwa kwa njia ya ubaya tunaofanya, Mungu anaonekana kuwa mwenye haki, basi tutasema kama Mungu hana haki wakati anapotuazibu? (Ninasema kwa mafikiri ya kimtu.) ⁶ Hapana hata kidogo! Ingekuwa vile, namna gani basi Mungu angeweza kuhukumu dunia? ⁷ Lakini ikiwa kwa njia ya uongo wangu ukweli wa Mungu unaonekana naye anatumizwa zaidi, basi kwa nini tena ninahukumiwa kama mwenye zambi? ⁸ Ikiwa ni vile, basi tuseme: «Tufanye mabaya kusudi kutokee mema?» Hakika kuna watu wamoja wanaonisingizia wakisema kwamba nimesema vile. Watu hawa wataazibiwa sawa inavyowapasa! Hakuna mwenye haki mbele ya Mungu. ⁹ Basi tuseme nini? Sisi Wayuda tunawapita Wagriki nini? Hatuwapiti kitu hata kimoja! Kwa maana nimekwisha kuonyesha kwamba Wayuda na watu wa mataifa mengine wote wako chini ya utawala wa zambi. ¹⁰ Ni sawa ilivyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Hakuna hata mtu mmoja mwenye haki! ¹¹ Hakuna mtu mwenye ufahamu, hakuna mwenye kushugulika na Mungu. ¹² Wote wamepotea, wote kwa jumla wamepotoka. Hakuna mwenye kufanya mema, hata mmoja. ¹³ Vinywa vyao ni kama kaburi wazi, ndimi zao ni za kudanganya, ndani ya midomo yao munaoka sumu kali sawa ya nyoka. ¹⁴ Vinywa vyao vinajaa laana na maneno ya uchungu. ¹⁵ Wao ni wepesi kwa kumwanga damu. ¹⁶ Wanaharibu na kuangamiza popote wanapopita, ¹⁷ hawawazi juu ya njia ya kuleta amani, ¹⁸ nao hawamwogopi Mungu hata kidogo.» ¹⁹ Basi tunajua kama maneno yote yanayosemwa na Sheria, yanawaelekea wale wanaolazimishwa kutii Sheria, kusudi mtu yeyote asikuwe na namna ya kujitetea, na dunia nzima ipaswe kuhukumiwa na Mungu. ²⁰ Kwa sababu hakuna mtu atakayehesabiwa haki mbele ya Mungu kwa kuwa anatii Sheria, maana Sheria inamusaidia mtu tu kwa kutambua kwamba amefanya zambi. ²¹ Lakini sasa Mungu ameonyesha njia ya kumuhesabia mtu haki mbele yake, na si kwa njia ya Sheria. Maandiko ya Sheria na manabii yanashuhudia kwamba ²² kuhesabiwa haki na Mungu kunapatikana kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote wanaoamini, kwa maana hakuna tofauti yoyote kati yao, ²³ kwa maana wote wamefanya zambi na kukosa utukufu wa Mungu. ²⁴ Lakini kwa neema ya Mungu wanahesabiwa haki kwa bure kwa njia ya Kristo Yesu anayewakomboa. ²⁵ Kristo alitolewa na Mungu kuwa sadaka ya usamehe wa zambi kwa njia ya damu yake kwa ajili ya wenye kumwamini. Mungu alifanya hivi kwa kuonyesha haki yake. ²⁶ Zamani, katika uvumilivu wake, aliacha kuazibu zambi za watu. Lakini kwa wakati wa sasa anaonyesha haki yake kusudi akuwe mwenye haki na kumuhesabia haki kila mtu anayemwamini Yesu. ²⁷ Basi sasa mtu ataweza kujivuna? Hapana! Kwa sababu gani? Kwa sababu anatii Sheria? Hapana. Lakini kwa sababu anamwamini Yesu. ²⁸ Kwa maana tunaona kama mtu anahesabiwa haki mbele ya Mungu kwa njia ya imani wala si kwa njia ya kutii Sheria. ²⁹ Au Mungu ni Mungu wa Wayuda tu? Yeye si Mungu wa watu wa mataifa mengine vilevile? Ndiyo, yeye ni Mungu wa watu wa mataifa mengine vilevile, ³⁰ kwa sababu kuna Mungu mmoja tu. Na ni yeye atakayewahesabia waliotahiriwa na wasiotahiriwa haki mbele yake kwa njia ya imani ya kila wamoja. ³¹ Basi ni kusema kwa sababu ya imani ile tunaitupilia Sheria? Hapana hata kidogo! Lakini tunasimamisha Sheria.

Chapter 4

¹ Basi tuseme nini juu ya babu yetu kimwili Abrahamu? Nini iliyomutokea? ² Ikiwa Abrahamu alihesabiwa haki mbele ya Mungu kwa njia ya matendo yake, angeweza kujivuna. Lakini hawezi kujivuna mbele ya Mungu. ³ Kwa maana Maandiko Matakatiifu yanasema: «Abrahamu alimwamini Mungu na kwa hiyo akahesabiwa kuwa mwenye haki.» ⁴ Mtu anayefanya kazi, mushahara wake hauhesabiwi kama zawadi, lakini ni haki yake. ⁵ Lakini mtu asipotegemea matendo yake mwenyewe, naye akimwamini Mungu anayemuhesabia mwovu haki, basi imani yake inahesabiwa kuwa haki. ⁶ Na ni vile Daudi anavyosema juu ya uheri wa mtu ambaye Mungu anayehesabia haki pasipo kuangalia matendo yake. ⁷ Heri wale waliosamehewa makosa yao, nazo zambi zao zimefutwa. ⁸ Heri mtu yule Bwana asiyemuhesabia zambi zake. ⁹ Uheri huu si kwa watu wanaotahiriwa tu, lakini ni kwa watu wasiotahiriwa vilevile. Kwa maana tumekwisha kusema kwamba Abrahamu alihesabiwa kuwa mwenye haki kwa njia ya imani yake. ¹⁰ Yeye alihesabiwa vile alipokuwa katika hali gani? Alipokuwa amekwisha kutahiriwa au alipokuwa hajatahiriwa bado? Halikutendeka nyuma ya kutahiriwa kwa Abrahamu lakini mbele ya kutahiriwa kwake! ¹¹ Nyuma ya pale alitahiriwa, na kutahiriwa kwake kulikuwa kitambulisho cha kuhakikisha ile haki Mungu aliyomuhesabia kwa njia ya imani yake. Hivi Abrahamu akakuwa baba wa watu wote wanaoamini, ijapokuwa hawatahiriwi, kusudi wao vilevile wahesabiwe haki. ¹² Vilevile yeye ni baba ya wale wanaotahiriwa, si kwa sababu wametahiriwa tu, lakini kwa sababu wanafuata vilevile njia ile ile ya imani ambayo babu yetu Abrahamu alifuata alipokuwa hajatahiriwa. Mungu anatimiza ahadi yake kwa wenye kumutumainia ¹³ Mungu alimwahidi Abrahamu na wazao wake kwamba atawapa dunia kuwa urizi wao, si kwa sababu alishika Sheria lakini kwa sababu Mungu alimuhesabia haki kwa njia ya imani yake. ¹⁴ Kwa maana ikiwa wale wanaotii Sheria ndio watakaopokea kitu anachoahidi, basi imani haina mafaa yoyote, nayo ahadi ya Mungu ni bure. ¹⁵ Kwa sababu Sheria inaamusha kasirani ya Mungu. Lakini Sheria haingekuwa, kuvunja Sheria hakungekuwa vilevile. ¹⁶ Kwa hiyo ahadi inafuatana na imani, kusudi ikuwe imetolewa kwa neema ya Mungu. Na zaidi kuwe uhakikisho kwamba ahadi hiyo ni kwa ajili ya wazao wote wa Abrahamu, si kwa wale wanaotii Sheria tu, lakini vilevile kwa wale wanaokuwa na imani kama Abrahamu, babu yetu sisi wote. ¹⁷ Ni sawa vile inavyoandikwa katika Maandiko Matakatiifu: «Nimekuweka kuwa babu wa mataifa mengi. Abrahamu alimwamini Mungu, kwa hiyo yeye ni baba yetu mbele yake. Ni yeye Mungu anayewafufua wafu na kuamuru vitu visivyokuwa vipate kuwa. ¹⁸ Abrahamu aliamini na kutumainia mambo ambayo yasingewezekana kutumainia na hivi akakuwa babu ya mataifa mengi, kufuatana na maneno haya Mungu aliyomwambia: “Hivi ndivyo wazao wako watakavyokuwa wengi.” ¹⁹ Yeye alikuwa na umri wa miaka karibu mia moja, lakini imani yake haikupunguka alipofikiri juu ya hali yake iliyokuwa kama ya mwenye kungojea tu lufu wala juu ya hali ya Sara aliyekuwa hawezi tena kuzaa. ²⁰ Hakuona shaka juu ya ahadi aliyopewa na Mungu wala kupoteza tumaini, lakini imani yake ilimutia nguvu hata akamutukuza Mungu. ²¹ Alifanya vile kwa sababu alijua hakika kwamba yule aliyetoa ahadi ile yuko na uwezo wa kuitimiza. ²² Kwa sababu hiyo alihesabiwa kuwa mwenye haki ²³ Lakini maneno hayo alihesabiwa kuwa mwenye haki» hayakuandikwa kwa ajili yake yeye mwenyewe, ²⁴ lakini vilevile kwa ajili yetu sisi tutakaohesabiwa haki. Ndio sisi tunaomwamini yule aliyemufufua Yesu Bwana wetu. ²⁵ Alitolewa kufa sababu ya makosa yetu na kufufuliwa kusudi tupate kuhesabiwa haki mbele ya Mungu.

Chapter 5

¹ Sasa kufuatana na vile tumekwisha kuhesabiwa haki mbele ya Mungu kwa njia ya imani, kunakuwa sasa amani kati yetu na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. ² Kwa njia ya imani, Yesu ametuwezesha kukaribia neema ya Mungu, inayokuwa musingi wetu. Sababu hii tunafurahi tukiwa na tumaini la kushiriki katika utukufu wa Mungu. ³ Zaidi ya hii, tunafurahi vilevile kwa ajili ya mateso tunayopata, kwa sababu tunajua kwamba mateso yanaleta uvumilivu, ⁴ na uvumilivu unaleta uaminifu kamili na uaminifu ule unaleta tumaini. ⁵ Nalo tumaini hili si la udanganyifu, kwa sababu Mungu amemimia upendo wake ndani ya mioyo yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu aliyetupatia. ⁶ Kwa maana tulipokuwa hatuna uwezo wowote, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu kwa wakati uliopangwa. ⁷ Ni vigumu kwa mtu kukubali kufa kwa ajili ya mwenye haki. Labda mtu anaweza kujitolea kufa kwa ajili ya mtu mwema. ⁸ Lakini Mungu ameonyesha wazi upendo wake kwetu ni wapata gani, kwa maana tulipokuwa tungali wenye zambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. ⁹ Sasa kwa kuwa tumehesabiwa haki mbele ya Mungu kwa njia ya damu ya Yesu, inaonyesha zaidi sana kwamba atatuokoa kusudi kasirani ya Mungu isituangukie. ¹⁰ Basi ikiwa kama tulipokuwa waadui za Mungu tulipatanishwa naye kwa njia ya kufa kwa Mwana wake, inaonyesha zaidi sana kwamba tukiwa tumepatanishwa naye, tutaokolewa kwa njia ya uzima wa Kristo. ¹¹ Wala si ile tu, lakini tunafurahi kwa ajili ya Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo aliyetupatanisha sasa na Mungu. ¹² Kwa njia ya mtu mmoja zambi iliingia katika dunia, nayo zambi ikaleta kifo. Ni hivi vilevile kifo kimefikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi. ¹³ Kulikuwa zambi katika dunia mbele hakujakuwa Sheria, na kwa muda Sheria ilipokuwa haijakuwa, Mungu hakuhesabu zambi. ¹⁴ Lakini kifo kilitawala tangia wakati wa Adamu mpaka wakati wa Musa, hata juu ya wale wasiofanya zambi kwa kuvunja amri, sawa vile Adamu alivyofanya. Naye ni mufano wa yule aliyengojewa kuja. ¹⁵ Lakini kuna tofauti kubwa kati ya zawadi ya Mungu na kosa la Adamu. Kwa maana ikiwa kosa la mtu mmoja lilisababisha kifo cha watu wengi, inaonyesha zaidi sana kwamba Mungu amezidisha neema yake kwa ajili ya watu wengi na zawadi inayotokana nayo kwa njia ya mtu mmoja, Yesu Kristo. ¹⁶ Tena, kuna tofauti kati ya zawadi ya Mungu na mambo yaliyotokea kwa sababu ya zambi ya yule mtu mmoja. Kwa maana hukumu iliyosababishwa na zambi ya mtu mmoja, ilileta azabu, lakini zawadi ya neema ambayo Mungu alitoa kisha makosa mengi, ilileta kuhesabiwa haki mbele yake. ¹⁷ Ni kweli kwamba kifo kilitawala kwa njia ya mtu mmoja, kwa sababu ya kosa la huyo mmoja. Lakini inaonyesha zaidi sana kwamba wale wanaopewa neema ya Mungu kwa uwingi na zawadi ya haki yake, wataishi na kutawala kwa njia ya mtu mmoja, Yesu Kristo. ¹⁸ Basi kama vile kosa la mtu mmoja limewaletea watu wote azabu, ni hivi vilevile tendo la haki la mtu mmoja limewaweka huru na kuwapa uzima. ¹⁹ Na kama vile kutokana na uasi wa mtu mmoja, watu wengi wamekuwa wenye zambi, ni hivi vilevile kutokana na utii wa mtu mmoja, watu wengi watahesabiwa haki mbele ya Mungu. ²⁰ Sheria ilitokea na kusababisha kuongezeka kwa makosa, lakini nafasi yoyote palipozidi zambi, neema ilizidi sana. ²¹ Hivi kama vile zambi ilivyotawala na kuleta kifo, hivi vilevile neema ya Mungu itawale kwa njia ya haki na kuleta uzima wa milele, kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu.

Chapter 6

¹ Basi sasa tuseme nini? Tuendeleo kuishi katika zambi kusudi neema ya Mungu izidi kuongezeka? ² Hapana hata kidogo! Sisi tuliokufa kwa ajili ya zambi, namna gani tutaweza tena kuishi katika zambi? ³ Munajua hakika kwamba sisi wote tulipobatizwa tuliungana na Yesu Kristo; kwa njia hiyo tuliungana naye katika kufa. ⁴ Hivi, kwa njia ya ubatizo, tuliungana naye katika kufa na katika kuzikwa kwake, kusudi kama vile Kristo alivyofufuliwa kwa uwezo wenye utukufu wa Baba, sisi vilevile tupate kuishi katika maisha mapya. ⁵ Ikiwa tuliungana naye kwa njia ya kufa kama yeye, tutaungana naye vilevile kwa njia ya kufufuliwa kama yeye. ⁶ Kwa maana tunajua kwamba ule utu wetu wa zamani ulitundikwa pamoja na Kristo, kusudi tusitawaliwe tena na hiyo tabia ya zambi na tusikuwe tena watumwa wa zambi. ⁷ Kwa sababu mtu akikufa anapata uhuru toka katika zambi. ⁸ Ikiwa tumekufa pamoja na Kristo, tunaamini kwamba tutaishi pamoja naye vilevile. ⁹ Kwa maana tunajua kwamba Kristo amefufuliwa, naye hawezi kufa tena, kwa sababu kifo hakina tena uwezo juu yake. ¹⁰ Kuelekea jambo la kufa kwake, alikufa mara moja tu kwa ajili ya zambi; lakini kuelekea maisha yake, sasa anaishi kwa ajili ya Mungu. ¹¹ Hivi vilevile mujihesabu kuwa mumekufa kwa ajili ya zambi na kuwa munaishi pamoja na Mungu mukiungana na Yesu Kristo. ¹² Basi musiache tena zambi kutawala katika mwili wenu wa kufa, hata mupate kufuata tamaa zake mbaya. ¹³ Musitoe tena viungo vya mwili wenu kufanya zambi, mukivitumikisha kama vyombo vya kufanya mabaya. Lakini mujitoe wenyewe kwa kumutumikia Mungu kama watu waliofufuliwa na mutumikishe viungo vya mwili wenu kama vyombo vya kufanya haki. ¹⁴ Kwa maana hamutatawaliwa tena na zambi, kwa sababu hamuishi chini ya uongozi wa Sheria lakini chini ya uongozi wa neema ya Mungu. ¹⁵ Ni nini basi? Tufanye zambi kwa sababu sisi hatuishi chini ya Sheria, lakini chini ya uwongozi wa neema ya Mungu? Hapana hata kidogo! ¹⁶ Munajua hakika kwamba mukijitoa wenyewe kwa mtu fulani kuwa watumwa wake na kulazimishwa kumutii, munakuwa kweli watumwa wa yule munayemutii. Ikiwa ni utumwa wa zambi, mwisho wake ni kifo; ikiwa ni kumutii Mungu, mwisho wake ni maisha ya haki. ¹⁷ Lakini asante kwa Mungu, kwa maana ninyi muliokuwa zamani watumwa wa zambi mumetii sasa kwa moyo wenu wote kanuni za mafundisho muliyopewa. ¹⁸ Mumewekwa kuwa huru toka katika utumwa wa zambi, na sasa mumegeuka watumwa wa haki. ²¹ ¹⁹ (Ninatumia luga ya kawaida ya wanadamu kwa sababu ya uzaifu wenu wa kimtu). Zamani mulijitoa kabisa kuwa watumwa wa kufanya mambo machafu na maovu kwa kuishi katika machafuko. Hivi vilevile mujitoe kabisa kuwa watumwa wa kufanya haki kusudi muweze kuishi katika utakatifu. ²⁰ Wakati mulipokuwa watumwa wa zambi, mulikuwa huru kufuatana na mambo ya haki. ²¹ Basi mulipata faida gani kwa kufanya mambo yale munayopata haya juu yake sasa? Maana mwisho yao ni kifo! ²² Lakini sasa kufuatana na vile mumewekwa huru toka utawala wa zambi na kugeuka watumwa wa Mungu, munapata faida ya kuishi katika utakatifu na kwa mwisho kupewa uzima wa milele. ²³ Kwa maana mushahara wa zambi ni kifo, lakini zawadi Mungu anayotoa ni uzima wa milele kwa kuungana na Yesu Kristo, Bwana wetu.

Chapter 7

¹ Wandugu zangu, munajua uhakika juu ya maneno haya nitakayowaambia, kwa maana ninyi ni watu wanaoelewa Sheria vizuri: Sheria haina mamlaka juu ya mtu isipokuwa tu wakati angali mzima. ² Kwa mufano, mwanamuke aliye olewa anafungwa na Sheria katika maisha yake na mume wake wakati mume wake angali mzima. Lakini kama mume wake akikufa, yeye anakuwa huru kufuatana na Sheria ile iliyomufunga. ³ Basi kama akiolewa na mtu mwingine wakati mume wake angali mzima, atahesabiwa kuwa muzinzi. Lakini kama mume wake akikufa, yeye anakuwa huru toka Sheria ile iliyomufunga na hata akiolewa na mtu mwingine hatahesabiwa kuwa muzinzi. ⁴ Nanyi wandugu zangu, ni hivi inavyokuwa kwa ngambo yenu. Kufuatana na maneno ya Sheria, ninyi vilevile mumekufa, kwa maana muliungana na mwili wa Kristo. Na sasa munakuwa wa mtu mwingine, ndiye yule aliyefufuka, kusudi tupate kufanya matendo yanayofaa katika kazi ya Mungu. ⁵ Kwa maana tulipoishi maisha ya kimwili, tamaa ya kufanya zambi iliyotokana na Sheria ilitumika ndani yetu na kutuletea kifo. ⁶ Lakini sasa tumekuwa huru toka vifungo vya Sheria, kwa maana tunakuwa kama waliokufa kufuatana na mambo yale yaliyotufunga. Kwa hiyo tunaweza kumutumikia Mungu kwa kufuata njia mupya chini ya uongozi wa Roho wake, wala si kufuata njia ya zamani chini ya uongozi wa maandiko ya Sheria. ⁷ Tuseme nini basi? Sheria ni zambi? Hapana hata kidogo! Lakini pasipo Sheria singejua zambi ni nini. Kwa maana singejua kutamani ni nini kama Sheria isingesema: «Usitamani.» ⁸ Kutokana na amri, zambi ilipata njia hata kuamusha kila namna ya tamaa ndani yangu. Kwa maana pasipo Sheria zambi ingekuwa kama mufu. ⁹ Zamani nilikuwa mzima pasipo kujua Sheria, lakini wakati amri ilipotokea, zambi ikaanza kutenda kazi, ¹⁰ nami nikakufa. Hivi ile amri iliyopasa kuniletea uzima ikaniletea kifo. ¹¹ Maana kutokana na amri ile, zambi ilipata njia ya kunidanganya na kuniua kufuatana na amri ile ile. ¹² Basi Sheria yenyewe ni takatifu na amri ni takatifu, ya haki na nzuri. ¹³ Basi ni kusema kile kinachokuwa kizuri kimeniletea kifo? Hapana hata kidogo! Ni zambi ndiyo iliyoniletea kifo. Lakini kusudi zambi ionekane kuwa zambi kweli kweli, ilipitia kwa njia ya kile kinachokuwa kizuri kwa kusababisha kifo changu. Hivi kwa njia ya amri ile, zambi ilizidi kujikamilisha kuwa zambi kabisa. ¹⁴ Tunajua kwamba Sheria inaelekea maisha ya kiroho, lakini mimi ni mtu wa kimwili, kwa maana nimeuzishwa kama vile mutumwa wa zambi. ¹⁵ Hakika sijui kitu ninachofanya. Kwa maana kile ninachotaka kufanya, sikifanyi; lakini kile ninachochukia, ndicho ninachofanya. ¹⁶ Ikiwa kile ninachofanya ndicho nisichotaka, maana yake ninakubali ya kuwa Sheria ni nzuri. ¹⁷ Basi sasa si mimi ninayekifanya, lakini ni zambi inayokaa ndani yangu. ¹⁸ Kwa maana ninajua kwamba hakuna kitu kizuri kinachokaa ndani yangu, ni kusema katika hali yangu ya kimwili. Ni hivi kwa sababu ninakuwa na utashi wa kufanya jambo jema, lakini sifikii kulifanya. ¹⁹ Jambo jema ninalotaka kufanya, silifanyi, lakini jambo baya nisilotaka, ndilo ninalofanya. ²⁰ Basi kama ninafanya kile nisichotaka kufanya, si mimi ninayekifanya, lakini ni ile zambi inayokaa ndani yangu. ²¹ Basi ninatambua kanuni hii: wakati ninapotaka kufanya jambo jema, mara moja ninavutwa kufanya jambo baya. ²² Ndani ya roho yangu ninapendezwa na Sheria ya Mungu, ²³ lakini ndani ya mwili wangu ninaona sheria ingine ikipigana na mafikiri yangu. Nayo inanifanya mufungwa wa sheria ya zambi inayotumika ndani ya mwili wangu. ²⁴ Ole kwangu, mimi mtu wa taabu! Ni nani atakayeniokoa kutoka katika mwili huu unaokuwa wa kufa? ²⁵ Mungu ashukuriwe kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo! Basi hivi kwa upande mmoja ninatumikia sheria ya Mungu kwa akili yangu, lakini kwa upande mwingine ninatumikia sheria ya zambi kwa hali yangu ya kimwili.

Chapter 8

¹ Basi sasa hakuna azabu kwa wale wanaoungana na Yesu Kristo. ² Maana sheria ya Roho anayepana uzima kwa kuungana na Yesu Kristo imetuweka kuwa huru kutoka sheria ya zambi na ya kifo. ³ Mungu alitimiza mambo yale Sheria ya Musa iliyoshindwa kuyatimiza, kwa sababu ya ukosefu wa nguvu unaotokana na hali zaifu ya kimwili. Mungu alitoa hukumu juu ya zambi inayotawala mwili kwa kutuma mwana wake wa peke katika hali ya kimtu, mwenye hali zaifu ya zambi kwa ajili ya kuondoa zambi. ⁴ Alifanya vile kusudi maagizo ya haki ya Sheria yapate kutimizwa ndani yetu sisi tunaishi kufuatana na uongozi wa Roho wa Mungu, lakini si kufuatana na hali yetu ya kimwili. ⁵ Kwa maana wale wanaoishi kwa kufuatana na hali ya kimwili, na uongozi wa Roho wa Mungu wanashugulika na mambo yanayotakiwa na Roho yule. ⁶ Kushugulika na mambo yanayotakiwa na hali ya kimwili kunaleta kifo lakini kushugulika na mambo yanayotakiwa na Roho wa Mungu kunaleta uzima na amani. ⁷ Kwa maana wale wanaoshugulika na hali ya kimwili ni waadui za Mungu; hawatii sheria ya Mungu wala hawawezi kuitii. ⁸ Watu wanaotawaliwa na hali ya kimwili hawawezi kumupendeza Mungu. ⁹ Lakini ninyi sasa hamutawaliwi na hali yenu zaifu ya kimwili, lakini munatawaliwa na Roho Mtakatifu, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu. Na mtu yeyote asiyekuwa na Roho wa Kristo ndani yake, yeye si mtu wa Kristo. ¹⁰ Lakini kama Kristo anakaa ndani yenu, ijapokuwa mwili wenu unakufa kwa sababu ya zambi, Roho ndiye uzima wenu kwa maana munahesabiwa haki mbele ya Mungu. ¹¹ Na kama Roho wa Mungu aliyemufufua Yesu anakaa ndani yenu, basi huyo aliyemufufua Kristo atapatia mwili wenu unaokuwa wa kufa uzima kwa njia ya Roho wake anayekaa ndani yenu. ¹² Basi wandugu, tuko na deni, lakini si la kutimiza mapaswa ya hali yetu ya kimwili hata tuishi kufuatana na hali ile. ¹³ Kwa maana kama mukiishi kufuatana na hali ya kimwili, mutakufa. Lakini kama mukiua matendo mabaya ya mwili kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, mutaishi. ¹⁴ Wote wanaoishi chini ya uongozi wa Roho wa Mungu ni watoto wa Mungu. ¹⁵ Kwa maana hamukupewa roho anayewafanya muishi katika utumwa na kuwatia tena woga, lakini mulipewa Roho anayewafanya mukubaliwe kuwa watoto wa Mungu. Na kwa uwezo wa Roho huyo, tunaweza kumwita Mungu Baba. ¹⁶ Roho huyo mwenyewe anahakikisha ndani ya roho zetu kwamba sisi ni watoto wa Mungu. ¹⁷ Na kama sisi ni watoto, basi tutakuwa na sehemu katika urizi ule Mungu aliowaahidi watu wake, na tutashiriki pamoja na Kristo katika urizi ule; kwa maana kama tukiteswa pamoja naye tutatukuzwa pamoja naye vilevile. ¹⁸ Ninaona kwamba mateso ya wakati huu wa sasa hayawezi kupima kulinganishwa na utukufu ambao Mungu atakaoonyesha kwetu waziwazi. ¹⁹ Viumbe vyote vinangojea kwa hamu sana wakati Mungu atakapowaonyesha watoto wake waziwazi. ²⁰ Kwa maana viumbe vyote vimewekwa chini ya utawala wa mambo ya ovyo, si kwa mapenzi yao, lakini kwa sababu ya yule aliyewatia katika hali hiyo. Lakini kungali tumaini hili: ²¹ siku moja viumbe hivi vitawekwa huru toka katika utumwa wa uharibifu na kushiriki katika uhuru wenye utukufu wa watoto wa Mungu. ²² Kwa maana tunajua kwamba mpaka sasa viumbe vyote vinaugua kwa uchungu kama mwanamuke anayesikia maumivu ya kuzaa. ²³ Na si viumbe hivi tu; hata sisi tuliokwisha kuwa na Roho wa Mungu kama sehemu ya kwanza ya zawadi Mungu atakazotoa, tunaugua vilevile ndani yetu, tuingojea kukubaliwa na Mungu kuwa watoto wake, maana yake kukombolewa kwa kimwili. ²⁴ Kwa maana tumeokolewa, lakini ni kwa tumaini. Mtu akiona kitu anachokitumainia, hilo si tumaini tena, kwa maana nani anayeweza kuendelea kutumainia kitu anachokiona? ²⁵ Lakini tukitumainia kitu tusichokiona, tunakingojea kwa uvumilivu. ²⁶ Na ni hivi vilevile Roho wa Mungu anatusaidia katika uzaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba sawa inavyopaswa. Lakini Roho wa Mungu yeye mwenyewe anatuombea kwa Mungu kwa kuugua kusikoweza kuelezwa. ²⁷ Na Mungu anayeona yanayokuwa ndani ya mioyo yetu, anajua nia ya Roho Mtakatifu, kwa maana Roho anawaombea watu wa Mungu kufuatana na mapenzi ya Mungu. ²⁸ Tunajua kwamba katika mambo yote Mungu anatumika kwa mazuri ya wale wanaomupenda, ndio wale walioitwa naye kufuatana na kusudi lake. ²⁹ Kwa maana wale Mungu aliowachagua tangu zamani, ndio aliofanya mupango juu yao tangu zamani, apate kuwafananisha na Mwana wake, kusudi Mwana wake akuwe muzaliwa wa kwanza wa wandugu wengi. ³⁰ Na wale Mungu aliowachagua tangia zamani, aliwaita vilevile; nao aliwaita, akawahesabia haki, nao aliowahesabia haki, akawatukuzisha vilevile. ³¹ Basi kufuatana na mambo hayo, tuseme nini zaidi? Mungu akiwa upande wetu, ni nani anayeweza kupingana nasi? ³² Yeye hakumwacha Mwana wake wa pekee, lakini alimutoa kwa ajili yetu sisi wote. Namna gani atakosa kutupatia vilevile vitu vyote kwa njia ya mwana wake? ³³ Ni nani anayeweza kuwashitaki watu ambao Mungu alijichagulia? Hakuna hata mmoja! Mungu peke yake amewahesabia haki mbele yake. ³⁴ Ni nani anayeweza basi kuwahukumu? Hakuna hata mmoja! Maana Yesu Kristo ndiye aliyekufa, na zaidi ya hiyo, alifufuka, na sasa anakaa na mamlaka kwa kuume kwa Mungu, na yeye ndiye anayetuombea. ³⁵ Ni nani anayeweza kututenga na upendo wa Kristo? Ni taabu, au huzuni, au mateso, au njaa, au ukosefu wa nguo, au hatari, au kifo? ³⁶ Kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema: «Kwa sababu yako tunauawa kila siku.

Tunahesabiwa kama kondoo wa kuchinjwa.» ³⁷ Lakini katika mambo haya yote tunapata ushindi kabisa kwa njia ya yule aliyetupenda. ³⁸ Kwa maana ninajua hakika kwamba hakuna kitu kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu: wala kifo, wala uzima, wala wamalaika, wala watawala, wala mambo ya sasa, wala mambo yatakayokuja, wala wenye uwezo, ³⁹ wala nguvu za juu, wala nguvu za chini, wala kiumbe kingine chochote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu alioonyesha kwetu kwa njia ya Kristo Yesu Bwana wetu.

Chapter 9

¹ Ninasema ukweli kwa kuungana na Kristo. Na kwa uongozi wa Roho Mtakatifu zamiri yangu inanihakikishia kwamba sisemi uongo: ² mimi nina huzuni kubwa na uchungu usiokuwa na mwisho ndani ya moyo wangu. ³ Ingekuwa heri nilaaniwe na kutengwa na Kristo kwa ajili ya wandugu zangu wa damu, ⁴ ndilo taifa la Waisraeli. Wao walikubaliwa na Mungu kuwa watoto wake, yeye aliwaonyesha utukufu, alifanya maagano nao, aliwapa Sheria, aliwaonyesha namna ya kumwabudu na kuwatolea ahadi zake. ⁵ Wao ni wazao wa babu zetu, na Kristo alizaliwa kimwili katika kizazi chao. Yeye ndiye mkubwa kupita wote na Mungu anayesifiwa kwa milele! Amina. ⁶ Sisemi kwamba ahadi ya Mungu haikutimia. Kwa maana si wote wanaotoka katika uzao wa Israeli ndio Waisraeli wa kweli, ⁷ wala si wote wanaotoka katika uzao wa Abrahamu, ndio watoto wa kweli wa Abrahamu. Kwa kuwa Mungu alimwahidia Abrahamu: «Ni kwa njia ya Isaka utapata wazao watakaoitwa wako. ⁸ Maana yake, si wale waliozaliwa sawa na kawaida wanaohesabiwa kuwa watoto wa Mungu; lakini ni wale waliozaliwa kufuatana na ahadi ya Mungu ndio wanaohesabiwa kuwa wazao wake wa kweli. ⁹ Kwa sababu hii ndiyo ahadi ya Mungu: “Kwa wakati kama huu, nitakuja tena, na Sara atazaa mtoto mwanaume.” ¹⁰ Na si vile tu; Rebeka alikuwa na watoto wawili aliowazaa na mume mmoja, ndiye babu yetu Isaka. ¹¹ Watoto wale walipokuwa hawajazaliwa bado, wala hawajatenda jambo lolote nzuri au baya, Mungu alimwambia Rebeka hivi juu yao: “Mkubwa atamutumikia mudogo.” ¹² Alisema vile kwa kutimiza mupango wake unaotokana na uchaguzi wake usiofuatana na matendo ya watu, lakini mwito wake kwao. ¹³ Kama vile Maandiko Matakatifu yanavyosema: “Nimemupenda Yakobo, lakini nimemuchukia Esau.” ¹⁴ Basi tuseme nini? Mungu hafuati haki? Hapana hata kidogo! ¹⁵ Kwa maana anamwambia Musa: “Nitamuhurumia yule ninayependa kumuhurumia; nitamurehemu yule ninayependa kumurehemu.” ¹⁶ Basi mambo hayo, hayatokani na mapenzi ya mtu wala juhudi yake, lakini yanatokana na rehema ya Mungu. ¹⁷ Mungu anamwambia mfalme wa Misri katika Maandiko Matakatifu: “Nimekusimika kuwa mfalme kwa sababu hii moja, ni kusudi kwa njia yako nipate kuonyesha uwezo wangu na kusudi jina langu lipate kutangazwa katika dunia yote.”» ¹⁸ Basi ni kusema kwamba Mungu anamuhurumia yule anayetaka, na kumufanya mugumu yule anayetaka. Kasirani na huruma za Mungu ¹⁹ Labda utaniambia: «Ikiwa ni vile, sababu gani Mungu anawashitaki watu? Kwa maana hakuna anayeweza kupingana na mapenzi yake. ²⁰ Halafu sasa wewe mwanadamu ni nani hata ubishane na Mungu? Chombo cha udongo hakiwezi kumwuliza mufinyanzi: “Kwa nini umenitengeneza hivi?”» ²¹ Mufinyanzi anaweza kufanya sawa vile anavyotaka na udongo. Toka donge moja la udongo anaweza kutengeneza chombo kimoja cha heshima na kingine cha matumizi ya kawaida. ²² Basi kuna nini? Mungu alitaka kuonyesha kasirani yake na kutambulisha uwezo wake. Lakini aliwawumilia sana wale waliostahili kupatwa na kasirani yake na waliokuwa wametayarishwa kwa kuangamizwa. ²³ Vilevile alitaka kuonyesha uwingi wa utukufu wake kwa wale aliowasikilia huruma; wale ambao alitayarisha tangu zamani kwa kuwatukuzisha. ²⁴ Ndio sisi tulioitwa naye, si toka kati ya Wayuda tu, lakini toka kati ya watu wa mataifa mengine vilevile. ²⁵ Ni vile anavyosema katika maandiko haya ya nabii Hosea: «Wale waliokuwa si watu wangu nitawaita sasa Watu wangu. Taifa lile nililokosa kulipenda nitaliita sasa Mupendwa wangu. ²⁶ Na pahali pale walipoambiwa: “Ninyi si watu wangu! pale wataitwa Watoto wa Mungu Mwenye Uzima.” ²⁷ Isaya alisema kwa sauti juu ya Waisraeli: “Ijapokuwa Waisraeli ni wengi kama muchanga wa bahari, ni wachache tu watakaookolewa. ²⁸ Kwa maana Baba atatimiza kabisa kusudi lake juu ya dunia bila kukawia.” ²⁹ Ni kama vile Isaya alivyokuwa ametangulia kusema: “Kama Bwana wa Majeshi hangetuponyeshea wamoja wa wazao wetu, ingetutokea sawa Sodoma, ingegeuka kwetu sawa Gomora.”» Waisraeli hawakufuata njia ya kuhesabiwa haki ³⁰ Basi tuseme nini? Watu wa mataifa mengine waliokosa kutafuta kuhesabiwa haki mbele ya Mungu wamehesabiwa haki mbele yake kwa njia ya imani. ³¹ Na kwa ngambo ingine, Waisraeli waliokuwa wakitaifuta Sheria kusudi kwa njia yake wapate kuhesabiwa haki mbele ya Mungu, hawakuifikia. ³² Kwa sababu gani? Kwa sababu walitafuta haki ile, si kwa njia ya imani, lakini kwa njia ya matendo. Walijikwaa juu ya lile jiwe la kukwalisha, ³³ kama ilivyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Angalia, ninaweka jiwe la kukwalisha katika Sayuni nalo ni la kuangusha. Lakini yule anayemwamini hatapata haya.»

Chapter 10

¹ Wandugu zangu, kitu ninachotamani kwa moyo wote nami ninachomwomba Mungu kwa ajili ya Waisraeli, ni kwamba waokolewe. ² Kwa maana ninashuhudia kwamba wanajitoa kwa bidii kutumikia Mungu, lakini bidii ile haitokani na ufahamu wa kweli. ³ Hawakufahamu namna Mungu anavyowahesabia watu haki na wakatafuta kusimamisha haki yao wenyewe. Wakakataa kufuata njia ya kuhesabiwa haki mbele ya Mungu. ⁴ Kwa maana kwa njia ya Kristo, Sheria imepata kufikia ukomo wake kusudi kila mtu anayeamini apate kuhesabiwa haki mbele ya Mungu. ⁵ Haya ndiyo mambo Musa aliyoandika juu ya kuhesabiwa haki mbele ya Mungu kwa njia ya kushika Sheria: «Mtu anayetimiza maagizo ya Sheria, ataishi kwa njia yake. ⁶ Lakini hivi ndivyo inavyosemwa juu ya kuhesabiwa haki kwa njia ya imani: “Usijiulize moyoni: Ni nani atakayepanda mbinguni?” (maana yake ni kumushusha Kristo toka kule.) ⁷ Wala usijiulize: “Ni nani atakayeshuka katika kuzimu?” (maana yake kumupandisha Kristo toka kule kwenye wafu). ⁸ Lakini inasemwa namna gani? “Neno la Mungu liko karibu nawe, liko ndani ya kinywa chako na ndani ya moyo wako.” Neno hili ni ujumbe tunaohubiri juu ya imani. ⁹ Kama ukiitikia kwa kinywa chako mwenyewe kwamba Yesu ni Bwana na kuamini katika moyo wako kwamba Mungu alimufufua, utaokolewa. ¹⁰ Kwa maana mtu akiamini kwa moyo wake, Mungu anamuhesabia haki mbele yake; naye anapoitikia kwa kinywa chake, anaokolewa. ¹¹ Kwa maana Maandiko Matakatifu yanasema: “Kila mtu anayemwamini hatapata haya.” ¹² Basi hakuna tofauti kati ya Wayuda na Wagriki, kwa maana Bwana wa wote ni mmoja tu, na anawabariki sana wote wanaomusihi. ¹³ Ni kama vile Maandiko Matakatifu yanavyosema: “Kila mtu anayemusihi Bwana, ataokolewa.” ¹⁴ Basi namna gani watamusihii yule wasiyemwamini? Na namna gani watamwamini yule wasiyesikia habari zake? Na namna gani watasikia habari zake ikiwa hakuna wanaohubiri? ¹⁵ Na namna gani watahubiri ikiwa hawatumwi? Ni kama inavyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: “Angalia jinsi kunavyofurahisha kuja kwa wale wanaoleta habari njema.” ¹⁶ Lakini wote hawakukubali ile Habari Njema. Kwa maana Isaya, alisema: “Ee Bwana, ni nani aliyeamini habari tulizotangaza?” ¹⁷ Hivi basi imani inatokana na kusikia habari, na habari ile inatokana na neno la Kristo. ¹⁸ Basi ninauliza: hawakusikia habari hii? Ndiyo, wameisikia! Kwa maana Maandiko Matakatifu yanasema: “Sauti yao imesikilika katika dunia yote, maneno yao yamefika pande zote za dunia.” ¹⁹ Ninauliza tena: Waisraeli hawakufahamu kitu? Kwanza Musa alikuwa amekwisha kujibu: “Nitawafanya kuwa na wivu juu ya watu wasiokuwa taifa. Nitawakasirisha ninyi kwa njia ya taifa pumbavu.” ²⁰ Isaya kwa uhodari anaongeza kusema maneno haya: “Nimepatikana kwa watu wasionitafuta, nimejifunua kwa watu wasioniuliza.” ²¹ Lakini juu ya Waisraeli anasema hivi: “Muchana kutwa ninanyoosha mikono yangu kwa kuita taifa lenye uasi na ubishi.”»

Chapter 11

¹ Basi ninauliza: Mungu amewatupilia watu wake? Hapana hata kidogo! Maana kwa ngambo yangu, mimi ni Mwisraeli wa uzao wa Abrahamu, toka kabila la Benjamina. ² Mungu hakuwakataa watu wake aliojichagulia tangu mbele. Munakumbuka Maandiko Matakatiifu yanayosema juu ya mashitaki ya Elia mbele ya Mungu juu ya Waisraeli? Yeye alisema: ³ «Bwana, wamewaua manabii wako na kubomoa mazabahu zako; nami nimebaki peke yangu, nao wanatafuta kuniua. ⁴ Lakini Mungu alimujibu namna gani? Alimwambia: “Nimejiwekea watu elfu saba waliokataa kupiga magoti mbele ya mungu Bali.”» ⁵ Ni hivi vilevile kwa wakati huu wa sasa kunabaki wamoja ambao Mungu alichagua kwa neema yake. ⁶ Na ikiwa walichaguliwa kwa neema ya Mungu, si kufuatana na matendo. Ingekuwa vile, neema isingekuwa neema tena. ⁷ Nini basi? Taifa la Waisraeli halikupata kile walichokitafuta. Ni wachache tu ambao Mungu aliwachagua ndio waliokipata. Lakini wengine waliobaki, walifanywa kuwa wagumu, ⁸ kama vile ilivyoandikwa katika Maandiko Matakatiifu: «Mungu ameifanya mioyo yao kuwa migumu, macho yao yasipate kuona na masikio yao yasipate kusikia, na ni hivi wanavyokuwa hata leo. ⁹ Daudi anasema vilevile: “Karamu ziwageukie kama mitego ya kuwanasa, waanguke na kuazibiwa. ¹⁰ Macho yao yatiwe giza wasione, na migongo yao ikunjame siku zote.”» ¹¹ Basi ninauliza: Waisraeli wamejikwaa hata wakaanguka kabisa? Hapana hata kidogo! Lakini kutokana na kosa la Waisraeli, watu wa mataifa mengine wamepata kuokolewa, kusudi wayasikilie wivu. ¹² Kosa lao limeiletea dunia baraka nyingi, na upungufu wao umeleta baraka nyingi kwa watu wa mataifa mengi. Basi haitaleta baraka zaidi sana wakati Waisraeli wote watakapookoka? Kuokolewa kwa mataifa mengine ¹³ Sasa ninasema na ninyi watu wa mataifa mengine. Nami ninafurahia kazi yangu, kwa kuona nimetumwa kuwa mutume wa watu wa mataifa. ¹⁴ Kwa sababu hii ninaweza kuwafanya watu wa taifa langu wawasikilie wivu, hata nipate kuwaokoa wamoja kati yao. ¹⁵ Kwa maana ikiwa kukataliwa kwao na Mungu kumeleta upatanisho kati yake na dunia, basi si hakika kwamba kukubaliwa kwao na Mungu kutaleta uzima kwa wale waliokufa. ¹⁶ Donge la kwanza la unga wenye kupondwa likitolewa kwa Mungu, mikate itakuwa yake vilevile. Na kama shina la muti likitolewa kwa Mungu, matawi yatakuwa yake vilevile. ¹⁷ Matawi mamoja ya muzeituni uliopandwa yamekatwa, na chipukizi la muzeituni uliojitesha katika pori umepandikizwa kwenye nafasi yao. Na sasa unafaidia vilevile utomvu unaotoka ndani ya shina la yule muzeituni uliopandwa. ¹⁸ Basi musizarau yale matawi yaliyokatwa. Ninyi hamuna cha kujivunia, kwa maana si ninyi munaoshikilia shina, lakini ni shina linalowashikilia. ¹⁹ Labda utaweza kuniambia: «Matawi yale yalikatwa kusudi mimi nipandikizwe kwenye nafasi yao.» ²⁰ Unasema ukweli. Yamekatwa kwa sababu yalikataa kuamini na wewe unasimama imara katika imani yako. Sasa usijivune, lakini uogope! ²¹ Kwa maana ikiwa Mungu hakuachilia yale matawi ya asili kuendelea kukomaa, namna gani atakuachilia wewe? ²² Basi ufikiri juu ya wema wa Mungu na ukali wake vilevile. Yeye ni mukali kwa wale walioanguka, lakini yeye ni mwema kwako, ikiwa utaendelea katika wema wake. Kama si vile, wewe vilevile utakatwa. ²³ Na kama Wayuda wasipoendelea kukataa kuamini, watapandikizwa kwenye nafasi ile walipokuwa mbele, kwa maana Mungu yuko na uwezo wa kuwapandikiza tena. Ninyi watu wa mataifa mengine ni kama tawi la muzeituni wa pori lililokatwa na kisha likapandikizwa ndani ya muzeituni uliopandwa, umbalimbali na kawaida. ²⁵ Wandugu zangu, sitaki mukose kujua siri hii, kusudi musijione kuwa wenye akili sana. Siri ile ni hii: Waisraeli wamoja wataendelea kuwa wagumu mpaka watu wa mataifa mengine kwa jumla watakapokuja kwa Mungu. ²⁶ Na halafu taifa lote la Israeli litaokolewa kama vile inavyoandikwa katika Maandiko Matakatiifu: «Mukombozi atatokea Sayuni, atakomesha uovu kati ya wazao wa Yakobo. ²⁷ Na hili ndilo agano nitakalofanya nao, wakati nitakapowasamehe zambi zao.» ²⁸ Wayuda wamegeuka waadui za Mungu kwa sababu ya kukataa Habari Njema, na jambo hilo limekuwa faida kwenu ninyi watu wa mataifa mengine. Lakini wao ni wapendwa wake kufuatana na vile wamechaguliwa naye, kwa njia ya babu zao. ²⁹ Kwa maana Mungu habadilishi mafikiri juu ya zawadi anazotoa, wala juu ya wale anaowachagua. ³⁰ Zamani ninyi mulimwasi Mungu, lakini sasa amewahurumia kutokana na uasi wa Wayuda. ³¹ Ni hivi vilevile, kutokana na vile mulivyohurumiwa, sasa wao wanamwasi Mungu, kusudi wao vilevile wapate kuhurumiwa na Mungu. ³² Maana Mungu amewafanya watu wote kama wafungwa kwa sababu ya kuasi kwao, kusudi awahurumie wote. ³³ Utajiri wa Mungu, hekima na ufahamu wake ni vikubwa kupita kipimo! Hakuna anayeweza kuvumbua kusudi lake wala kuelewa mipango yake! ³⁴ Kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema: «Ni nani anayejua mafikiri ya Bwana? Ni nani anayeweza kuwa mushauri wake? ³⁵ Ni nani anayeweza kumupa Mungu kitu kwanza, kusudi naye apate kumurudishia?» ³⁶ Kwa maana vitu vyote vinatoka kwake, navyo viko kwa uwezo wake na kwa ajili yake. Atukuzwe hata milele! Amina.

Chapter 12

¹ Basi wandugu zangu, kufuatana na vile Mungu alivyoonyesha huruma yake kwetu, ninawasihi mujitoe wenyewe kwake kuwa sadaka yenye uzima, takatifu na yenye kumupendeza. Hii ndiyo njia ya kweli ya kumwabudu. ² Musifuata mwenendo wa siku hizi, lakini muache Mungu awabadilishe kwa kugeuza upya nia zenu, hata mukuwe na mawazo mapya. Kwa hiyo mutaweza kutambua mapenzi ya Mungu. ³ Kufuatana na neema niliyopewa na Mungu, ninawaambia ninyi wote: mtu asijiwazie kuwa na ukubwa kupita vile inavyomustahili. Lakini mukuwe na mawazo ya ukadirifu, kila mmoja kulingana na kipimo cha imani aliyopewa na Mungu. ⁴ Katika mwili mmoja kuna viungo vingi, lakini viungo hivi vyote havina kazi moja. ⁵ Hivi vilevile, sisi tunaokuwa wengi tumekuwa mwili mmoja katika kuungana kwetu na Kristo, na sisi wote ni viungo kila mmoja kwa mwingine. ⁶ Tuko na zawadi mbalimbali kwa kadiri ya neema tuliyopewa na Mungu. Aliyepewa zawadi ya unabii, anapaswa kutabiri kwa kadiri ya imani yake. ⁷ Aliyepewa zawadi ya utumishi, atumike. Aliyepewa zawadi ya kufundisha, afundishe. ⁸ Aliyepewa zawadi ya kuonya wengine, awaanye. Aliyepewa zawadi ya kutoa, atoe kwa moyo mweupe. Anayesimamia wengine, awasimamie kwa bidii. Aliyepewa zawadi ya kuhurumia wengine, afanye vile kwa furaha. ⁹ Upendo wenu ukuwe pasipo udanganyifu. Muchukie chochote kinachokuwa kibaya, mushikamane na kinachokuwa chema. ¹⁰ Mupendane ninyi kwa ninyi kwa kweli kama vile wandugu, nanyi muheshimiane ninyi kwa ninyi. ¹¹ Musikuwe wavivu katika kazi lakini mukuwe na bidii rohoni, mukimutumikia Bwana kwa juhudi. ¹² Mufurahi mukiwa na tumaini, muvumilie katika mateso, mudumu katika kuomba. ¹³ Muwasaidie watu wa Mungu katika mahitaji yao na muwakaribishe wageni. ¹⁴ Mumwombe Mungu awabariki wale wanaowatesa; muwaombee baraka wala musiwalaani. ¹⁵ Mufurahi pamoja na wenye kufurahi. Mulie pamoja na wenye kulia. ¹⁶ Mukuwe na masikilizano kati yenu. Musikuwe na nia ya kujitukuza, lakini mukubali kuishi katika unyenyekevu. Musijiwazie kuwa wenye akili sana. ¹⁷ Musimurudishie mtu ubaya kwa ubaya. Mukuwe na roho ya kufanya mema mbele ya watu wote. ¹⁸ Kama ikiwezekana, kwa upande wenu, muishi katika amani na watu wote. ¹⁹ Wandugu wapendwa, musilipize kisasi ninyi kwa ninyi, lakini mumwachie Mungu wakati wa kutenda kufuatana na kasirani, maana imeandikwa katika Maandiko Matakatiifu: «Ni kazi yangu kulipiza kisasi. Ni mimi nitakayelipiza. ²⁰ Lakini kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema: “Adui yako akisikia njaa, umupe chakula; kama akisikia kiu, umupe kinywaji. Maana kwa kufanya hivi utamupatisha haya kama vile ungemubebesha makaa ya moto juu ya kichwa.”» ²¹ Usijiachilie kushindwa na ubaya, lakini ushinde ubaya kwa kutenda mema.

Chapter 13

¹ Kila mtu anapaswa kutii wakubwa wenye mamlaka. Maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; nao wakubwa wanaotawala wamesimikwa na Mungu. ² Kwa hiyo yeye anayepingana na mwenye mamlaka anapinga amri ya Mungu, nao wanaofanya vile wanajiletea azabu wenyewe. ³ Kwa maana wanaofanya mema hawaogopi watawala, lakini wale wanaofanya mabaya. Unataka kuishi bila kumwogopa mwenye mamlaka? Basi fanya mema naye atakusifu, ⁴ maana yeye anamutumikia Mungu kwa faida yako. Lakini kama ukifanya mabaya, umwogope kwa sababu yeye yuko na uwezo kwa kuazibu. Yeye anamutumikia Mungu wa kuazibu wale wanaofanya mabaya. ⁵ Kwa sababu hii ni lazima kuwatii wenye mamlaka, si kwa sababu ya kuogopa azabu ya Mungu tu, lakini tena kwa sababu ya kusongwa na zamiri. ⁶ Kwa sababu hii vilevile munalipa kodi, maana watawala wanamutumikia Mungu wakijitoa kwa kazi ile. ⁷ Mumupe kila mtu haki yake: mulipishaji wa kodi, mumulipe kodi; mulipishaji wa ushuru, mumulipe ushuru. Mumuheshimu anayestahili kuheshimiwa na mumutukuze anayestahili kutukuzwa. ⁸ Musikuwe na deni la mtu yeyote. Deni moja munalopaswa kuwa nalo ni kupendana. Kwa maana yule anayemupenda mwenzake ametimiza Sheria kabisa. ⁹ Kwa hiyo amri hizi: «Usizini, usiue, usiibe, usitamani, pamoja na zingine zote, zinafungwa katika amri hii moja: “Umupende mwenzako sawa vile unavyojipenda mwenyewe.”» ¹⁰ Anayemupenda mwenzake hawezi kumutendea vibaya. Basi Sheria inatimizwa kwa njia ya upendo. ¹¹ Mufanye vile, maana munajua tunaishi katika siku gani sasa. Saa ya kuamuka katika usingizi wenu imetimia, kwa maana sasa wakati wetu wa kuokolewa unakaribia kuliko vile ilivyokuwa wakati tulipoanza kuamini. ¹² Usiku umepita, na muchana unakaribia. Basi tutupilie mbali matendo ya giza na kuvaa silaha za kupigana nazo wakati wa mwangaza. ¹³ Tukuwe na mwenendo mzuri unaostahili wakati wa muchana, tukijilinda na ulafi na ulevi, uasherati na uzinzi, magombano na wivu. ¹⁴ Lakini Bwana Yesu Kristo akuwe kama vile silaha munayobeba, musijiachilie kuvutwa na hali yenu ya kimwili hata mutimize tamaa zake.

Chapter 14

¹ Mumupokee yule anayekuwa zaifu katika imani pasipo kubishana naye juu ya mawazo yake. ² Kwa mufano, mtu mmoja kutokana na imani yake anaona kwamba anaweza kula kila chakula, lakini mwingine kutokana na imani yake zaifu, anakula tu mboga za majani. ³ Yule anayekula kila chakula asimuzarau yule asiyekula kila chakula. Vilevile yule asiyekula kila chakula asimuhukumu yule anayekikula, kwa maana Mungu amemupokea. ⁴ Wewe ni nani unayehukumu mtumishi wa mwingine? Akisimama imara katika kazi yake au akianguka, hilo ni shauri la bwana wake. Naye atasimama imara maana Bwana yuko na uwezo wa kumusimamisha. ⁵ Watu wamoja wanahesabu siku fulani kuwa yenye maana zaidi kuliko siku zingine, lakini wengine wanahesabu siku zote kuwa sawasawa. Kwa hiyo kila mtu asadiki sawa vile anavyowaza yeye mwenyewe. ⁶ Mtu yeyote anayeshugulika juu ya siku fulani, anafanya hivi kwa kumutukuza Bwana. Yule anayekula kila chakula, anafanya vile kwa kumutukuza Bwana; maana anamushukuru Mungu kwa ajili ya chakula chake. Na asiyekula kila chakula anafanya hivi vilevile kwa kumutukuza Bwana na kumushukuru Mungu. ⁷ Kwa maana hakuna hata mtu mmoja kati yetu anayeishi kwa ajili yake mwenyewe, wala hakuna anayekufa kwa ajili yake mwenyewe. ⁸ Maana kama tunaishi, tunaishi kwa ajili ya Bwana, na kama tunakufa, tunakufa kwa ajili ya Bwana. Basi ikiwa tunaishi, au ikiwa tunakufa, sisi ni watu wa Bwana. ⁹ Ni kwa sababu hii Kristo alikufa na kufufuka kusudi apate kuwa Bwana wa waliokufa na wa wanaokuwa wazima vilevile. ¹⁰ Lakini wewe, kwa sababu gani unamuhukumu ndugu yako? Au wewe kwa sababu gani unamuzarau ndugu yako? Maana sisi wote tutasimama kwa kusambishwa mbele ya tribinali ya Mungu. ¹¹ Kwa maana imeandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Bwana anasema: “Kama vile ninavyoishi, kila mtu atapiga magoti mbele yangu, na kila mtu ataitikia kwamba mimi ni Mungu.”» ¹² Kwa hiyo kila mmoja kati yetu atajitetea mwenyewe kwa Mungu. Usimukoseshe ndugu yako ¹³ Basi tusihukumiane tena sisi wenyewe. Lakini tafazali mukamate kusudi hili: mtu asifanye kitu kinachoweza kumukwaza au kumwangusha ndugu yake katika zambi. ¹⁴ Kufuatana na vile ninaungana na Bwana Yesu, ninajua hakika kwamba hakuna kitu kinachohesabiwa kichafu katika hali yake ya asili. Lakini kama mtu akihesabu kwamba kitu fulani ni kichafu, basi kitu kile ni kichafu kwake. ¹⁵ Kama ukimuhuzunisha ndugu yako kwa sababu ya chakula unachokula, wewe hautendi tena kufuatana na upendo. Kwa njia ya chakula chako usimupoteze mtu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake. ¹⁶ Basi musikubali kitu kile kinachoonekana kwenu kuwa kizuri kizarauliwe. ¹⁷ Kwa maana kazi ya Ufalme wa Mungu si kushugulika na mambo ya kula na kunywa, lakini ni kushugulika na haki, amani na furaha vinavyotolewa na Roho Mtakatifu. ¹⁸ Na yeyote anayemutumikia Kristo kwa njia hiyo anamupendeza Mungu, naye anapata kuwa mwenye kustahili mbele ya watu. ¹⁹ Basi kwa hiyo tujikaze sana kufanya mambo yale yanayoleta amani na yanayotusaidia kujengana katika imani. ²⁰ Usiharibu kazi ya Mungu kwa sababu ya maneno ya chakula. Hakika vyakula vyote vinaruhusiwa kukuliwa, lakini ni vibaya kwa mtu kula chakula kinachoweza kukwaza mwingine. ²¹ Ni vema kuacha kula nyama, kunywa divai na kujizuiza kufanya chochote kinachoweza kumukwaza ndugu yako. ²² Ulinde kwa ajili yako mwenyewe kile unachoaminia juu ya mambo yale mbele ya Mungu. Heri mtu asiyejihukumu katika kusudi lake. ²³ Lakini mtu anayekuwa na mashaka juu ya chakula anachokula, Mungu anamuhukumu, kwa sababu hatendi kufuatana na imani. Na kitendo chochote kisichotokana na imani ni zambi.

Chapter 15

¹ Sisi tunaokuwa na nguvu katika imani tunapaswa kubeba muzigo wa uzaifu wa wale wasiokuwa na nguvu. Tusifanye tu mambo yanayotupendeza wenyewe. ² Lakini kila mmoja wetu anapaswa kumupendeza mwingine kwa kumutendea mema na kuweza hivi kumujenga katika imani. ³ Kwa maana hata Kristo hakufanya mambo yanayomupendeza mwenyewe sawa vile ilivyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Matusi wanayokutukana, yananiangukia.» ⁴ Na yote yaliyoandikwa zamani katika Maandiko Matakatifu yameandikwa kwa ajili ya kutufundisha sisi, kusudi tuendeleo kuchunga tumaini kwa njia ya kuvumilia na kufarijiwa sawa tunavyofundishwa katika Maandiko Matakatifu. ⁵ Basi, Mungu anayewapa watu nguvu ya kuvumilia na kufarijika awape kuwa na nia moja mukifuata mufano wa Kristo Yesu. ⁶ Hivi kusudi mutaweza kwa nia moja na kwa sauti moja kumutukuza Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Habari Njema kwa watu wote ⁷ Basi mupokeane kwa upendo sawa vile Kristo alivyotupokea kusudi Mungu apate kutukuzwa. ⁸ Kwa maana ninawaambia wazi kwamba Kristo alifanya utumishi kwa ajili ya Wayuda kwa kuhakikisha kuwa Mungu ni mwaminifu na kusudi atimize ahadi zile babu zetu walizopewa. ⁹ Vilevile ilikuwa kusudi watu wa mataifa mengine wamutukuze Mungu kwa huruma yake, kama inavyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Kwa hiyo nitakutukuza kati ya mataifa, nitakuambia sifa. ¹⁰ Na tena Maandiko yanasema: “Ninyi watu wa mataifa yote mufurahi pamoja na taifa lake!” ¹¹ Na tena hivi: “Enyi mataifa yote, mumusifu Bwana; enyi watu wote, mumusifu!” ¹² Isaya naye anasema: “Muzao wa Yese atatokea, atatawala watu wa mataifa, nao watamutumainia.”» ¹³ Basi, Mungu anayekuwa musingi wa matumaini, awajaze furaha kamili na amani kutokana na imani yenu; hata tumaini lenu lipate kuongezeka kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. ¹⁴ Wandugu zangu, kwa ngambo yangu ninajua hakika kwamba ninyi munajaa wema, nanyi munafahamu yote yanayofaa na munaweza kushauriana vizuri. ¹⁵ Lakini mara moja moja nimewaandikia kwa uhodari juu ya mambo fulani kusudi niwakumbushe tena mambo yale. Nimefanya vile kutokana na neema ile niliyopewa na Mungu ¹⁶ kuwa mtumishi wa Yesu Kristo kwa watu wa mataifa mengine. Ninafanya kazi ya ukuhani ya kuhubiri Habari Njema ya Mungu, kusudi watu wa mataifa mengine wapate kuwa kama sadaka inayokubaliwa na Mungu na iliyotakaswa na Roho Mtakatifu. ¹⁷ Basi katika kuungana kwangu na Kristo Yesu, ninaweza kujisifu kwa ajili ya kazi hii ninayomutumikia Mungu. ¹⁸ Kwa maana sitasubutu kuongeza kitu kingine, isipokuwa tu kile Kristo alichotimiza kwa njia yangu kusudi watu wa mataifa wapate kumutii Mungu. Alifanya vile kwa njia ya yale aliyoniwezesha kusema na kutenda, ¹⁹ kwa njia ya uwezo wa vitambulisho na maajabu, na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Hivi tokea Yerusalema mpaka kufika katika jimbo la Iliriko nimehubiri fasi zote Habari Njema ya Kristo. ²⁰ Nayo nia moja niliyokuwa nayo ni kuhubiri tu Habari Njema fasi zote ambapo habari za Kristo zilipokuwa hazijasikilika bado. Nilikusudia vile kusudi nisijenge juu ya musingi uliowekwa na mtu mwingine, ²¹ kama vile inavyoandikwa katika Maandiko Matakatifu: «Wale ambao hawajaambiwa bado habari zake, watamwona. Wale hawajazielezwa bado, watazifahamu.» ²² Hiyo ndiyo sababu iliyonizuiza mara nyingi kufika kule kwenu. ²³ Lakini kwa sasa nimemaliza kazi yangu katika pande hizi za inchi, na tena tangu miaka mingi nina hamu sana ya kuja kuwaona; ²⁴ kwa hiyo nitawafikia nitakapokwenda Spania. Ninatumaini kupitia kule na kuonana nanyi, na kisha kufurahi kwanza pamoja nanyi kwa muda mufupi, ningetamani kupata musaada wenu kwa ajili ya safari ile. ²⁵ Lakini sasa ninakwenda kwanza Yerusalema kuwasaidia watu wa Mungu kule. ²⁶ Kwa maana imependeza makanisa ya Makedonia na ya Akaya kukusanya mali kwa kuwasaidia wamasikini wanaokuwa kati ya watu wa Mungu kule Yerusalema. ²⁷ Ndiyo wamefanya vile kwa mapenzi yao, lakini vilevile ilikuwa mapaswa kwao kuwasaidia. Kwa maana ikiwa watu wa mataifa wameshirikiana baraka za kiroho na Wayuda, imewapasa watu wa mataifa mengine kuwasaidia Wayuda katika mahitaji ya kimwili. ²⁸ Basi nitakapomaliza kazi ile na kuwafikishia mali iliyokusanywa, nitapitia kwenu, nikiwa katika safari yangu ya kwenda Spania. ²⁹ Nami ninajua kwamba wakati nitakapokuja kwenu, nitakuja na baraka nyingi sana kutoka kwa Kristo. ³⁰ Wandugu zangu, ninawasihi kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo na kwa ajili ya upendo unaoletwa na Roho wa Mungu, muungane nami kwa kuniombea kwa Mungu. ³¹ Muniombe kusudi nisipate hasara toka kwa watu wale wasioamini wanaokuwa Yudea na kusudi musaada ninaoupeleka Yerusalema upate kupokelewa vizuri kule na watu wa Mungu. ³² Na hivi Mungu akitaka, nitakuja kwenu kwa furaha, nami nitapata kutulizwa moyo kati yenu. ³³ Basi Mungu anayeleta amani akuwe pamoja nanyi wote. Amina!

Chapter 16

¹ Ninawatumia dada yetu mwamini Foibe, anayekuwa musaidizi wa kanisa la Kenkurea. ² Mumupokee kwa ajili ya Bwana, kama vile watu wa Mungu wanavyopaswa kufanya. Mumusaidie katika kila jambo atakalohitaji toka kwenu, maana yeye amewasaidia watu wengi na hata mimi peke yangu vilevile nimeshuhudia. ³ Munisalimie Prisila na Akila, watumishi wenzangu katika kazi ya Yesu Kristo. ⁴ Wao walijitolea kufa kwa kuokoa maisha yangu. Ninawashukuru, wala si mimi peke yangu tu, nayo makanisa yote ya inchi za watu wa mataifa wanawashukuru vilevile. ⁵ Munisalimie vilevile kanisa linalokusanyika katika nyumba yao. Munisalimie mupendwa wangu Epeneto, anayekuwa mwamini wa kwanza wa Kristo katika jimbo la Azia. ⁶ Munisalimie Maria, aliyewashugulikia sana. ⁷ Munisalimie wanainchi wenzangu Androniko na Yunia, waliofungwa pamoja nami katika kifungo. Wao wanasifiwa sana kati ya mitume, nao walikuwa katika Kristo mbele yangu. ⁸ Munisalimie Ampuliato, mupendwa wangu katika Bwana. ⁹ Munisalimie Urbano, mtumishi mwenzetu katika kazi ya Kristo, na Staki, mupendwa wangu. ¹⁰ Munisalimie Apele, aliyehakikisha uaminifu wake katika Kristo. Munisalimie watu wanaoishi katika nyumba ya Aristobulo. ¹¹ Munisalimie Herodio, mwanainchi mwenzangu. Munisalimie watu wanaoishi katika nyumba ya Narkiso, wanaomwamini Bwana. ¹² Munisalimie Tirifena na Tirifosa, wale wanawake wanaomushugulikia Bwana, na mupendwa wangu Persi, aliyemushugulikia sana Bwana. ¹³ Munisalimie Rufo, mtumishi hodari katika kazi ya Bwana, na mama yake ninayemuhesabu kama mama yangu vilevile. ¹⁴ Munisalimie Asinkristo, Fulego, Herme, Patroba, Herma, na wandugu wanaoshiriki pamoja nao. ¹⁵ Munisalimie Filologo na Yulia, Nereo na dada yake, na Olimpa, na watu wote wa Mungu wanaoshiriki pamoja nao. ¹⁶ Musalimiane kwa upendo wa kikristo. Makanisa yote ya Kristo yanawasalimia. ¹⁷ Wandugu zangu, ninawasihi, mufanye angalisho na wale wanaoleta matengano na mambo ya kuwapotosha wengine wakipinga mafundisho muliyopokea. Mujitenge mbali nao. ¹⁸ Kwa maana watu wa namna hii hawamutumikii Bwana wetu Yesu Kristo, lakini wanatumikia tu tumbo yao wenyewe. Tena kwa maneno yao matamu na ya kujipendekeza wanadanganya mioyo isiokuwa na makosa. ¹⁹ Watu wote wanajua namna munavyomutii Bwana, na kwa sababu hii ninafurahi kwa ajili yenu. Lakini ninataka mukuwe wenye hekima kwa kutenda mema, na mukuwe safi mukijitenga na mambo mabaya. ²⁰ Mungu, anayeleta amani, atamupondaponda sasa hivi Shetani chini ya miguu yenu. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo ikuwe pamoja nanyi. ²¹ Timoteo, mtumishi mwenzangu anawasalimia, nao Lukio, Yasoni, na Sosipateri, wanainchi wenzangu wanawasalimia vilevile. ²² Mimi Tertio, niliyeandika barua hii, ninawasalimia kwa jina la Bwana. ²³ Gayo, aliyenikaribisha na anayekaribisha kanisa zima kwa kukusanyika kwake, anawasalimia. Erasto, mulinzi wa mali ya mji, pamoja na ndugu yetu Kwarto, wanawasalimia. [²⁴ Tunawataki ninyi wote neema kutoka kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Amina.] ²⁵ Mungu asifiwe! Yeye yuko na uwezo wa kuwaimarisha katika imani juu ya Habari Njema ninayotangaza kwa kuhubiri ujumbe juu ya Yesu Kristo, kufuatana na ufunuo wa siri iliyofichwa tangia zamani za kale na kale. ²⁶ Lakini sasa yamefunuliwa na maandiko ya manabii kufuatana na amri ya Mungu wa milele, kusudi mataifa yote yapate kumwamini na kumutii. ²⁷ Basi Mungu anayekuwa peke yake mwenye hekima atukuzwe milele na milele kwa njia ya Yesu Kristo! Amina.

Book: 1 Corinthians

1 Corinthians

Chapter 1

¹ Barua hii inatoka kwangu mimi Paulo na kwa ndugu yetu Sositeni. Ni mimi niliyeitwa na Mungu kwa mapenzi yake kuwa mutume wa Kristo Yesu. ² Tunawaandikia ninyi kanisa la Mungu linalokuwa Korinto, ninyi ambao mumetakaswa kwa njia ya kuungana kwenu na Yesu Kristo na mumeitwa na Mungu kuwa watu wake. Vilevile barua hii ni kwa wote wanaoabudu jina la Bwana Yesu Kristo fasi zote, anayekuwa Bwana wao na Bwana wetu vilevile. ³ Tunawatakia neema na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. ⁴ Ninamushukuru Mungu wangu siku zote kwa ajili yenu, kwa sababu ya neema Mungu aliyowapa ninyi kwa njia ya Yesu Kristo. ⁵ Kwa maana katika kuungana kwenu na Kristo, mumejaliwa katika vitu vyote, zaidi sana katika mambo yanayoelekea masemi na ufahamu. ⁶ Ile inatokana na vile ujumbe juu ya Kristo umehakikishwa kwa nguvu kati yenu, ⁷ hata hamukosewi zawadi yoyote ya Mungu, mukiwa muingojewa wakati Bwana wetu Yesu Kristo atakapoonekana. ⁸ Ni yeye atakayewasimamisha ninyi imara mpaka mwisho kusudi musishitakiwe juu ya kosa lolote Siku ile ya kurudi kwa Bwana wetu Yesu Kristo. ⁹ Mungu ni mwaminifu katika ahadi zake, yeye aliyewaita ninyi muishi katika ushirika pamoja na Mwana wake Yesu Kristo, Bwana wetu. ¹⁰ Wandugu zangu, ninawasihi ninyi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, mukuwe na masikilizano kusudi matengano yasikuwe katikati yenu. Muishi katika umoja kabisa mukiwa na nia moja na wazo moja. ¹¹ Kwa maana, wandugu zangu, nimepata habari zenu kwa njia ya jamaa ya Kloe kwamba kuko ugomvi katikati yenu. ¹² Ninataka kusema: kila mmoja kati yenu anasema maneno yake mbalimbali. Mmoja anasema: «Mimi ni wa Paulo, mwingine anasema: «Mimi ni wa Apolo,” mwingine anasema: «Mimi ni wa Petro,” na mwingine anasema: «Mimi ni wa Kristo.”» ¹³ Munafikiri kwamba Kristo amegawanyika? Paulo ndiye aliyetundikwa juu ya musalaba kwa ajili yenu? Au mumebatizwa kwa jina la Paulo? ¹⁴ Ninamushukuru Mungu kuwa sikubatiza hata mmoja wenu isipokuwa Krispo na Gayo. ¹⁵ Hivi hakuna anayeweza kusema kwamba amebatizwa kwa jina langu. ¹⁶ Ni kweli, nilibatiza vilevile jamaa ya Stefano, zaidi ya wale sikumbuki kama nilibatiza mtu mwingine. ¹⁷ Kristo hakunituma kwa kubatiza, lakini amenituma kwa kutangaza Habari Njema. Amenituma kuitangaza bila kutumia hekima ya usemi, kusudi uwezo unaotokana na kufa kwa Kristo juu ya musalaba usihesabiwe kuwa bure. ¹⁸ Hivi, mahubiri ya kufa kwa Kristo juu ya musalaba yanahesabiwa kuwa upumbavu kwa wale wanaopotea. Lakini kwa sisi tunaokolewa ni uwezo wa Mungu. ¹⁹ Kwa maana Maandiko Matakatiifu yanasema: «Nitaharibu hekima ya wenye hekima, Nitapoteza akili ya wenye akili.» ²⁰ Basi, tuseme nini juu ya wenye hekima, walimu wa Sheria, nao wafundi wa usemi siku hizi? Mungu ameonyesha wazi kwamba hekima ya dunia hii ni upumbavu! ²¹ Mungu alikusudia kuwaokoa wale wanaomwamini kwa njia ya mahubiri tunayotangaza yanayoonekana kuwa mambo ya upumbavu. Amefanya vile kwa sababu, kwa njia ya hekima yao ya kimtu, watu hawakumutambua Mungu na hekima yake ya kimungu. ²² Wayuda wanaomba kuonyeshwa vitambulisho nao Wagriki wanatafuta hekima. ²³ Lakini sisi tunamuhubiri Kristo aliyetundikwa juu ya musalaba, na mahubiri hayo yanahesabiwa kama kikwazo kwa Wayuda na upumbavu kwa watu wa mataifa mengine. ²⁴ Lakini kwa wale walioitwa na Mungu, ikiwa Wayuda au Wagriki, Kristo ni kitambulisho cha uwezo na hekima ya Mungu. ²⁵ Kwa maana mambo wanayomuhesabilia Mungu kuwa ya upumbavu, yanapita hekima ya watu; nayo mambo yale wanayomuhesabilia kuwa ya uzaifu yanapita nguvu za watu. ²⁶ Basi wandugu zangu, mukumbuke vile mulivyoitwa na Mungu, kwamba si wengi kati yenu wenye hekima kufuatana na mafikiri ya watu; si wengi kati yenu wanaokuwa wenye nguvu, wala wenye vyeo. ²⁷ Lakini Mungu anachagua vitu ambavyo watu wanahesabu kuwa vya upumbavu kusudi apatishe wenye hekima haya, naye amechagua vitu wanavyohesabu kuwa vya uzaifu kusudi apatishe wenye nguvu haya. ²⁸ Mungu amechagua vitu ambavyo watu wanahesabu kuwa vya hali ya chini na vyenye kuzarauliwa, visivyokuwa na maana mbele ya macho ya watu, kusudi aharihu vile wanavyohesabu kuwa vya lazima. ²⁹ Alifanya vile kusudi hata mtu mmoja asijivune mbele ya Mungu. ³⁰ Lakini Mungu amewaunganisha na Yesu Kristo, naye amemufanya Kristo kuwa hekima yetu. Kwa njia ya Kristo tunahesabiwa haki mbele ya Mungu, tumekuwa watu watakatiifu wa Mungu, na kukombolewa toka zambi zetu. ³¹ Kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema: «Anayetaka kujivuna, ajivune kwa ajili ya Bwana.»

Chapter 2

¹ Wandugu zangu, wakati nilipokuja kwenu kuwapasha habari ya siri ya Mungu, sikutumia maneno magumu wala hekima ya dunia. ² Kwa maana wakati nilipokuwa pamoja nanyi nilikusudia nisijue mambo mengine lakini Yesu Kristo tu na habari ya kufa kwake juu ya musalaba. ³ Sababu ya hii nilikuwa kwenu katika hali ya uzaifu na woga, mwenye kutetemeka sana. ⁴ Mafundisho yangu na mahubiri yangu hayakutolewa kwa maneno ya werevu na hekima ya kimtu, lakini katika onyesho la uwezo wa Roho wa Mungu, ⁵ kusudi imani yenu isikuwe katika hekima ya watu, lakini katika uwezo wa Mungu. ⁶ Ingawa vile, mimi ninatangaza mambo ya hekima kwa watu waliokomaa kiroho. Lakini mambo haya si ya hekima ya kidunia, wala ya watawala wa dunia hii watakaoangamizwa. ⁷ Ninatangaza hekima ya siri ya Mungu, hekima iliyofichwa kwa watu, na iliyopangwa na Mungu mbele ya kuumbwa kwa dunia kwa ajili ya utukufu wetu. ⁸ Hakuna hata mutawala mmoja kati ya watawala wa dunia hii aliyelewa hekima ile. Kama wangeielewa wasingemutundika Bwana wa utukufu juu ya musalaba. ⁹ Lakini ni kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema: «Mambo yale ambayo hakuna mtu aliyepata kuyaona wala kuyasikia, mambo yale ambayo hakuna mtu aliyepata kufikiri moyoni juu yake, ndiyo yale Mungu aliyowatayarishia wale wanaomupenda.» ¹⁰ Lakini Mungu ametufunulia sisi siri yake kwa njia ya Roho wake. Maana Roho anachunguza vitu vyote, hata mipango ya Mungu inayofichwa kabisa. ¹¹ Hakuna mtu anayeweza kujua mawazo ya mtu mwingine isipokuwa tu roho ya mtu inayokuwa ndani yake. Vilevile, hakuna anayejua mawazo ya Mungu isipokuwa Roho wa Mungu tu. ¹² Na sisi hatukupokea roho ya dunia hii, lakini tulipokea Roho anayetoka kwa Mungu, kusudi tupate kujua vitu vyote tulivyojaliwa kwa neema ya Mungu. ¹³ Nasi tunaposema hatutumii maneno yanayotokana na hekima ya kimtu, lakini maneno yanayotokana na Roho wa Mungu, tukieleza maneno ya kiroho kwa watu wanaokuwa wa Roho. ¹⁴ Lakini mtu anayefuata hali yake ya kidunia hawezi kukubali maneno yanayotoka kwa Roho wa Mungu. Kwa sababu anayaona kuwa ni upumbavu kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa maana yanatambulikana tu kwa njia ya Roho. ¹⁵ Mtu anayekuwa na Roho wa Mungu anahukumu mambo yote, lakini hakuna mtu anayeweza kumuhukumu. ¹⁶ Kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema: «Ni nani anayejua mawazo ya Bwana? Ni nani anayeweza kumushauria?» Lakini sisi tuko na mawazo yanayotoka kwa Kristo.

Chapter 3

¹ Kweli wandugu zangu, sikuweza kusema nanyi kama watu wanaotawaliwa na Roho wa Mungu, lakini kama watu wanaotawaliwa na mambo ya kidunia. Mungali kama watoto wachanga katika mambo ya Kikristo. ² Niliwanywesha maziwa, sikuwapa chakula kigumu, kwa maana mulikuwa hamujakiweza bado. Na hata sasa hamukiwezi, ³ kwa sababu mungali munatawaliwa na mambo ya kidunia. Kwa maana ikiwa kungali wivu na ugomvi katikati yenu, haionyeshi kwamba munatawaliwa na mambo ya kidunia, nanyi munaishi kufuatana na hali ya kimtu? ⁴ Wakati mmoja wenu anaposema: «Mimi ni wa Paulo na mwingine anasema: “Mimi ni wa Apolo,”» basi ninyi hamufanyi mambo ya kidunia? ⁵ Basi, Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Sisi ni watumishi wa Mungu, waliowaonyesha ninyi njia ya kuamini. Tumefanya vile kila mmoja wetu kwa kadiri ya zawadi aliyopewa na Bwana. ⁶ Mimi nilipanda mbegu na Apolo alinywesha maji, lakini Mungu ndiye aliyeyotesha. ⁷ Hivi yule anayepanda na yule anayenywesha maji, wote si kitu; Mungu ndiye anayekuwa wa lazima kwa maana ni yeye anayeyotesha mbegu. ⁸ Yule anayepanda na yule anayenywesha maji wote ni sawa; naye Mungu atamupa kila mtu mushahara wake kufuatana na kazi aliyofanya. ⁹ Kwa maana sisi tunashirikiana na Mungu katika kazi, na ninyi ni shamba la Mungu. Vilevile ninyi ni majengo ya Mungu. ¹⁰ Kwa kadiri ya zawadi Mungu aliyonipatia, kama vile fundi wa kujenga mwenye hekima, niliweka musingi. Na sasa, mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini inafaa kila mtu aangalie vizuri namna anavyojenga. ¹¹ Kwa maana hakuna mtu anayeweza kuweka musingi mwingine pahali pa ule uliokwisha kuwekwa, ni kusema Yesu Kristo. ¹² Mtu anaweza kujenga juu ya musingi huu na zahabu, feza, mawe ya bei kali, miti, nyasi au majani. ¹³ Lakini hali ya kazi ya kila mtu itaonekana wazi, kwa sababu Siku ile ya hukumu itaionyesha waziwazi. Kwa maana Siku ile itajitokeza katikati ya moto, na moto ule ndio utakaopima na kuonyesha hali ya kazi ya kila mtu. ¹⁴ Na ikiwa kile mtu alichojenga juu ya musingi huu hakiungui na moto, mtu yule atapokea zawadi. ¹⁵ Lakini kama kile alichojenga kikiungua, yeye atakosa zawadi, hata hivi yeye mwenyewe ataokolewa, lakini itakuwa kama vile ameopolewa toka ndani ya moto. ¹⁶ Hamujui hakika kuwa ninyi ni hekalu la Mungu na kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? ¹⁷ Basi mtu akiharibu hekalu la Mungu, Mungu atamuharibu vilevile. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, na ninyi ndilo hekalu lake. ¹⁸ Mtu yeyote asijidanganye mwenyewe. Kama mtu fulani kati yenu akijizania kuwa mwenye hekima ya kidunia, ajifanye kama mupumbavu kusudi apate kuwa na hekima ya kweli. ¹⁹ Kwa maana hekima ya kidunia ni upumbavu mbele ya Mungu. Ni sawa vile Maandiko Matakatifu yanavyosema: «Mungu anawanasa wenye hekima katika werevu wao wenyewe. ²⁰ Nayo yanasema vilevile: “Bwana anatambua mawazo ya wenye hekima; anajua kwamba ni ya bure.”» ²¹ Basi mtu asijivune kwa ajili ya wanadamu. Kwa maana vitu vyote ni vyenu: ²² ikiwa Paulo, Apolo au Petro, dunia, uzima, kifo, mambo ya sasa au mambo yatakayokuja. ²³ Lakini ninyi ni watu wa Kristo, naye Kristo ni wa Mungu.

Chapter 4

¹ Kwa hiyo mutuhesabu kama watumishi wa Kristo, wanaoshugulika na ujumbe wa siri wa Mungu. ² Yanayohitajika kwa mwenye madaraka kama hayo, ni kuwa mwaminifu. ³ Kwa ngambo yangu, si neno hata kidogo kuhukumiwa nanyi au na tribinali ya watu. Na hata mimi mwenyewe sijihukumu. ⁴ Kweli zamiri yangu hainihukumu juu ya neno lolote, lakini hii si kusema kwamba mimi ni mwenye haki. Bwana ndiye anayenihukumu. ⁵ Kwa hiyo musihukumu mtu mbele ya wakati uliopangwa; mungojee mpaka Bwana atakaporudia. Yeye ndiye atakayeonyesha wazi katika mwangaza mambo yote yaliyofichwa katika giza na kufunua nia za mioyo za watu. Halafu kila mtu atapokea sifa anayostahili toka kwa Mungu. ⁶ Wandugu zangu, nimesema maneno haya nikitwaa mufano wa Apolo na wangu mimi mwenyewe kusudi yakuwe fundisho kwenu. Nilitaka kwamba kufuatana na mufano huu mujifunze maana ya masemi haya: «Musipite pembeni ya maandiko.» Hata mtu mmoja kati yenu asijivunie mtu fulani na kuzarau mwingine. ⁷ Ni nani aliyekuweka kuwa mkubwa kuliko wengine? Si Mungu ndiye aliyekupa vitu vyote unavyokuwa navyo? Ikiwa ni hivi, kwa sababu gani unajivuna kama vile haukuvipewa kama zawadi? ⁸ Sasa mumekwisha kupata vyote munavyohitaji! Mumekwisha kuwa watajiri! Munakuwa wafalme ingawa sisi hatuko wafalme. Heri mungekuwa kweli watawala kusudi nasi vilevile tupate kutawala pamoja nanyi. ⁹ Kwa maana inaonekana kuwa Mungu ametufanya sisi mitume kuwa watu wenye hali ya chini kabisa. Tunahesabiwa kama watu wanaohukumiwa kufa mbele ya watu. Tumewekwa kama kitu cha kushangaza, kinachoangaliwa na dunia nzima, nao wamalaika na watu vilevile. ¹⁰ Sisi ni wapumbafu kwa ajili ya Kristo, lakini ninyi ni wenye hekima katika kuungana kwenu na Kristo. Sisi ni zaifu, lakini ninyi ni wenye nguvu. Tunazarauliwa, lakini ninyi munaheshimiwa! ¹¹ Hata sasa, tunateswa na njaa na kiu, tunakosa nguo, tunapigwa, tunatangatanga bila makao. ¹² Tunasumbuka sana tukifanya kazi kwa mikono yetu wenyewe. Wakati tunapotukanwa, tunabariki; wakati tunapoteswa, tunavumilia; ¹³ wakati tunaposingiziwa, tunajibu kwa upole. Hata sasa tunahesabiwa kama takataka za dunia, na kila mtu anatuangalia kama uchafu. ¹⁴ Siwaandikii maneno haya kwa kuwapatisha haya, lakini kwa kuwaonya kama watoto wangu wapendwa. ¹⁵ Hivi kuelekea maisha yenu na Kristo, hata mukiwa na walezi maelfu muko tu na baba mmoja. Kwa maana kuelekea maisha yenu na Yesu Kristo ni mimi niliyewazaa kwa njia ya kuwatangazia Habari Njema. ¹⁶ Basi ninawasihi, mufuate mufano wangu. ¹⁷ Ni kwa sababu hii ninawatumia ninyi Timoteo. Yeye ni mwana wangu mupendwa na mwaminifu mbele ya Bwana. Atawakumbusha kanuni ninazofuata katika maisha yangu na Yesu Kristo, nami ninazofundisha fasi zote katika makanisa yote. ¹⁸ Watu wamoja kati yenu wanajivuna wakifikiri kwamba sitakuja kuwaona. ¹⁹ Lakini nitakuja kwenu upesi Bwana akitaka. Basi pale nitajua maneno ya wale wanaojivuna na kujionea uwezo wao vilevile! ²⁰ Kwa maana kazi ya Ufalme wa Mungu haionyeshwi kwa njia ya kusema tu, lakini vilevile kwa njia ya matendo ya uwezo. ²¹ Basi munataka nini? Nifike kule kwenu, nikikuja na fimbo au na moyo unaojaa upendo na upole?

Chapter 5

¹ Habari inasikilika fasi zote kwamba kunafanyika uzinzi katikati yenu. Wanaeleza kwamba uzinzi huu ni ubaya mkubwa, usiofanyika hata katikati ya wapagani, kwa maana wanasema kwamba kuna mmoja wenu ambaye amekamata muke wa baba yake kuwa muke wake! ² Nanyi munajaa na kiburi. Ninyi mungepaswa kuhuzunika na mtu yule aliyefanya kile kitendo, naye angepaswa kutengwa toka katikati yenu. ³ Ijapokuwa mimi ni mbali nanyi kimwili, mimi ni pamoja nanyi kiroho. Kwa hiyo nimefanya kama ningekuwa katikati yenu, maana yake, nimekwisha kumuhukumu kwa jina la Bwana wetu Yesu, yule mtu aliyetenda ubaya ule. ⁴ Wakati mutakapokusanyika, mimi vilevile nitakuwa pamoja nanyi kiroho, nao uwezo wa Bwana Yesu utakuwa katikati yenu. ⁵ Basi munapaswa kumutoa mtu yule kwa Shetani, kusudi mwili wake uharibiwe, nayo roho yake iweze kuokolewa Siku ile Bwana Yesu atakaporudi. ⁶ Hamuna kitu cha kujivunia! Hamujui vizuri mufano unaosema kwamba chachu kidogo inachachisha donge zima? ⁷ Basi mujitakase, mukiondoa ile chachu ya zamani ya zambi. Hivi mutakuwa kama donge jipya, lisilotiwa chachu, sawa vile munavyokuwa kwa kweli. Mufanye vile kwa maana Kristo amekwisha kutolewa sadaka kwa ajili yetu kama vile kondoo wa Pasaka. ⁸ Kwa hiyo tufanye karamu yetu ya Pasaka pasipo kutumia mikate iliyotiwa chachu; ni kusema pasipo zambi na uovu. Lakini tutumie mikate isiyotiwa chachu; ni kusema katika usafi na ukweli. ⁹ Katika barua niliyowatumia, niliwaandikia kwamba musishirikiane na washerati. ¹⁰ Hiyo sikusema kabisa kwamba musishirikiane na wote wanaokuwa wazinzi katika dunia hii, wala wenye tamaa, wala wanyanganyi, wala wenye kuabudu sanamu. Kwa maana kwa kujitenga nao, ingewapasa kutoka katika dunia! ¹¹ Lakini niliwaandikia kwamba musishirikiane na mtu anayejiita ndugu mwamini, akiwa mwasherati, mwenye tamaa, mwenye kuabudu sanamu, mutukanaji, mulevi au munyanganyi. Na zaidi ya ile musichangie chakula na mtu wa namna hii. ¹² Basi si kazi yangu kuhukumu wale wanaokuwa wa inje ya kanisa. Mungu ndiye atakayewahukumu. Lakini ninyi hamupaswi kuhukumu watu wa kanisa lenu? ¹³ Kama vile Maandiko Matakatifu yanavyosema: «Mumwondoe mtu yule mubaya toka katikati yenu.»

Chapter 6

¹ Wakati mtu mmoja kati yenu anapokuwa na ugomvi na ndugu mwenzake mwamini, atasubutu namna gani kwenda kumushitaki mbele ya waamuzi wapagani pahali pa kumushitaki mbele ya watu wa Mungu?

² Hamujui kwamba watu wa Mungu ndio watakaohukumu dunia? Na kama ikiwapasa kuhukumu dunia, hamuwezi hata kuhukumu mambo ya burebure? ³ Ninyi hamujui kwamba tutawahukumu wamalaika? Basi, ninyi munaweza kuhukumu zaidi mambo ya maisha haya! ⁴ Basi ikiwa muna magomvi juu ya mambo ya namna hii, kwa nini munayapeleka mbele ya waamuzi wasiokuwa na madaraka katika kanisa? ⁵ Ninasema hivi kwa kuwapatisha haya. Hakika kati yenu hakuna hata mtu mmoja mwenye hekima anayeweza kukata maneno kati ya wandugu zake waamini? ⁶ Lakini sasa ndugu mwamini anamushitaki mwenzake mbele ya waamuzi wasioamini. ⁷ Kweli mambo haya ya kuwa na mashitaki kati yenu yanahakikisha kwamba mumeshindwa kabisa. Si ingekuwa vizuri zaidi kwenu kuvumilia ubaya? Si ingekuwa vizuri zaidi kunyanganywa mali zenu? ⁸ Lakini, ni ninyi ndio munaotenda vibaya na kunyanganya mali ya wengine, nao munaowatendea vile ni wandugu zenu waamini. ⁹ Ninyi munajua hakika kwamba watenda mabaya hawatapata urizi katika Ufalme wa Mungu. Musidanganyike: waasherati, wenye kuabudu sanamu, wazinzi, waasherati wa muke kwa muke na mume kwa mume, ¹⁰ wizi, wenye tamaa, walevi, watukanaji, wanyanganyi, watu wale wote hawatapata urizi katika Ufalme wa Mungu. ¹¹ Na wamoja kati yenu walikuwa kama wao. Lakini mumesafishwa toka zambi, mumetakaswa na kuhesabiwa haki mbele ya Mungu kwa jina la Bwana Yesu Kristo na kwa Roho wa Mungu wetu. ¹² Wamoja kati yenu wanasema: «Vitu vyote vinaruhusiwa kwangu. Ndiyo, lakini vyote si vyenye kufaa kwenu. Ninaweza kusema kwamba vitu vyote vinaruhusiwa kwangu, lakini sitakubali kuwa mutumwa wa kitu chochote. ¹³ Nanyi munasema vilevile: “Chakula kiliumbwa kwa ajili ya tumbo nayo tumbo kwa ajili ya chakula.”» Ndiyo, lakini Mungu ataharibu vyote viwili. Lakini mwili haukuumbwa kwa ajili ya uasherati. Mwili uliumbwa kwa ajili ya Bwana nao ni wake. ¹⁴ Mungu aliyemufufua Bwana Yesu atatufufua nasi vilevile kwa uwezo wake. ¹⁵ Munajua kwamba miili yenu ni viungo vya mwili wa Kristo. Basi nitatwaa kiungo cha mwili wa Kristo kwa kukifanya kuwa kiungo cha kahaba? Hapana hata kidogo! ¹⁶ Au hamujui kwamba mtu yule anayeungana na kahaba amekwisha kuwa mwili mmoja naye? Kwa maana Maandiko Matakatiifu yanasema: «Hao wawili watakuwa mwili mmoja.» ¹⁷ Lakini anayeungana na Bwana anageuka kuwa mmoja naye kiroho. ¹⁸ Muepuke uzinzi! Zambi ingine yoyote mtu anayofanya haigusi mwili wake, lakini yule anayefanya uzinzi anafanya zambi juu ya mwili wake mwenyewe. ¹⁹ Hamujui kwamba mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu anayekuwa ndani yenu, yule muliyepewa na Mungu? Na ninyi si mali yenu wenyewe. ²⁰ Kwa sababu mulinunuliwa na Mungu kwa bei kali. Basi mutumie miili yenu na roho zenu kwa utukufu wa Mungu.

Chapter 7

¹ Sasa tuangalie mambo yale muliyoniandikia. Ni vizuri mwanaume asioe. ² Lakini kwa ajili ya kuepuka uasherati inafaa kila mwanaume akuwe na muke wake wa pekee, na kila mwanamuke akuwe na mume wake wa pekee. ³ Mume anapaswa kumutimizia muke wake mapaswa yake, na muke anapaswa kumutimizia mume wake mapaswa yake. ⁴ Muke hawezi kuamua sawa anavyotaka juu ya mwili wake mwenyewe; kwa sababu ni mwili wa mume wake. Vilevile mume hawezi kuamua sawa anavyotaka juu ya mwili wake mwenyewe; kwa sababu ni mwili wa muke wake. ⁵ Musinyimane, isipokuwa tu mumeapatana na kwa muda tu kusudi mupate wakati wa kujitoa kwa kufunga na kuomba. Kisha munaweza kurudiliana tena kusudi Shetani asiwajaribu katika uzaifu wenu. ⁶ Maneno hayo ninayowaambia si amri, lakini ni ruhusa tu ninayowapa. ⁷ Hakika, ningetamani watu wote wakuwe kama mimi, lakini kila mtu amepewa zawadi yake ya kipekee na Mungu, mmoja zawadi hii, na mwingine zawadi ile. ⁸ Na kwa wale wasiooa bado na wajane, ninawaambia kwamba ingekuwa vema waendele kuishi peke yao kama vile mimi. ⁹ Lakini kama hawawezi kujizuiza wao wenyewe, basi waoane; kwa maana afazali kuo kuwa kuliko kuwaka tamaa. ¹⁰ Kwa wale waliokwisha kuoana, ninatoa amri hii, isiyotoka kwangu, lakini kwa Bwana Mungu: muke hapaswi kuachana na mume wake. ¹¹ Lakini kama muke akiachana na mume wake, asirolewe tena, kama si vile apatane tena na mume wake. Vilevile mume hapaswi kufukuza muke wake. ¹² Na kwa wengine, mimi ninawaambia maneno haya, lakini hayatoki kwa Bwana: kama mume mwamini akiwa na muke asiyeamini, naye muke yule akikubali kuishi pamoja naye, asimufukuze. ¹³ Vilevile kama muke mwamini akiwa na mume asiyeamini, naye mume yule akikubali kuishi pamoja naye, asiachane na mume wake. ¹⁴ Kwa maana, mume asiyeamini anapata ushirika na Mungu kwa njia ya kuungana kwake na muke wake. Vilevile muke asiyeamini anapata ushirika na Mungu kwa njia ya kuungana kwake na mume wake mwamini, watoto wao wangehesabiwa kama watoto wa wapagani. ¹⁵ Lakini kama mume au muke mupagani akitaka kuachana na mwamini aliyeoana naye, aachane naye. Katika mambo kama hayo, ndugu au dada mwamini yuko huru, kwa maana Mungu amewaita kusudi mukae katika amani. ¹⁶ Wewe muke mwamini unaweza kujua namna gani kwamba utamwoko mume wako? Au wewe mume mwamini utaweza kujua namna gani kwamba utamwoko muke wako? ¹⁷ Kwa ngambo ingine, kila mtu aendele kuishi kufuatana na zawadi aliyopewa na Bwana na kufuatana na vile alivyokuwa mbele ya kuitwa na Mungu. Hii ndiyo kanuni ninayofundisha katika makanisa yote. ¹⁸ Ikiwa mtu alitahiriwa mbele ya kuitwa na Mungu, asitafute kufuta kovu la kutahiriwa kwake. Ikiwa alikuwa hajatahiriwa wakati alipoitwa na Mungu, hapaswi kutahiriwa. ¹⁹ Kutahiriwa au kutotahiriwa hakufai kitu. Kitu kinachofaa ni kutii amri za Mungu. ²⁰ Inafaa kila mtu abaki sawa alivyokuwa wakati alipoitwa na Mungu. ²¹ Ikiwa ulikuwa mutumwa wakati Mungu alipokuita, usihuzunike. Lakini ikiwa kuna bahati ya kupata uhuru, usiipoteze bure. ²² Kwa maana mutumwa aliyeitwa kuwa wa Bwana, amepewa uhuru na Bwana. Hivi vilevile mtu mwenye uhuru aliyeitwa na Kristo, ni mutumwa wa Kristo. ²³ Mumenunuliwa na Mungu kwa bei kali, basi musikuwe tena watumwa wa watu. ²⁴ Wandugu zangu, inafaa kila mtu akae katika ushirika wake na Mungu akibaki sawa alivyokuwa wakati alipoitwa naye. ²⁵ Kuelekea wale ambao hawajaoa wala kuolewa, sina neno la kuwaamuru kutoka kwa Bwana. Lakini nitawatolea shauri kufuatana na vile ninavyokuwa mtu anayestahili kuaminiwa, kutokana na neema niliyopewa na Bwana. ²⁶ Kwa sababu ya taabu ya siku hizi, ninafikiri kwamba ni vizuri mtu akae sawa vile anavyokuwa. ²⁷ Ikiwa umekwisha kuo, usitafute kuachana na muke wako. ²⁸ Lakini kama ukioa, haufanyi zambi, na kama binti anaolewa, yeye hafanyi zambi vilevile. Lakini wale wanaoana watakuwa na mateso katika maisha yao, na mimi ninataka kuwaonya kusudi muepuke mateso yale. ²⁹ Wandugu zangu, mimi ninataka kusema hivi: wakati uliopangwa unabaki mufupi. Tangu sasa wale walioa waishi kama vile wasioa. ³⁰ Wale wanaolia wakuwe kama vile wasiolia. Wale wanaofurahi wakuwe kama vile wasiofurahi. Wale wanaonunua vitu wakuwe kama vile hawana kitu. ³¹ Wale wanaotumia mali ya dunia hii wakuwe kama vile wasioitumia. Kwa maana dunia hii inakaribia kupita. ³² Ningependa muishi bila masumbuko yoyote. Mtu asiyeoa anashugulikia mambo ya Bwana, anatafuta jinsi ya kumupendeza Bwana. ³³ Lakini mtu aliyeoa anasumbukia mambo ya dunia, anatafuta jinsi ya kupendeza muke wake. ³⁴ Yeye anashugulikia mambo mawili. Vilevile mwanamuke asiyeolewa au binti anashugulikia mambo ya Bwana. Anajitolea kwa Bwana katika mwili na moyo wake wote. Lakini mwanamuke anayeolewa, anashugulikia mambo ya dunia, anatafuta jinsi ya kumupendeza mume wake. ³⁵ Maneno hayo ninayosema ni kwa faida yenu, wala si kwa kuwafungia njia. Ninataka kuwaonyesha namna ya kuishi sawa inavyofaa, kusudi mupate kumutumikia Bwana pasipo kizuizo chochote. ³⁶ Mtua akiona kwamba hatembeyi vilivyo kuhusu ubikira wake, kama wakati unapita na inapashwa kuwa hivyo, afanye kile anataka, hatendi zambi, aoe ao aolewe. ³⁷ Lakini yule ambaye ana msimamo mkali katika moyo wake bila kusurutishwa, akiwa na uwezo juu ya tamaa yake

mwenyewe na hii ameamua katika moyo wake mwenyewe kulinda ubikira wake mwenyewe anafanya vema. ³⁸ Hivyo, mwenye kutoa ubikira wake kwa kuoa ao kuolewa anafanya vema, na yule ambaye hatowi ubikira wake atafanya vema zaidi. ³⁹ Mwanamuke aliye olewa anafungwa na Sheria katika maisha yake na mume wake wakati mume wake angali mzima. Lakini kama mume wake akikufa, yeye ni huru kuolewa na yule anayetaka, lakini sherti ndoa ikuwe ya kikristo. ⁴⁰ Lakini ingekuwa heri zaidi kama angekaa sawa vile anavyokuwa. Hilo ni shauri langu, nami vilevile ninazani kwamba ninaongozwa na Roho wa Mungu.

Chapter 8

¹ Sasa tuangalie mambo yanayoelekea nyama zinazotolewa kwa kutambikia sanamu za miungu: tunajua kwamba sisi wote tuko na elimu, kama vile munavyozoea kusema. Elimu inamufanya mtu kuwa na kiburi, lakini upendo unawajenga watu katika imani. ² Kama mtu anajizania kwamba anajua kitu, yeye hakijui hakika sawa vile inavyomupasa kukijua. ³ Lakini yule anayemupenda Mungu, huyu anajulikana naye. ⁴ Basi kuelekea lile ulizo juu ya kula nyama za kutambikiwa kwa sanamu za miungu, tunajua kwamba sanamu ni kitu bure katika dunia, na ya kuwa kuna Mungu mmoja peke yake tu. ⁵ Kuko wale wanaoitwa miungu katika mbingu na katika dunia, na hivi kuko miungu mingi na wabwana wengi. ⁶ Ingawa hivi, kwa ngambo yetu sisi tuko na Mungu mmoja peke yake tu, ndiye Baba aliyeumba vitu vyote, nasi tunaishi kwa nguvu yake. Vilevile kuko Bwana mmoja tu, ndiye Yesu Kristo. Kwa njia yake vitu vyote viliumbwa, nasi tunaishi kwa nguvu yake. ⁷ Lakini si watu wote wanaofahamu mambo hayo. Wengi wamezoea kutambikia sanamu za miungu mpaka sasa, wanakula nyama wakizihesabu hakika kuwa za kutambikia sanamu zile. Kwa sababu zamiri yao ni mbovu, wanajisikia kwamba wanajichafua kwa kula chakula kile. ⁸ Chakula hakitaleta ushirika kati yetu na Mungu. Kama tukiacha kula hatupungukiwi kitu na kama tukikula hatuongezewi kitu. ⁹ Lakini, muangalie vizuri kusudi uhuru wenu usiangushe wale wanaokuwa zaifu katika imani. ¹⁰ Kwa maana kama mtu zaifu katika imani akikuona wewe mwenye elimu unakula katika hekalu la sanamu, si zamiri yake itamusukuma kula vyakula vya kutambikia sanamu? ¹¹ Na hivi kwa sababu ya elimu yako, yule ndugu mwamini zaifu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake, atapotea. ¹² Kwa kuwakosesha wandugu zenu kama hivi na kuumiza zamiri yao, ni kama vile munamukosea Kristo mwenyewe. ¹³ Kwa hiyo chakula kikimwangusha ndugu yangu katika zambi, nitajizuiza kula nyama siku zote kusudi nisimwangushe ndugu yangu.

Chapter 9

¹ Mimi si huru? Mimi si mutume? Mimi sikumuona Yesu Kristo Bwana wetu? Ninyi si matunda ya kazi yangu kwa ajili ya Bwana? ² Hata ikiwa watu wengine hawakubali kuwa mimi ni mutume, ninyi munakubali kuwa mimi ni mutume. Ninyi ni kitambulisho kinachohakikisha kwamba mimi ni mutume, kwa ajili ya kuungana kwenu na Bwana. ³ Watu wanaponishitaki, mimi ninajitetea kwa namna hii: ⁴ basi sina haki ya kupokea chakula na kinywaji kwa ajili ya kazi yangu? ⁵ Au sina haki ya kusafiri pamoja na mwanamuke mukristo kama vile mitume wengine wanavyofanya, nao wandugu za Bwana na hata Petro? ⁶ Au ni mimi na Barnaba tu ndio tunaopaswa kujitumikia wenyewe kwa kupata vifaa vya maisha? ⁷ Ni askari gani anayejilipia mwenyewe vifaa vya kiaskari? Au mtu gani asiyekula matunda ya mizabibu aliyopanda? Au ni mchungaji gani asiyekunywa maziwa ya kundi analochunga? ⁸ Musifikiri kuwa ninasema maneno hayo kufuatana na mambo ya maisha. Hata Sheria ya Musa inasema maneno hayo vilevile. ⁹ Kwa maana imeandikwa hivi katika Sheria ile ya Musa: «Usifunge kinywa cha ngombe anapokanyaga nganoa.» Mungu anashugulikia ngombe? ¹⁰ Hasemi maneno haya zaidi sana kwa ajili yetu? Hakika, maneno hayo yaliandikwa kwa ajili yetu. Inafaa yule anayelima na yule anayetwanga watumike wakiwa na tumaini la kupata sehemu yao ya mavuno. ¹¹ Ikiwa tumepanda mbegu ya kiroho ndani yenu, basi kuna jambo gani kubwa kama nasi tukitazamia kupata vifaa vya kimwili toka kwenu? ¹² Ikiwa wengine wako na haki ya kupata vitu kama vile toka kwenu, sisi hatuna haki zaidi kuliko wao? Sisi hatudai kutendewa sawa na haki yetu, lakini tunavumilia kusudi tusiiwekee Habari Njema ya Kristo kizuizo chochote. ¹³ Munajua hakika kuwa wale wanaotumika katika hekalu wanapata chakula chao ndani ya hekalu. Na wale wanaotumika kwa kutoa sadaka juu ya mazabahu wanapata sehemu yao kutoka sadaka zile. ¹⁴ Vilevile, Bwana aliagiza kuwa wale wanaohubiri Habari Njema wanapaswa kuishi kwa njia ya Habari Njema. ¹⁵ Lakini mimi sikudai hata neno moja ya haki hizo, wala sikuandikii haya kwa kusudi la kutafuta kuzipewa. Ingekuwa heri kwangu kufa kuliko kuzuizwa na mtu yeyote kwamba nisijisifu juu ya jambo hili. ¹⁶ Mimi sina haki ya kujisifu kwa sababu ninatangaza Habari Njema, kwa maana nimelazimishwa kuitangaza. Basi ole kwangu kama nisipotangaza Habari Njema. ¹⁷ Ingekuwa nimechagua kazi hii kwa mapenzi yangu mwenyewe, ningeweza kungojea kupokea mushahara. Lakini kwa kuwa ni muzigo niliopewa, inanipasa kuitimiza. ¹⁸ Basi mushahara wangu ni gani? Mushahara wangu ni kutangaza Habari Njema bila kulipwa, maana yake bila kudai haki ninazostahili kwa kuitangaza. ¹⁹ Mimi si mutumwa wa mtu yeyote. Lakini nimejifanya kuwa mutumwa wa watu kusudi nipate wengi kati yao sawa inavyowezekana. ²⁰ Kwa Wayuda, ninaishi kama Muyuda, kusudi niwapate Wayuda. Mimi siishi chini ya uongozi wa Sheria ya Musa, lakini kusudi niwapate wale wanaoishi chini ya Sheria ile, ninapokuwa kati yao, ninaishi kufuatana na Sheria ile. ²¹ Vilevile ninapokuwa kati ya wasioishi chini ya Sheria ya Musa, ninaishi kama wao, bila kuangalia Sheria, kusudi niwapate. Hii si kusema kwamba mimi sishiki sheria ya Mungu, kwa maana mimi ni chini ya uongozi wa sheria ya Kristo. ²² Na kwa wale wanaokuwa zaifu katika imani, ninajifanya kama muzaifu kusudi niwapate hao wanaokuwa zaifu. Kwa wote nimejifunza kuwa mwenye hali kama yao, kusudi nipate kuokoa wamoja kati yao kwa njia mbalimbali. ²³ Ninafanya hayo yote kwa ajili ya Habari Njema kusudi nipate sehemu ya baraka zake. ²⁴ Munajua hakika kuwa wale wanaofanya mashindano ya kukimbia, wote wanakimbia lakini ni mmoja tu anayepokea zawadi. Basi mukimbie hata mufikie kupokea zawadi. ²⁵ Na kila mtu anayefanya mashindano katika michezo anajizuiza na vitu vingi katika mazoezi yake. Basi wanafanya hivi kusudi wapate taji yenye kuharibika; lakini sisi tunafanya vile, kusudi tupate taji isiyoharibika. ²⁶ Ni kwa sababu hiyo ninakimbia nikiwa na shabaha ya kushinda. Mimi ni kama mupiganaji wa ngumi asiyepiga katika hewa. ²⁷ Lakini ninatesa mwili wangu kwa mazoezi makali na kuutumikisha vikali kusudi mimi mwenyewe nisikataliwe kisha kutangaza ujumbe kwa watu wengine.

Chapter 10

¹ Wandugu zangu, ninataka mukumbuke kwamba babu zetu wote walisafiri wakiongozwa na wingu, nao wote walivuka katikati ya bahari Nyekundu kwa usalama. ² Wote walibatizwa katika lile wingu na katika ile bahari kusudi wapate kuungana na Musa. ³ Wote walikula chakula kimoja cha kiroho. ⁴ Wote walikunywa kinywaji kimoja cha kiroho; kwa maana walikunywa maji yaliyotoka ndani ya lile jiwe lililosafiri pamoja nao, nalo jiwe lilikuwa Kristo. ⁵ Lakini, wengi sana kati yao hawakumupendeza Mungu, kwa hiyo wakakufia katika jangwa. ⁶ Mambo hayo ni mufano kwetu, kusudi tusikuwe na tamaa mbaya kama vile wao. ⁷ Basi musikuwe wenye kuabudu sanamu kama wamoja kati yao walivyokuwa; kama vile Maandiko haya Matakatiifu yanavyosema: «Watu wakaikaa kula na kunywa na kisha wakasimama kwa kujifurahisha.» ⁸ Musifanye uasherati kama vile wamoja kati yao walivyofanya hata wakakufa kwa siku moja watu elfu makumi mbili na tatu. ⁹ Vilevile tusimupime Kristo kama vile wamoja wao walivyofanya, hata wakauawa na nyoka. ¹⁰ Musinungunike kama vile wamoja kati yao walivyofanya hata malaika mwangamizaji akawateketeza. ¹¹ Mambo haya yote yaliwafikia kusudi yakuwe mufano kwa watu wengine; yameandikwa kwa kutuonya sisi, kwa maana tunaishi katika kipindi cha mwisho wa nyakati. ¹² Kwa hiyo yule anayefikiri kwamba anasimama imara, afanye angalisho asianguke. ¹³ Majaribu yale munayopata, ni yale yanayowapata watu wengine wote. Mungu hatawaachilia kujaribiwa kupita nguvu zenu, kwa maana yeye ni mwaminifu. Jaribu litakapowatokea, atawapatia nguvu ya kulivumilia, hata muweze kulishinda. ¹⁴ Kwa hiyo wapenzi wangu, muepuke kutambikia sanamu. ¹⁵ Ninasema nanyi kama watu wenye akili; muamue ninyi wenyewe juu ya maneno ninayotaka kuwaambia: ¹⁶ tunapokunywa kikombe ambacho kwa ajili yake tunamutolea Mungu shukrani, basi kwa njia ya kikombe kile hatuungani na damu ya Kristo? Nasi tunapomega mukate na kuukula, kwa njia hiyo, mukate ule hautuungi na mwili wa Kristo? ¹⁷ Kwa kuwa mukate ni mmoja, ijapokuwa sisi ni wengi, tuko mwili mmoja, kwa maana sisi wote tunashiriki mukate ule mmoja. ¹⁸ Muangalie mufano wa Waisraeli: wale wanaokula vitu vinavyotolewa sadaka juu ya mazabahu wanaungana na Mungu kwa njia ya sadaka ile. ¹⁹ Basi niseme nini? Nyama iliyotambikiwa kwa sanamu ni yenye mafaa? Au kwamba sanamu ni kitu cha lazima? ²⁰ Hapana. Ninataka kusema kwamba vitu wapagani wanavyotambikia, wanavitolea pepo wala si Mungu. Nami sipendi mushirikiane na pepo hata mara moja. ²¹ Hamuwezi kuchangia kikombe cha Bwana na kikombe cha pepo. Vilevile hamuwezi kuchangia meza ya Bwana na meza ya pepo. ²² Au tunataka kumuchokoza Bwana hata asikie wivu? Munafikiri kuwa sisi tuko na nguvu kuliko yeye? ²³ Wamoja wenu wanasema: «Vitu vyote vinaruhusiwa. Ni kweli, lakini vyote havifai. Vitu vyote vinaruhusiwa, lakini vyote havifai kwa kujenga imani. ²⁴ Mtu asitafute faida yake mwenyewe, lakini faida ya mwenzake. ²⁵ Ninyi ni huru kwa kula kila kitu kinachouzishwa katika soko bila kuulizauliza neno kwa sababu ya zamiri. ²⁶ Kwa «maana Maandiko Matakatiifu yanasema: Dunia na vyote vinavyokuwa ndani yake ni vya Bwana.» ²⁷ Kama mupagani anawaalika kula chakula, nanyi mukikubali kwenda kule, mukule vyote wanavyotoa kwenu bila kuulizauliza neno kwa sababu ya zamiri. ²⁸ Lakini kama mtu akiwaambia ninyi: «Vyakula hivi vimetambikiwa kwa sanamu,» basi musivikule kwa ajili ya yule aliyewaarifu na kwa ajili ya zamiri. ²⁹ Sisemi juu ya zamiri zenu, lakini juu ya zamiri ya yule aliyewaarifu. Labda kuna mtu anayeweza kuuliza: «Kwa sababu gani ninaweza kuzuizwa kutenda sawa na uhuru wangu kwa ajili ya mwingine? ³⁰ Kama ninamushukuru Mungu kwa ajili ya chakula ninachokula, kwa nini wananiteta juu ya chakula ambacho kwa ajili yake ninamutolea Mungu shukrani?» ³¹ Basi, kama mukikula au mukikunywa, au mukifanya neno lolote, mufanye yote kwa ajili ya utukufu wa Mungu. ³² Basi muangalie, kusudi musiwakwaze Wayuda, wala Wagriki, wala kanisa la Mungu. ³³ Mufanye kama vile mimi: ninajikaza kwa kupendeza watu wote katika mambo yote, maana sitafuti faida yangu mimi mwenyewe, lakini faida ya watu wote, kusudi waokolewe.

Chapter 11

¹ Mufuate mufano wangu kama vile mimi ninavyofuata mufano wa Kristo. ² Ninawashukuru kwa sababu munanikumbuka katika mambo yote na kwa sababu munashika mafundisho yangu sawa vile nilivyoyafundisha kwenu. ³ Lakini ninataka mufahamu maneno haya: Kristo ni kichwa cha kila mwanaume, na mwanaume ni kichwa cha muke wake, na Mungu ni kichwa cha Kristo. ⁴ Basi mwanaume yeyote akifunika kichwa chake wakati anapoomba Mungu, au anapotabiri, anamuzaraulisha Kristo. ⁵ Lakini mwanamuke yeyote asipofunika kichwa chake wakati anapoomba au anapotabiri, anamuzaraulisha mume wake. Tendo hilo linahesabiwa kama vile amenyolewa. ⁶ Kama mwanamuke hafuniki kichwa, anaweza basi kunyolewa! Lakini kwa sababu ni haya kwa mwanamuke kukatwa nywele au kunyolewa, basi inafaa afunike kichwa. ⁷ Mwanaume hapaswi kufunika kichwa, kwa sababu yeye ni mufano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamuke ni utukufu wa mwanaume. ⁸ Kwa maana mwanaume hakuumbwa kutoka katika mwanamuke, lakini mwanamuke aliumbwa kutoka katika mwanaume. ⁹ Na zaidi ya hii, mwanaume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamuke, lakini mwanamuke aliumbwa kwa ajili ya mwanaume. ¹⁰ Kwa hiyo, kwa sababu ya wamalaika, mwanamuke anapaswa kufunika kichwa chake kuwa kitambulisho kinachoonyesha kuwa yuko chini ya mamlaka ya mume wake. ¹¹ Lakini katika ushirika wetu na Bwana, hakuwezi kuwa mwanamuke pasipo mwanaume wala mwanaume pasipo mwanamuke. ¹² Kwa maana kama vile mwanamuke alivyoombwa kutoka katika mwanaume, vilevile mwanaume anazaliwa na mwanamuke; na vyote vinatoka kwa Mungu. ¹³ Muamue ninyi wenyewe: ni vema mwanamuke asifunike kichwa anapoomba Mungu wakati wa ibada? ¹⁴ Hali ya asili yenyewe inawaonyesha kuwa ni haya kwa mwanaume kuwa na nywele ndefu, ¹⁵ lakini ni heshima kwa mwanamuke kuwa na nywele ndefu. Kwa maana nywele ndefu zimetolewa kwa mwanamuke kwa kuwa nguo ya kufunika kichwa. ¹⁶ Lakini kama mtu akitaka kubishana juu ya neno hili, ajue kwamba sisi wala makanisa ya Mungu hatuna desturi ingine. ¹⁷ Kuelekea maonyo yanayofuata, mimi siwasifu. Kwa maana munapokusanyika, mikutano yenu haiwafalii, lakini inawaletea hasara. ¹⁸ Kwanza, ninasikia kwamba munapokusanyika kuna matengano katikati yenu, nami ninasadiki kwamba nusu ya maneno yale ni ya kweli. ¹⁹ (Inafaa kuwe matengano kati yenu, kusudi wale wanaokuwa waaminifu wa kweli kati yenu wajulikane.) ²⁰ Munapokusanyika hamukuli karamu ya Bwana. ²¹ Kwa maana munapokula, kila mmoja anajiharikisha kula chakula chake mwenyewe, hivi wamoja wenu wanasikia njaa na wengine wanalewa. ²² Basi, ninyi hamuna nyumba munamoweza kukulia na kukunywea? Au munazarau kanisa la Mungu na munataka kuwapatisha haya wale wasiokuwa na kitu? Munataka niwaambie ninyi nini? Inafaa niwasifu? Hapana, siwezi kuwasifu hata kidogo juu ya jambo hilo! ²³ Kwa maana haya ndiyo mafundisho niliyopokea kutoka kwa Bwana, nami niliyotoa kwenu: katika usiku ule Bwana Yesu alipotolewa, alitwaa mukate, ²⁴ na alipokwisha kumushukuru Mungu, akaumega akisema: «Huu ni mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu. Mufanye hivi kwa kunikumbuka. ²⁵ Vilevile, nyuma ya kula akatwaa kikombe na kusema: “Kikombe hiki ni agano jipya la Mungu, linalohakikishwa kwa njia ya damu yangu. Mufanye hivi kwa kunikumbuka kila mara munapokikunywa.”» ²⁶ Kwa sababu kila mara munapokula mukate huu na kunywa kikombe hiki, munatangaza kufa kwa Bwana mpaka atakapokuja. ²⁷ Basi kila mtu anayekula mukate wa Bwana au kunywa kikombe chake bila kustahili, anafanya zambi akikosea mwili na damu ya Bwana. ²⁸ Basi kila mtu ajichunguze mwenyewe na kisha akule mukate huu na kunywa kikombe hiki. ²⁹ Kwa maana mtu akikula mukate na kunywa kikombe pasipo kutambua maana ya mwili wa Bwana, anajiletea azabu yeye mwenyewe kwa kula na kunywa. ³⁰ Na kwa sababu hii wengi kati yenu ni wagonjwa na wazaifu, na wengi wamekufa. ³¹ Lakini tungejichunguza sisi wenyewe kwanza, hatungehukumiwa na Mungu. ³² Lakini tunahukumiwa na kuazibiwa na Bwana kusudi tusiazibiwe pamoja na watu wa dunia hii. ³³ Kwa hiyo wandugu zangu, wakati munapokusanyika kwa kula karamu ya Bwana, sherti mungojeane. ³⁴ Kama mtu akiwa na njaa, akule katika nyumba yake, kusudi musikusanyike kwa kujiletea azabu. Basi maneno mengine yanayobaki nitayatengeneza wakati nitakapofika kwenu.

Chapter 12

¹ Sasa tuangalie mambo yanayoelekea zawadi za Roho Mtakatifu. Wandugu zangu, sitaki mukose kufahamu ukweli wa zawadi hizi. ² Munajua kwamba wakati mulipokuwa wapagani, mulikuwa mukivutwa na kupotoshwa na sanamu zisizosema. ³ Kwa sababu hii ninataka mufahamu kwamba hakuna mtu ambaye anaongozwa na Roho wa Mungu anayeweza kusema: «Yesu alaniwe, na hakuna mtu anayeweza kusema: “Yesu ni Bwana,”» kama asipoongozwa na Roho Mtakatifu. ⁴ Kuna zawadi mbalimbali, lakini ni Roho mmoja anayezitoa. ⁵ Kuna utumishi wa namna mbalimbali, lakini ni Bwana mmoja ndiye wanayemutumikia. ⁶ Kuna kazi za namna mbalimbali, lakini Mungu ni mmoja anayewezesha watu wote kuzitimiza. ⁷ Na kwa kila mtu Roho anajifunua kwa faida ya wote. ⁸ Basi mtu mmoja anapewa na Roho uwezo wa kusema maneno ya hekima, na mwingine uwezo wa kusema maneno ya ufahamu na Roho yule yule. ⁹ Mwingine anapewa imani na Roho yule yule na mwingine napewa zawadi ya uwezo wa kuponyesha wagonjwa. ¹⁰ Mwingine anapewa uwezo wa kufanya miujiza, mwingine zawadi ya kutabiri, na mwingine uwezo wa kutambua roho ya uongo na Roho wa ukweli. Mwingine alipewa uwezo wa kusema lugha za ajabu na mwingine uwezo wa kutafsiri lugha zile. ¹¹ Ni yule yule Roho mmoja anayetenda mambo hayo yote, akimupa kila mmoja zawadi mbalimbali kama anavyopenda. ¹² Kwa maana, Kristo ni kama mwili mmoja unaokuwa na viungo vingi. Ijapokuwa viungo vya mwili ni vingi, vinakuwa mwili mmoja tu. ¹³ Vilevile sisi wote, Wayuda na Wagriki, watumwa na watu wanaokuwa huru, tumebatizwa kwa Roho mmoja kusudi tukuwe mwili mmoja na sisi wote tumenyweshwa Roho mmoja. ¹⁴ Mwili hauundwi na kiungo kimoja tu, lakini na viungo vingi. ¹⁵ Kama muguu ungesema: «Kwa sababu mimi si mukono, basi mimi si wa mwili, hata vile haungeacha kuwa kiungo cha mwili. ¹⁶ Na kama sikio lingesema: “Kwa sababu mimi si jicho, basi mimi si wa mwili,” hata vile halingeacha kuwa kiungo cha mwili. ¹⁷ Kama mwili wote ungekuwa jicho, namna gani ungeweza kusikia? Na kama ungekuwa sikio, namna gani ungeweza kunusa? ¹⁸ Lakini sasa, Mungu amepanga viungo vya mwili kila kimoja kama ilivyomupendeza. ¹⁹ Kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili haungekuwa! ²⁰ Kwa hivi sasa kunakuwa viungo vingi lakini mwili ni mmoja. ²¹ Jicho haliwezi kuuambia mukono: “Sina lazima yako!” Wala kichwa hakiwezi kuiambia miguu: “Sina lazima yenu!”» ²² Lakini zaidi ya hiyo, viungo vya mwili vinavyoonekana kuwa zaifu, ndivyo vinavyokuwa vya lazima. ²³ Tena viungo vile tunavyozania kwamba havistahili heshima kubwa ndivyo tunavyoheshimu zaidi. Na viungo vinavyokuwa vya haya ndivyo tunavyotunza sana, ²⁴ wakati vile vinavyoheshimiwa havihitaji kitu. Mungu ameunganisha mwili hata akavipatia heshima zaidi viungo vilivyokosa heshima, ²⁵ kusudi kusikuwe mabishano katikati ya viungo vya mwili, lakini vyote visaidiane sawasawa. ²⁶ Kama kiungo kimoja kikiumia, viungo vingine vyote vinaugua pamoja nacho. Kiungo kimoja kikiheshimiwa, viungo vingine vyote vinafurahi pamoja nacho. ²⁷ Ninyi wote ni mwili wa Kristo, na kila mmoja wenu ni kiungo cha mwili ule. ²⁸ Vilevile Mungu ameweka kwanza mitume katika kanisa; pili manabii na tatu walimu; kisha kunakuwa wale wenye zawadi ya kufanya miujiza, ya kuponyesha wagonjwa, ya kusaidia wengine, ya kuongoza wengine, ya kusema lugha za ajabu. ²⁹ Wote si mitume, manabii au walimu. Wote hawana uwezo wa kufanya miujiza, ³⁰ Ao zawadi ya kuponyesha wagonjwa, wa kusema kwa lugha za ajabu, au wa kutafsiri. ³¹ Basi mutamani sana zawadi inayokuwa bora zaidi.

Chapter 13

¹ Hata nikiwa na uwezo wa kusema luga za watu na za wamalaika, lakini kama sina upendo, masemi yangu ni bure kama vile kelele la kengele au matoazi. ² Hata nikiwa na zawadi ya kutabiri, na uwezo wa kujua mafumbo yote na maarifa yote; hata nikiwa na imani kubwa inayoweza kuhamisha milima; lakini kama sina upendo, mimi ni kitu bure. ³ Ninaweza vilevile kugawanya mali yangu yote kwa kulisha wamasikini na hata kutoa mwili wangu uunguzwe, lakini kama sina upendo, hakuna faida ninayopata. ⁴ Upendo unavumilia, ni wenye wema; upendo hauna wivu, upendo haujivuni, na hauna kiburi. ⁵ Upendo haukosi kuwa na adabu, hautafuti faida yake mwenyewe, haukasiriki upesi, nao hauhesabii mtu ubaya. ⁶ Upendo haufurahii ubaya, lakini unafurahia ukweli. ⁷ Upendo hauchoki na mambo yote, unaamini mambo yote, unatumaini mambo yote na kuvumilia mambo yote. ⁸ Upendo haukomi hata kidogo. Lakini kutabiri kunatoweka, zawadi ya kusema kwa luga za ajabu inatoweka, na maarifa yanapita. ⁹ Kwa maana tunafahamu tu mambo machache na kutabiri tu mambo machache. ¹⁰ Lakini wakati mambo matimilifu yatakapokuja, yale yasiokuwa matimilifu yatatoweka. ¹¹ Wakati nilipokuwa mtoto, nilisema kama mtoto, niliwaza kama mtoto, nilifikiri kama mtoto. Lakini nilipokuwa mtu mzima niliacha mambo ya kitoto. ¹² Kwa maana wakati wa sasa tunaona kama mwenye kuangalia ndani ya kioo kisichoonyesha wazi, lakini wakati utakaokuja tutaona waziwazi. Kwa sasa ninajua tu mambo machache, lakini nyuma nitajua kwa utimilifu kama vile Mungu anavyonijua mimi. ¹³ Basi sasa, hivi vitu vitatu vinadumu: imani, tumaini na upendo; lakini kinachokuwa kikubwa kuliko hivi vingine ni upendo.

Chapter 14

¹ Mujikaze mukuwe na upendo. Vilevile mutamani sana kupata zawadi za Roho, hasa zaidi zawadi ya kutabiri. ² Mtu anayesema kwa luga ya ajabu hasemi na watu lakini anasema na Mungu, kwa maana hakuna mtu anayemusikia. Kwa uwezo wa Roho, mtu yule anasema mafumbo. ³ Lakini yule anayetabiri anasema na watu maneno ya kuwajenga katika imani, kuwatia moyo na kuwatuliza. ⁴ Yule anayesema kwa luga ya ajabu anajenga imani yake mwenyewe, lakini yule anayetabiri anajenga imani ya kanisa zima. ⁵ Ninataka ninyi wote museme kwa luga za ajabu, lakini ninataka zaidi tena mupate kutabiri. Kwa maana, yule anayetabiri ni wa lazima kuliko yule anayesema kwa luga za ajabu, isipokuwa kama huyo mtu anaweza kutafsiri yale anayosema kusudi kanisa zima lijengwe katika imani. ⁶ Basi wandugu zangu, nitawafalia nini kama nikikuja kwenu na kusema nanyi katika luga za ajabu? Sitawafalia kitu pasipo kuwaelezea maneno ya ufunuo, au ya elimu, pasipo kuwatabiria au kuwafundisha. ⁷ Tuangalie mufano wa vyombo vya muziki kama vile filimbi au kinanda. Milio ya vyombo hivi isipokuwa mbalimbali, namna gani mtu anavyoweza kutambua wimbo unaopigwa? ⁸ Ngunga isipopigwa kwa mulio wa kuarifu, askari gani atakayeweza kujitayarisha kwa vita? ⁹ Ni hivi vilevile mambo munayosema yatatambulika namna gani ikiwa maneno munayoeleza kwa luga za ajabu hayako wazi? Kwa maana mutakuwa kama wenye kusema na upepo. ¹⁰ Kuna namna mbalimbali za luga katika dunia, lakini hakuna hata moja isiyokuwa na maana. ¹¹ Basi kama nisipojua luga fulani, nitakuwa kama mujinga kwa yule anayeisema, naye atakuwa kama mujinga kwangu. ¹² Hivi vilevile kufuatana na vile munavyotamani sana zawadi za Roho, mujikaze kupata kwa uwingi zile zinazoweza kujenga kanisa katika imani. ¹³ Kwa hiyo yule anayesema kwa luga ya ajabu, aombe Mungu amupatie uwezo wa kuitafsiri. ¹⁴ Kwa maana kama nikiomba katika luga ya ajabu, roho yangu inaomba, lakini akili yangu haitumiki. ¹⁵ Basi ninapaswa kufanya nini? Nitaomba katika roho na katika akili vilevile. Nitaimba katika roho na katika akili vilevile. ¹⁶ Kwa maana kama ukimwomba Mungu ndani ya roho tu kwa kumushukuru, mtu asiyelewa kitu anayehuzuria katika mkutano hawezi kusema amina kwa kuitikia maombi yako ya kushukuru. Ni kwa sababu hasikii mambo unayosema. ¹⁷ Ijapokuwa ni kweli maombi yako ya kushukuru yanawezekana kuwa mazuri, lakini hayajengi mtu mwingine katika imani. ¹⁸ Ndiyo, ninamushukuru Mungu kwamba ninasema kwa luga za ajabu kuliko ninyi wote. ¹⁹ Lakini, katika mkutano ninapenda kusema maneno matano yenye kusikilika, kusudi niwafundishe wengine, kuliko kusema maneno elfu kumi kwa luga za ajabu. ²⁰ Wandugu zangu, musikuwe kama watoto kwa kufikiri: lakini katika mambo mabaya, iwatokee kutenda kama watoto wachanga. Inafaa mafikiri yenu yakuwe kama ya watu wazima. ²¹ Imelandikwa katika Sheria: «Bwana anasema: «Nitasema na watu hawa kwa njia ya wageni wenye luga ngeni Na hata hivi hawatanisikiliza.»» ²² Kwa hiyo, zawadi ya kusema luga za ajabu ni kitambulisho kwa wasioamini, lakini si kwa waamini. Na zawadi ya kutabiri ni kitambulisho kwa waamini, lakini si kwa wasioamini. ²³ Basi kama kanisa zima limekusanyika, na watu wote wanaanza kusema kwa luga za ajabu; na kisha watu wasioelewa kitu au wasioamini wakiingia katika mkutano wenu hawatasema kuwa ninyi ni wenda-wazimu? ²⁴ Lakini kama wote wakitabiri, na kama mtu mmoja asiyeamini au asiyelewa kitu anaingia, atapata uhakikisho kutokana na maneno ya hao wote. Naye atahukumiwa kufuatana na yote aliyosikia na ²⁵ kufichuliwa waziwazi mawazo yake aliyoficha. Na hivi atainama uso mpaka chini na kumwabudu Mungu, akisema: «Kweli Mungu ni katikati yenu!» ²⁶ Wandugu zangu, niseme nini basi? Wakati munapokusanyika kwa ibada, mmoja anaweza kuimba wimbo, mwingine kufundisha, mwingine kutoa ufunuo, mwingine kusema kwa luga za ajabu na mwingine anaweza kutafsiri. Na hayo yote yanapaswa kufanyika katika nia ya kujenga kanisa katika imani. ²⁷ Kukiwa wenye kusema kwa luga za ajabu, inafaa wasikuwe zaidi ya wawili au watatu, nao waseme mmoja kwa mmoja. Na tena kunapaswa kuwa mtu wa kutafsiri maneno wanayosema. ²⁸ Kama hakuna mtu anayetafsiri, basi kila mmoja wao anyamaze katika mkutano, aseme tu ndani ya moyo, yeye mwenyewe na Mungu. ²⁹ Na kwa upande wa wale wanaotabiri, wanaweza kusema wawili au watatu na watu wengine wapime yale wanayosema. ³⁰ Lakini kukiwa mtu anayesema, na mwingine anayekaa karibu akipata ufunuo, inafaa yule anayesema anyamaze. ³¹ Kwa maana ninyi wote munaweza kutabiri mmoja kwa mmoja, kusudi wote wapate kufundishwa na kutiwa moyo. ³² Moyo ya unabii inapaswa kuwa chini ya utawala wa yule aliyeipewa, ³³ kwa maana Mungu hataki sisi tuishi katika fujo, lakini katika amani. Sawa vile inavyokuwa desturi katika makanisa yote ya watu wa Mungu, ³⁴ wanawake wanapaswa kukaa kimya katika mikutano ya kanisa. Wao hawaruhusiwi kusema katika kanisa, lakini wanapaswa kutii sawa vile Sheria inavyosema. ³⁵ Kama wakiwa na neno la kuuliza, waulize waume wao kwenye nyumba zao. Ni haya kwa mwanamuke kusema katika mkutano wa kanisa. ³⁶ Munazani kwamba Neno la Mungu limetoka kwenu au limewafikia ninyi peke yenu tu? ³⁷ Kama mtu akizani kwamba yuko na zawadi ya unabii au zawadi ingine ya Roho, anapaswa kujua kwamba maneno haya ninayowaandikia ninyi ni amri ya Bwana. ³⁸ Lakini kama yeye

hajui vile, basi mtu asishugulike naye. ³⁹ Kwa hiyo wandugu zangu, mutamani sana kupata zawadi ya kutabiri, nanyi musiwazuize watu kusema kwa luga za ajabu. ⁴⁰ Lakini maneno yote yatendeke katika usawa na katika utaratibu.

Chapter 15

¹ Wandugu zangu, sasa ninataka kuwakumbusha Habari Njema niliyowatangazia, ile muliyopokea na kuishika imara. ² Nanyi kwa njia ya habari hiyo munaokolewa, ikiwa munaishika kufuatana na maneno niliyowahubiri. Kama isipokuwa hivi, muliamini bure. ³ Kwanza nimewatolea mafundisho haya ambayo mimi mwenyewe nilipokea: Kristo alikufa kwa sababu ya zambi zetu kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema. ⁴ Alizikwa na kufufuliwa kwa siku ya tatu kisha kufa kwake kama vile Maandiko Matakatiifu yanavyosema. ⁵ Alimutokea Petro, na kisha akawatokea mitume wake kumi na wawili. ⁶ Nyuma aliwatokea waamini zaidi ya mia tano pamoja, na wengi kati yao wangali wanaishi mpaka sasa, lakini wachache wamekwisha kufa. ⁷ Kisha alimutokea Yakobo, na nyuma akawatokea mitume wote. ⁸ Na kwa mwisho wa wote akanitokea mimi vilevile, mimi ninayekuwa kama mtoto aliyezaliwa pasipo kutimiza miezi. ⁹ Kwa maana mimi ni mudogo kati ya mitume wote, nami sistahili hata kuitwa mutume, kwa maana nilitesa kanisa la Mungu. ¹⁰ Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa sawa hivi ninavyokuwa, na neema yake niliyopewa haikukuwa ya bure, lakini nilitumika zaidi sana kuliko mitume wote wengine. Hakika si mimi, lakini ni neema ya Mungu inayokuwa pamoja nami. ¹¹ Basi, ikiwa ni mimi au ikiwa ni wao, hii ndiyo habari tunayohubiri na ndiyo muliyoamini. ¹² Ikiwa tunahubiri kuwa Kristo amefufuka, namna gani basi wengine kati yenu wanasema kama wafu hawatafufuka? ¹³ Basi ikiwa kweli wafu hawatafufuka, Kristo vilevile hakufufuka. ¹⁴ Na kama Kristo hakufufuka, mahubiri yetu ni ya bure na kuamini kwenu ni kwa bure vilevile. ¹⁵ Na zaidi ya hii, sisi tumeonekana kuwa washuhuda wa uongo mbele ya Mungu, kwa sababu tumeshuhudia kuwa Mungu amemufufua Kristo, ingawa hakumufufua, ikiwa kweli wafu hawafufuki. ¹⁶ Kwa maana kama wafu hawafufuki, basi Kristo naye hakufufuka. ¹⁷ Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni ya bure, na mungali katika zambi zenu. ¹⁸ Na zaidi ya hii, wale waliokufa wakiamini Kristo wamepotea kabisa. ¹⁹ Ikiwa tunamutumainia Kristo juu ya maisha haya ya sasa tu, sisi ni wamasikini kuliko watu wote. ²⁰ Lakini, kwa hakika Kristo amefufuka na hii inahakikisha kwamba wale waliokufa watafufuliwa vilevile. ²¹ Kwa maana, kama vile kifo kililetwa na mtu mmoja, vilevile ufufuko wa wafu unaletwa na mtu mmoja. ²² Kama vile watu wote wanavyokufa kwa sababu ya kuungana kwao na Adamu, vilevile wote wataishi tena kwa sababu ya kuungana kwao na Kristo. ²³ Lakini kila mtu atafufuka kufuatana na utaratibu wake; Kristo ndiye anayekuwa wa kwanza, na kisha watu wake watafufuka, wakati atakaporudia. ²⁴ Na nyuma ya pale, mwisho wa vyote utatimia. Wakati ule Kristo ataharibu utawala wote, mamlaka yote na uwezo wote, naye atamupatia Mungu Baba ufalme. ²⁵ Kwa maana Kristo anapaswa kutawala mpaka atakapowashinda waadui zake wote na kuwaweka chini ya miguu yake. ²⁶ Adui wa mwisho atakayeangamizwa ni kifo. ²⁷ Kwa maana Maandiko Matakatiifu yanasema: «Mungu aliweka vitu vyote chini ya miguu yake.» Ndiyo Maandiko Matakatiifu yanasema kwamba alipewa mamlaka juu ya vitu vyote. Lakini maneno haya yanaonyesha wazi kwamba Mungu hahesabiwi katika hili neno vyote, kwa maana ni yeye aliyemupa mamlaka juu ya vitu vyote. ²⁸ Na wakati vitu vyote vitakapokuwa vimewekwa chini ya mamlaka ya Mwana, halafu yeye mwenyewe atajiweka chini ya mamlaka ya Mungu aliyemupa mamlaka juu ya vitu vyote, kusudi Mungu apate kutawala juu ya vyote kabisa. ²⁹ Ikiwa hakuna ufufuko, wale wanaobatikwa kwa ajili ya wafu watafanya nini? Ikiwa wafu hawafufuki kabisa, kwa sababu gani watu wanabatikwa kwa ajili yao? ³⁰ Na sisi wenyewe, kwa nini tunahatarisha maisha yetu kila saa? ³¹ Wandugu zangu, kila siku ninapatwa na hatari ya kufa. Na hii ni hakika sawa vile ninavyojivuna kwa ajili yenu katika kuungana kwangu na Yesu Kristo Bwana wetu. ³² Ikiwa ni kwa nia ya kimtu, nimepigana na nyama wakali wa pori katika Efeso, jambo lile limenifalia nini? Kama wafu hawafufuki, basi: «Tukule na tukunywe, kwa maana kesho tutakufa. ³³ Musidanganyike: “Warafiki wabaya wanaharibu tabia nzuri za watu.”» ³⁴ Mugeuze mafikiri, murudie katika usawa, muache kufanya zambi. Ninasema neno hili kwa kuwapatisha haya, kwa sababu wamoja kati yenu hawamujui Mungu. Mwili wa ufufuko ³⁵ Lakini labda kuko mtu anayeweza kuuliza: «Namna gani wafu watafufuka? Nao watakuwa na mwili wa namna gani wakati ule watakaporudia?» ³⁶ Wewe muinga! Wakati unapopanda mbegu, mbegu ile haiwezi kuota isipokufa kwanza. ³⁷ Kile unachopanda si mumea mzima utakaopaswa kutokea nyuma, lakini ni punje tu, labda ya ngano au mbegu ingine fulani. ³⁸ Mungu anatokeza ndani ya ile punje umbo la mumea anaotaka; yeye anatokeza ndani ya kila mbegu umbo la kipekee. ³⁹ Miili ya viumbe vyote si sawa: watu wako na mwili wao wa kipekee, na nyama vilevile, na mwili wa ndege na samaki ni mbalimbali. ⁴⁰ Vilevile kuna miili ya mbinguni na miili ya dunia; nao uzuri wa miili ya mbinguni ni mbalimbali na uzuri wa miili ya dunia. ⁴¹ Uzuri wa jua ni mbalimbali na uzuri wa mwezi, nao uzuri wa nyota ni mbalimbali, kwa maana hata nyota zinapishana uzuri vilevile. ⁴² Itakuwa hivi vilevile wakati wafu watakapofufuka. Mwili unazikwa katika udongo katika hali ya kuharibika, lakini unapofufuka, unafufuka na hali ya kutoweza kuharibika ⁴³ na hali ya utukufu; nao unazikwa katika uzaifu, lakini unafufuka na nguvu. ⁴⁴ Wakati

unapozikwa ni mwili wa kimtu, lakini unapofufuka unageuka mwili wa kiroho. Kama kuna mwili wa kimtu, basi kuna mwili wa kiroho vilevile. ⁴⁵ Kwa maana, Maandiko Matakatiifu yanasema: «Mtu wa kwanza, Adamu, alikuwa kiumbe chenye uzima»; lakini Adamu wa mwisho ni Roho anayewapatia watu uzima. ⁴⁶ Si mwili wa kiroho unaotangulia lakini ni mwili wa kimtu, kisha ule wa kiroho unafuata. ⁴⁷ Adamu wa kwanza aliumbwa kwa udongo, yeye ni wa dunia, lakini Adamu wa pili alitoka mbinguni. ⁴⁸ Watu wa dunia wanafanana na yule aliyeumbwa kwa udongo, na watu wa mbinguni wanafanana na yule aliyetoka mbinguni. ⁴⁹ Na kama vile tulivyofanana na yule mtu aliyeumbwa kwa udongo, vilevile tutafanana na yule aliyetoka mbinguni. ayopata kwa ajili ya Bwana hayatapita bure. ⁵⁰ Wandugu zangu, muangalie, jambo ninalotaka kusema ni hili: kile kilichoumbwa kwa nyama na damu hakiwezi kupata urizi katika Ufalme wa Mungu katika hali ile, wala hakuna chenye hali ya kuharibika kinachoweza kuwa na hali ya kutoharibika. ⁵¹ Sasa nitawaambia ninyi siri: sisi wote hatutakufa, lakini sisi wote tutabadilishwa ⁵² kwa rafla, kama vile mtu anavyofunga jicho na kulifungua, wakati ngunga ya mwisho itakapolia. Kwa maana wakati itakapolia, wafu watafufuka na kupata kuwa katika hali ya kutoweza kufa tena, na sisi wote tutabadilishwa. ⁵³ Kwa maana sherti mwili huu wa kuharibika uvae mwili wa kutoharibika, na mwili wa kufa sherti uvae mwili wa kutokufa. ⁵⁴ Na wakati mwili huu wa kuharibika utakapovaa ule wa kutoharibika, nao mwili wa kufa utakapovaa ule wa kutokufa, halafu Maandiko Matakatiifu haya yatatimia: «Kifo kimekomesha; kimeshindwa kabisa. ⁵⁵ Ewe kifo, ushindi wako uko wapi? Ewe kifo, uwezo wako wa kuua uko wapi?» ⁵⁶ Kifo kinapata uwezo wa kuua kutokana na zambi, na zambi inapata uwezo wake kutokana na Sheria. ⁵⁷ Lakini tumushukuru Mungu anayetupatia ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. ⁵⁸ Basi wandugu zangu wapenzi, musimame imara bila kutikisika. Muendeleo kumutumikia Bwana siku zote, mukijua kwamba masumbuko munayopata kwa ajili ya Bwana hayatapita bure.

Chapter 16

¹ Sasa juu ya muchango unaofanyika kwa ajili ya watu watakatifu wa Mungu wanaokuwa Yerusalema; ninyi vilevile mufanye sawa vile nilivyoagiza makanisa ya Galatia. ² Kila siku ya kwanza ya juma, kila mmoja wenu anapaswa kuweka akiba ya mali kwake, kwa kadiri ya mapato yake, kusudi musihitaji kufanya muchango wakati nitakapokuja. ³ Nami nitakapofika, nitatuma watu mutakaochagua, pamoja na barua kwa kupeleka zawadi yenu Yerusalema. ⁴ Ikiwa ni lazima mimi niende vilevile, basi nitasafiri pamoja nao. ⁵ Nitakuja kwenu kisha kupitia Makedonia kufuatana na mupango wangu wa kupitia kule. ⁶ Labda nitabakia pamoja nanyi muda kidogo, au tena wakati wote wa mvua kali; kusudi muweze kunisaidia kuendelea pahali popote nitakapokwenda. ⁷ Kwa maana sitaki kuonana nanyi kwa kupita tu. Ninatumaini kukaa pamoja nanyi siku chache Bwana akitaka. ⁸ Lakini, ninataka kubakia hapa Efeso, mpaka siku ya Pentekoste. ⁹ Kwa maana mulango moja umefunguliwa, nimepata hapa wakati mzuri wa kufanya kazi kubwa ijapokuwa wapinzani ni wengi. ¹⁰ Kama Timoteo akifika, mujikaze kumupokea vizuri kati yenu kwa sababu yeye anafanya kazi ya Bwana kama mimi mwenyewe. ¹¹ Basi hata mtu mmoja asimuzarau. Lakini mumusaidie aendelee na safari yake katika amani; kusudi apate kurudia kwangu, maana ninamungojea yeye pamoja na wandugu waamini. ¹² Kwa ngambo ya ndugu yetu Apolo, nimemusihi sana akuje kwenu pamoja na wandugu wengine, lakini hakutaka kabisa kwenda sasa; atakwenda kwa wakati utakaomupendeza. ¹³ Mukeshe, musimame imara katika imani, mukuwe hodari na wenye nguvu. ¹⁴ Mutende mambo yenu yote katika upendo. ¹⁵ Ninyi munajua Stefana na jamaa yake; munafahamu kwamba walikuwa watu wa kwanza walioamini katika inchi ya Akaya, nao wamejitoea kwa kutumikia watu wa Mungu. Hivi ninawasihi sana wandugu zangu, ¹⁶ mukubali kuongozwa na watu kama hawa na wale wote wanaotumika na bidii pamoja nao. ¹⁷ Nami ninafurahi kwa kufika kwa Stefana, Fortunato na Akaiko; wamekuwa kwa pahali penu, ¹⁸ nao wamenifariji kama vile walivyowafariji ninyi wenyewe. Inafaa kuwakumbuka watu kama hawa. ¹⁹ Makanisa ya jimbo la Azia yanawasalimia. Akila na Prisila pamoja na kanisa linalokusanyika ndani ya nyumba yao wanawasalimia sana katika Bwana. ²⁰ Wandugu wote wanaokuwa hapa wanawasalimia. Na ninyi vilevile musalimiane kwa upendo wa kikristo. ²¹ Hii ni salamu ninayoiandika kwa mukono wangu mimi Paulo mwenyewe. ²² Kama mtu hamupendi Bwana, alaaniwe! Bwana wetu, kujaa! ²³ Neema ya Bwana Yesu ikuwe pamoja nanyi. ²⁴ Ninawapenda ninyi wote katika kuungana na Yesu Kristo.

Book: 2 Corinthians

2 Corinthians

Chapter 1

¹ Barua hii inatoka kwangu mimi Paulo na kwa ndugu yetu Timoteo. Mimi ambaye kwa mapenzi ya Mungu, niliitwa kuwa mutume wa Kristo Yesu. Tunawaandikia kanisa la Mungu linalokuwa Korinto na watu wake wote wanaokuwa katika jimbo lote la Akaya. ² Tunawatakiya neema na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. ³ Asifiwe Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo, Baba mwenye kujaa huruma na Mungu anayefariji katika mambo yote! ⁴ Yeye anatumfariji katika taabu yetu yote, kusudi tupate kuwafariji wale wanaokuwa katika taabu yoyote kwa kuwaletea faraja tuliyopokea kutoka kwa Mungu. ⁵ Basi, kwa kadiri tunavyoshiriki katika mateso mengi ya Kristo, ni kwa kadiri ile sisi vilevile tunafarijiwa sana kwa njia ya Kristo. ⁶ Kama sisi tunapata taabu ni kusudi mupate kufarijiwa na kuokolewa. Kama tunafarijiwa ninyi vilevile munafarijiwa na kupata nguvu ya kuwawezesha kuvumilia taabu ile ile tunayopata. ⁷ Kwa hivi, hatuwezi kukata tumaini tunalokuwa nalo kwenu, kwa maana tunajua kwamba kwa kuwa munashiriki katika taabu yetu, munashiriki vilevile katika kufarijiwa kwetu. ⁸ Wandugu, tunataka mujue taabu tuliyopata katika jimbo la Azia. Taabu ile ilitulemea sana hata tukakata tumaini lote la kuendelea kuishi. ⁹ Tulikuwa tumefikiri kwamba tulihukumiwa kufa. Basi, ilitokea hivi kusudi tusijitegemee sisi wenyewe, lakini tumutegemee Mungu tu anayefufua wafu. ¹⁰ Yeye ndiye aliyetuopoa toka hatari kubwa sana ya kufa, naye atatuopoa tena. Nasi tunamutumainia kwamba ataendelea kutuopoa, ¹¹ nanyi wenyewe mutatusaidia kwa njia ya maombi. Kwa hivi Mungu atajibu kwa maombi yaliyotolewa na watu wengi kwa ajili yetu na kututendea wema, na watu wengi watamushukuru kwa ajili yetu. ¹² Jambo ambalo tunajivunia ni hili: zamiri yetu inayotuhakikishia kwamba tumeishi katika dunia na zaidi kati yenu katika uaminifu na ukweli tulivyojaliwa na Mungu. Sisi hatukuongozwa na hekima ya kimtu lakini na neema ya Mungu. ¹³ Basi katika barua zetu tunawaandikia tu mambo yale munayoweza kusoma na kufahamu. Ninatumaini kwamba mutafahamu mambo haya kabisa, ¹⁴ maana munayafahamu sasa kwa sehemu tu. Kwa Siku ile ya kurudi kwa Bwana wetu Yesu mutaweza kujivuna kwa ajili yetu kama vile tutakavyojivuna kwa ajili yenu. ¹⁵ Katika tumaini hili nilikusudia kufika kwenu kwanza kusudi mupate furaha mara mbili. ¹⁶ Nilikusudia kupitia kwenu kwa kwenda Makedonia, kisha ningewaona tena wakati wa kurudia, kwa hiyo mungenisaidia kwa safari yangu kwenda Yudea. ¹⁷ Basi, nilipokusudia kubadilisha mupango wangu mimi nimekuwa kama kigeugeu? Wakati ninapofanya mipango yangu, mimi ninaongozwa na mafikiri ya kimtu hata nipate kusema Ndiyo na Hapana kwa mara moja? ¹⁸ Kama vile Mungu anavyokuwa mwaminifu, hakika mambo tuliyowaambia hayakukuwa ya kusema Ndiyo na Hapana kwa mara moja. ¹⁹ Kwa maana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu ambaye Silvano, Timoteo na mimi mwenyewe tuliyemuhubiri kwenu hakukuja kusema Ndiyo na Hapana. Lakini yeye ni Ndiyo inayotoka kwa Mungu. ²⁰ Maana yeye ndiye anayetimiza ahadi zote za Mungu. Vilevile ni kwa njia ya Yesu Kristo tunasema Amina kwa kumutukuza Mungu. ²¹ Ni Mungu mwenyewe ndiye anayetumainisha pamoja nanyi katika ushirika na Kristo, na ni yeye mwenyewe ndiye aliyetuchagua. ²² Ameweka kitambulisho juu yetu kinachohakikisha kama sisi ni watu wake na kuweka Roho Mtakatifu ndani yetu kuwa rehani ya vitu vyote anavyotuwekea. ²³ Ninamutaja Mungu kuwa mushuhuda wangu, yeye anajua roho yangu! Mimi nilikusudia kutorudia tena Korinto kwa sababu ya kuwasikilia huruma. ²⁴ Hatutafuti kuwaamuru ninyi juu ya mambo yale munayopaswa kuamini, maana munasimama imara katika imani. Lakini tunataka kutumika pamoja nanyi kusudi mupate kufurahi.

Chapter 2

¹ Basi, nilikusudia kutorudia tena kwenu nikiwa mwenye huzuni. ² Kwa maana kama nikiwahuzunisha ninyi, ni nani atakayenifurahisha tena, isipokuwa tu wale niliowahuzunisha? ³ Ni kwa sababu hii niliwaandikia kwamba sitakuja tena kwenu nishuzunishwe na watu waliopaswa kunifurahisha. Maana nina uhakika kwamba mimi ninapofurahi, ninyi wote munafurahi vilevile. ⁴ Niliwaandikia nikiwa mwenye kusikitika sana na mwenye kufazaika moyoni nikilia machozi mengi, si kwa kuwahuzunisha ninyi, lakini ni kusudi mupate kujua namna gani ninavyowapenda. ⁵ Kulikuwa mtu aliyefanya mambo ya kuhuzunisha, hakunihuzunisha mimi, lakini amewahuzunisha ninyi wote au bila kwenda mbali zaidi wamoja kati yenu. ⁶ Azabu mtu yule aliyopewa na watu wengi kati yenu inatosha kwake. ⁷ Basi sasa ni afazali kumusamehe na kumufariji, na kuepuka asikate kitumaini kwa sababu ya huzuni kubwa. ⁸ Kwa hiyo ninawasihi ninyi kuhakikisha upendo wenu kwa mtu yule. ⁹ Kwa maana shabaha yangu ya kuwaandikia ile barua ni kutaka kuwapima nipate kujua kwamba muko tayari kunitii siku zote. ¹⁰ Wakati munaposamehe mtu, nami ninamusamehe vilevile. Kwa maana kama ninasamehe, na ikiwa kweli ninakuwa na neno lolote la kusamehe, ninasamehe mbele ya Kristo kwa ajili yenu, ¹¹ kusudi Shetani asipate njia ya kutushinda, maana tunajua nia zake. ¹² Wakati nilipofika katika mji Troa kwa kutangaza Habari Njema ya Kristo, Bwana alifungua mulango wa kutumika kule. ¹³ Ingawa vile, nilifazaika sana kwa sababu sikumukuta ndugu yangu Tito. Halafu nikaagana na watu wa mji ule na kwenda Makedonia. ¹⁴ Lakini Mungu ashukuriwe, maana yeye ndiye anayetupatia ushindi siku zote katika ushirika wetu pamoja na Kristo. Anatutumia sisi kwa kutambulisha Kristo pahali pote kama vile harufu nzuri ya marasi inavyosambaa popote. ¹⁵ Kwa maana sisi ni kama harufu nzuri iliyotolewa na Kristo kwa Mungu; na kunukia wale wanaookolewa na wale wanaopotea. ¹⁶ Kwa wale wanaopotea ni harufu ya kifo inayoleta kifo; lakini kwa wale wanaookolewa, ni harufu ya uzima inayoleta uzima. Basi nani anayekuwa na uwezo wa kutimiza kazi ya namna hii? ¹⁷ Basi sisi si kama wengine wengi wanaochuza neno la Mungu; lakini kwa sababu Mungu ndiye aliyetutuma, sisi tunasema ukweli mbele yake, kama vile watumishi wa Kristo.

Chapter 3

¹ Maneno haya yanaonyesha kwamba tunaanza kujisifu tena sisi wenyewe? Au tunahitaji kuwatolea ninyi barua za ushuhuda au kuziomba kwenu kama wengine? ² Ninyi wenyewe ni kama barua yetu ya ushuhuda iliyoandikwa katika mioyo yetu na watu wote wanaweza kuitambua na kuisoma. ³ Inaonekana wazi kwamba ninyi ni barua iliyoandikwa na Kristo na kutumwa kwa njia ya utumishi wetu. Barua hii inaandikwa si kwa wino, lakini kwa Roho wa Mungu Mwenye Uzima. Barua hiyo haikuandikwa juu ya vibao vya mawe, lakini katika mioyo ya watu. ⁴ Tunasema neno hili kwa ajili ya tumaini tunalokuwa nalo kwa Mungu kwa njia ya Kristo. ⁵ Si kusema kwamba sisi wenyewe tuko na uwezo wa kujitungia jambo hili, lakini uwezo wetu unatoka kwa Mungu. ⁶ Kwa maana Mungu ndiye aliyetuwezesha kuwa watumishi wa agano jipya, lisilotokana na Sheria iliyoandikwa, lakini na Roho. Sheria iliyoandikwa inaleta kifo lakini Roho analeta uzima. ⁷ Sheria ile inayoleta kifo imeandikwa neno kwa neno juu ya vibao vya mawe na utukufu wa Mungu ulingaa wakati ule. Uso wa Musa ukangaa vilevile hata Waisraeli hawakuweza kuangalia uso wake ingawa kungaa kule kulikuwa kwa muda tu. ⁸ Basi si zaidi sana matokeo ya utumishi wa Roho yatakuwa yenye utukufu? ⁹ Ikiwa utumishi unaowaletea watu hukumu ulikuwa na utukufu, basi si zaidi sana utumishi unaowafanya watu wahesabiwe haki mbele ya Mungu, utakuwa na utukufu mkubwa zaidi? ¹⁰ Tunaweza kusema kwamba ule utukufu ulionгаа zamani hauwezi kulinganishwa na utukufu wa sasa unaokuwa mkubwa zaidi. ¹¹ Kwa maana kama mambo yaliyokuwa ya muda tu yalipata utukufu, basi yale yanayodumu ni yenye utukufu zaidi. ¹² Na kwa sababu tunakuwa na tumaini lile, sisi tunasema kwa uhodari. ¹³ Sisi hatufanyi kama Musa alivyokuwa akifunika uso wake na kitambaa kwa kuzuiza Waisraeli wasiangalie mwisho wa utukufu uliokuwa wa muda tu. ¹⁴ Lakini akili yao ilikuwa nzito kwa kufahamu. Kwa maana mpaka sasa, Waisraeli wanaposoma katika vitabu vya Agano la Kale, akili yao inafunikwa na kitambaa kile kile. Kitambaa kile kitaondolewa tu kwa mtu anayeungana na Kristo. ¹⁵ Mpaka sasa, kila mara wanaposoma katika vitabu vya Musa, kitambaa kinafunika mioyo yao. ¹⁶ Lakini Wakati mtu anapomrudilia Bwana, kitambaa kile kinaondolewa. ¹⁷ Hapa Bwana ni Roho; na pahali Roho wa Bwana anapokaa, pale kuna uhuru. ¹⁸ Sisi wote ambao uso haukufunikwa, tunaonyesha kama kioo utukufu wa Bwana. Kwa hiyo, tunabadilishwa kwa kufanana na Bwana, nasi tunapita toka utukufu mmoja hata utukufu mwingine unaokuwa mkubwa zaidi tena. Kwa maana kazi hii inatimizwa na Bwana ndiye Roho.

Chapter 4

¹ Kwa wema wake, Mungu ametupatia utumishi huu, na kwa sababu hii sisi hatukati tumaini. ² Tumekataa mambo ya kisirisiri na ya haya. Hatuna mwenendo wa udanganyifu wala hatupotowi neno la Mungu. Lakini tunajulisha waziwazi ukweli kusudi tuvute kila mtu kutuaminia katika zamiri yake mbele ya Mungu. ³ Lakini kama Habari Njema tunayotangaza ni ngumu kwa kusikia, ni kwa wale tu wanaofuata njia ya upotevu. ⁴ Wao hawaamini kwa sababu yule mungu wa dunia hii amefunika akili zao. Yeye anawazuiza wasione mwangaza unaoletwa na Habari Njema ya utukufu wa Kristo, anayefanana na Mungu. ⁵ Kwa maana, hatutangazi habari zetu sisi wenyewe, lakini tunatangaza kwamba Yesu Kristo ndiye Bwana, nasi tuko watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. ⁶ Yule Mungu aliyesema: «Mwangaza uangaze katika giza,» ndiye aliyeangaza ndani ya mioyo yetu, na kutuwezesha kufahamu utukufu wa Mungu unaongaa kwenye uso wa Kristo. ⁷ Lakini sisi tunaokuwa na hazina hii ya kiroho, tuko vyombo vya udongo, kusudi watu waone waziwazi uwezo huu wa ajabu sana unaotoka kwa Mungu lakini si kwetu sisi wenyewe. ⁸ Sisi tunagandamizwa kila namna, lakini hatushindwi; tunahangaishwa, lakini hatukati tumaini; ⁹ tunateswa, lakini Mungu hatuachilii; tunatupwa chini, lakini hatuangamizwi. ¹⁰ Kila wakati tunabeba mateso ya kufa kwa Yesu katika mwili wetu, kusudi uzima wa Yesu uonekane vilevile ndani ya mwili wetu. ¹¹ Kwa maana katika maisha yetu, tunakuwa kila mara katika hatari ya kufa kwa ajili ya Yesu, kusudi uzima wake uonekane vilevile katika mwili wetu unaokuwa wa kufa. ¹² Kwa hivi, kifo kinafanya kazi ndani yetu, lakini uzima unafanya kazi ndani yenu. ¹³ Maandiko Matakatifu yanasema: «Niliamini ndiyo maana nilisema.» Sisi vilevile kwa moyo tunakuwa na imani ile ile, ndiyo maana tunasema. ¹⁴ Tunajua kwamba Mungu aliyemufufua Bwana Yesu atatufufua sisi vilevile pamoja na Yesu. Yeye atatufikisha pamoja nanyi mbele ya Yesu. ¹⁵ Kwa maana mambo haya yote yanafika kwa ajili yenu kusudi neema ya Mungu izidishwe kwa watu wengi siku zote, nao wapate kumutolea Mungu shukrani nyingi kwa ajili ya utukufu wake. ¹⁶ Kwa sababu hii hatukati tumaini hata kidogo. Ijapokuwa hali yetu ya kimwili inaharibika, hali yetu ya kiroho inafanywa upya siku kwa siku. ¹⁷ Kwa maana taabu tunayopata ni ndogo na ya muda tu, inatutayarishia utukufu mkubwa sana na wa milele unaokuwa mzuri zaidi kupita mateso haya. ¹⁸ Maana sisi hatuangalii vitu vile vinavyoonekana, lakini vitu visivyoonekana. Kwa sababu vile vinavyoonekana vinadumu muda kidogo tu, lakini vile visivyoonekana, vinadumu milele.

Chapter 5

¹ Kwa maana, tunajua kwamba hema hii tunayoishi ndani yake hapa katika dunia, maana yake mwili wetu, itakapobomolewa, Mungu atatupatia makao mengine mbinguni. Nayo ni nyumba aliyoienga yeye mwenyewe na inayodumu milele. ² Na sasa katika hali hii tunaugua kwa maana tunatamani sana kuvaa makao yetu yanayotoka mbinguni. ³ Kwa maana, tukisha kuyavaa hatutaonekana tena kuwa uchi. ⁴ Hakika kwa wakati wowote tungali tunaishi katika makao haya ya dunia, tunaugua kwa kulemewa. Si kwa sababu tunataka kuondolewa mwili wa dunia, lakini tunataka kuvaa mwili wa mbinguni, kusudi uzima wa milele upate kubadilisha miili yetu inayokuwa ya kufa. ⁵ Ni Mungu mwenyewe aliyetuwezesha kupata mabadiliko hayo na kuweka Roho Mtakatifu ndani yetu kuwa rehani ya vitu vyote anavyotuwekea. ⁶ Basi tuna uhodari siku zote. Tunajua kwamba wakati tunapoishi katika mwili huu, tunaishi mbali na makao ya Bwana. ⁷ Kwa maana tunaishi kwa imani lakini si kwa kuona. ⁸ Sisi tuna uhodari na tungependa zaidi kutoka katika mwili huu na kwenda kuishi pamoja na Bwana. ⁹ Lakini mbele ya yote tunataka sana kumupendeza Bwana, ikiwa tunakaa au kutoka katika mwili huu. ¹⁰ Kwa maana sisi wote tunapaswa kusimama kwa kusambishwa mbele ya tribinali ya Kristo, kusudi kila mtu alipwe kufuatana na matendo yake mema au mabaya aliyofanya alipokuwa akiishi ndani ya mwili wake. ¹¹ Basi, kwa sababu tunajua kwamba ni lazima kumwogopa Bwana, ndiyo maana tunajitoa kuwavuta watu kwake. Mungu anatumjua waziwazi nami ninatumaini kwamba ninyi wenyewe munatumjua waziwazi vilevile. ¹² Sisi hatuanzi tena kujisifu wenyewe mbele yenu, lakini tunawapa ninyi sababu ya kuweza kujivuna kwa ajili yetu. Hivi tena munaweza kupata maneno ya kuwajibu wale wanaojivunia tu hali yao ya inje, lakini si mambo yanayokuwa ndani ya mioyo yao. ¹³ Ikiwa kweli tunaonekana kuwa wenda-wazimu, ni kwa ajili ya Mungu, lakini kama sisi ni wenye akili sawa, ni kwa faida yenu. ¹⁴ Maana upendo wa Kristo unatuongoza sisi tunaokubali kwamba ni mtu mmoja tu ndiye aliyekufa kwa ajili ya watu wote; maana yake wote wanashiriki katika kifo chake. ¹⁵ Naye alikufa kwa ajili ya watu wote, kusudi wale wanaoishi, wasiishi kwa ajili yao wenyewe, lakini kwa ajili ya yule aliyekufa na kufufuka kwa ajili yao. ¹⁶ Kwa hiyo basi, tangu sasa hatumuhesabu tena mtu yeyote kufuatana na hali ya kimtu. Hata ikiwa tulimuhesabu Kristo kufuatana na hali ya kimtu, kwa sasa hatumuhesabu tena kufuatana na hali ile. ¹⁷ Basi mtu yeyote anapoungana na Kristo, yeye anakuwa kiumbe kipya. Mambo ya zamani yametoweka, na sasa hali mupya imefika. ¹⁸ Mambo haya yote yalifanyika na Mungu, aliyetupatanisha naye kwa njia ya Kristo na kutupatia kazi ya kuongoza watu wengine wapatane naye. ¹⁹ Ndiyo kusema, Mungu ndiye aliyekuwa akipatanisha watu wote na yeye mwenyewe kwa njia ya Kristo bila kuhesabu makosa yao. Yeye ametupatia ujumbe wa upatanisho. ²⁰ Basi sisi ni wajumbe wa Kristo. Kwa njia yetu, Mungu mwenyewe anawaita ninyi; na kwa hiyo tunawasihi katika jina la Kristo, mukubali kupatanishwa na Mungu. ²¹ Kwa maana Kristo alikuwa bila zambi, lakini Mungu alimubebesha muzigo wa zambi zetu, kusudi kwa njia yake tupate kuwa wenye haki mbele ya Mungu.

Chapter 6

¹ Basi, sisi tunaotumika pamoja na Mungu, tunawasihi musipoteze bure neema muliyopokea kwake. ² Kwa maana Mungu anasema hivi katika Maandiko Matakatifu: «Kwa wakati uliofaa, nilijibu maombi yako. Kwa siku ya wokovu, nilikusaidia.» Basi sasa, huu ndio wakati unaofaa, sasa leo ni siku ya wokovu. ³ Sisi hatutaki kumukwaza mtu yeyote katika jambo lolote kusudi kazi yetu isizarauliwe. ⁴ Lakini tunaonyesha katika mambo yote kwamba sisi ni watumishi wa Mungu: tumedumu sana katika mateso, katika ukosefu na katika taabu. ⁵ Tumepigwa, tumetiwa ndani ya kifungo, wamefanya fujo juu yetu, tumefanya kazi ngumu, tumekoseshwa usingizi na kukaa bila kula. ⁶ Tunaonyesha kwamba sisi ni watumishi wa Mungu kwa njia ya usafi wa moyo wetu, ya ufahamu, ya uvumilivu, ya wema wetu, ya Roho Mtakatifu, ya upendo wetu wa kweli, ⁷ ya ujumbe wa neno la kweli, na ya uwezo wa Mungu. Tunatumia kama vile silaha mambo ya haki kwa kushambulia na kujikinga. ⁸ Tunaheshimiwa na kuzarauliwa, tunatukanwa na kusifiwa. Tunahesabiwa kama wenye kusema uongo, ingawa sisi tunasema ukweli, ⁹ kama watu wasiojulikana ingawa tunajulikana vizuri, kama wanaokufa ingawa sisi ni wazima. Tunaazibiwa lakini hatuuawi, ¹⁰ tunahuzunishwa lakini tunafurahi siku zote. Tunaonekana kama wamasikini lakini tunatajirisha watu wengi, hatuna kitu, lakini tunakuwa na vitu vyote. ¹¹ Ee ninyi Wakorinto! Tumesema nanyi waziwazi na tumewafungulia kabisa moyo wetu. ¹² Sisi hatukuwafungia mioyo yetu, lakini ni ninyi ndio muliotufungia moyo wenu. ¹³ Sasa ninasema nanyi kama vile watoto wangu: kwa ngambo yenu mutufungulie nasi moyo wenu vilevile. ¹⁴ Musishirikiane pamoja na watu wasioamini. Kwa maana kuna ushirika gani kati ya haki na uovu? Kuna mapatano gani kati ya mwangaza na giza? ¹⁵ Kuna masikilizano gani kati ya Kristo na Beliari? Au mtu anayeamini yuko na ushirika gani na mtu asiyeamini? ¹⁶ Kuna ulinganisho gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi ni hekalu la Mungu Mwenye Uzima kama vile yeye mwenyewe alivyosema: «Nitakaa na kuishi pamoja nao, nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. ¹⁷ Kwa sababu hiyo Bwana anasema: “Mutoke kati yao, mujitenge nao. Musiguse kitu chochote kinachohesabiwa kuwa kichafu, nami nitawapokea. ¹⁸ Nitakuwa Baba yenu nanyi mutakuwa wana na wabinti wangu. Ni mimi Bwana Mwenye Uwezo ninayesema.”»

Chapter 7

¹ Basi wapendwa wangu, kwa kuwa tumepewa ahadi hizi zote, tujitakase toka uchafu wote unaochafua mwili na roho na tujikaze kuwa watakatifu kabisa tukiishi katika kumuogopa Mungu. ² Mutufungulie moyo wenu! Hatukumukosea mtu yeyote, hatukumunyanganya mtu yeyote, wala kumupotosha mtu yeyote. ³ Sisemi vile kwa kuwahukumu. Kwa maana, kama vile nilivyokwisha kusema, ninyi ni wapendwa wetu, muko mioyoni mwetu katika kuishi au katika kufa. ⁴ Mimi ninawaaminia sana na kujivuna kwa ajili yenu. Katika mateso yetu yote, ninafarijiwa sana na kujazwa na furaha. ⁵ Kwa maana hata wakati tulipofika Makedonia, hatukuweza kupumzika hata kidogo. Tulipata taabu pande zote: magomvi pamoja na watu wengine, na woga katika moyo wetu. ⁶ Lakini Mungu anayefariji watu wanyenyekevu, ametufariji kwa njia ya kufika kwa Tito. ⁷ Nasi hatukufarijiwa kwa kuja kwake tu, lakini vilevile kwa namna ile mulivyomufariji. Tito ametuelezea jinsi munavyokuwa na hamu kubwa ya kuniona, jinsi munavyohuzunika na jinsi munavyojitoa kwa ajili yangu. Kwa hivi sasa ninafurahi zaidi. ⁸ Basi, ikiwa nimewahuzunisha na barua yangu, sijuti juu yake sasa. Nilijuta wakati nilipotambua kwamba barua ile iliwahuzunisha ingawa ilikuwa ni kwa muda tu. ⁹ Sasa ninafurahi, si kwa sababu muliweza kuhuzunika, lakini kwa sababu huzuni yenu imewawezesha kugeuka toka katika zambi. Kwa maana mumehuzunishwa kufuatana na mupango wa Mungu. Kwa hivi hatukuwatendea ubaya wowote. ¹⁰ Basi, huzuni inayosababishwa na Mungu inamuwezesha mtu kugeuka toka katika zambi. Na kugeuka kule, kunamuletea kuokoka. Kule kuokoka hakuleti majuto. Lakini huzuni inayosababishwa na mwanadamu inaleta kifo. ¹¹ Basi, muangalie sasa matokeo ya ile huzuni inayosababishwa na Mungu! Imewafanya kuwa wenye bidii sana, wenye kujitetea, wenye kuonyesha kwamba hamuna kosa, wenye utii, wenye hamu kubwa ya kuniona, wenye kujitoa kwa ajili yangu na wenye kutaka kabisa kuazibu ubaya. Mumeonyesha katika njia zote kwamba hamukukuwa na kosa katika mambo haya. ¹² Basi ikiwa nimewaandikia, si kwa ajili ya yule aliyefanya kosa au si kwa ajili ya yule aliyemukosea. Lakini kusudi mupate kutambua waziwazi mbele ya Mungu bidii munayokuwa nayo kwa ajili yetu. ¹³ Hii ndiyo maana tumefarijiwa. Lakini zaidi ya kufarijiwa kwetu tulifurahi tena sana kwa ajili ya furaha ya moyo Tito aliyokuwa nayo kufuatana na jinsi mulivyomutuliza. ¹⁴ Mimi nimejivuna kidogo mbele yake kwa ajili yenu, nami sikupata haya. Lakini kama vile tulikuwa tunawaambia kila mara ukweli, vilevile kule kujisifu kwetu kwa ajili yenu mbele ya Tito, kumeonekana kuwa kwa kweli. ¹⁵ Mapendo yake kwa ajili yenu yanazidi kuongezeka anapokumbuka vile mulivyokuwa tayari kumutii na vile mulivyomupokea kwa woga na kutetemeka. ¹⁶ Ninafurahi sana kwa sababu ninaweza kuwaaminia katika kila jambo.

Chapter 8

¹ Wandugu, tunapenda kuwajulisha namna Mungu alivyojalia neema makanisa ya Makedonia. ² Yalijaribiwa sana kwa njia ya mateso mengi yaliyopata. Lakini yalizidi kuwa na furaha hata yakakuwa na moyo wa kutoa kupita kipimo, ingawa yalikuwa masikini sana. ³ Ninayashuhudia kwamba kwa mapenzi yao yalitoa kwa kadiri yalivyoweza na hata zaidi kupita uwezo wao. ⁴ Yalitusihi sana tukishiriki nayo katika kazi ya kuwasaidia watu wa Mungu wanaokaa Yudea. ⁵ Yalitoa kupita vile tulivyokuwa tukitumaini! Kwanza yalijitoa yenyewe kwa ajili ya kazi ya Bwana, kisha yakajitoa kwa ajili yetu vilevile kufuatana na mapenzi ya Mungu. ⁶ Ni kwa hiyo tulimusihiti Tito atimize kazi hiyo ya kuwaongoza ninyi kuwa na moyo wa kutoa sawa alivyoianzisha. ⁷ Ninyi munakuwa na kila kitu kwa uwingi: imani, usemi, ufahamu, kuwa na bidii ya kila namna na upendo munaokuwa nao kwetu. Kufuatana na hiyo mukuwe vilevile na uwingi katika kazi hii ya kuwa na moyo wa kutoa. ⁸ Sisemi hivi kwa kuwaamuru, lakini kwa njia ya kuwaelezea habari za bidii ya wengine, ninataka kuwapima kusudi upendo wenu upate kutambulikana kuwa wa kweli. ⁹ Kwa maana munajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, ingawa alikuwa tajiri, yeye mwenyewe alijifanya masikini kwa ajili yenu, kusudi mupate kuwa watajiri kwa njia ya umaskini wake. ¹⁰ Kuelekea jambo hilo, mimi ninawatolea shauri, nalo linafaa kwenu, kwa maana ni ninyi muliokuwa wa kwanza kukusudia kufanya kazi ile na kuianzisha tangu mwaka jana. ¹¹ Sasa muendelea nayo na kuitimiza. Kama vile mulivyokuwa na moyo mwema wa kukusudia kuifanya, basi mukuwe na moyo mwema wa kuitimiza kufuatana na uwezo wa mali munayokuwa nayo. ¹² Kwa maana kama mtu akiwa na moyo wa kutoa, Mungu anakubali kitu anachotoa kufuatana na kile anachokuwa nacho, wala si kufuatana na kile asichokuwa nacho. ¹³ Nia yangu si kusema kwamba munapaswa kujitia katika taabu kwa ajili ya kusaidia watu wengine, lakini inafaa kuwe usawa. ¹⁴ Na sasa ninyi muko na mapato mengi zaidi, basi munaweza kuwasaidia wale wanaokuwa katika mahitaji. Hivi wao vilevile watakapokuwa na mapato mengi wataweza kuwasaidia katika siku za mahitaji. Kwa hiyo kutakuwa usawa ¹⁵ kama vile Maandiko Matakatifu yanavyosema: «Yule aliyeokota kingi hakukuwa na cha zaidi, na aliyeokota kidogo, hakupungukiwa.» Tito na wenzake ¹⁶ Shukrani kwa Mungu aliyetia bidii moyoni mwa Tito ya kuwasaidia kama vile sisi tunavyokuwa nayo! ¹⁷ Amekubali ombi letu, na zaidi ya ile ameondoka kuja huko kwenu kwa bidii yake kubwa na kutokana na mapenzi yake mwenyewe. ¹⁸ Pamoja naye tunamutuma ndugu anayesifiwa na makanisa yote kwa ajili ya kazi yake ya kuhubiri Habari Njema. ¹⁹ Vilevile, yule ndugu amechaguliwa na makanisa kwa kutusindikiza katika safari ya kutimiza kazi hii ya kutoa kwa moyo mwema ambayo sisi tunafanya kwa ajili ya utukufu wa Bwana, na kwa kuonyesha nia yetu ya kusaidia watu wengine. ²⁰ Tunaepuka kushitakiwa na watu wengine juu ya mali mingi kama hii tunayochunga. ²¹ Kwa maana tunataka kufanya mema, si mbele ya Bwana tu, lakini mbele ya watu vilevile. ²² Tunatuma ndugu yetu mwingine pamoja nao. Sisi tumemupima mara nyingi na ameonyesha siku zote kwamba yeye ni mwenye bidii sana. Na sasa, yeye ni mwenye bidii zaidi tena kwa kuwa anawaaminia ninyi sana. ²³ Kwa ngambo ya Tito, yeye ni mwenzangu, ninafanya kazi pamoja naye kwa ajili yenu. Nao wale wandugu wengine wanaomusindikiza, ni wajumbe wa makanisa wanaotumika kwa ajili ya utukufu wa Kristo. ²⁴ Kwa hiyo muonyeshe mbele ya makanisa kwamba hakika munawapenda na kuyafahamisha kwamba tulikuwa na haki ya kujivuna kwa ajili yenu.

Chapter 9

¹ Si lazima niwaandikie juu ya musaada unaotumwa kwa watu wa Mungu wanaokuwa katika Yudea. ² Kwa maana ninajua nia yenu nzuri ya kusaidia, nami ninajivuna kwa ajili yenu mbele ya watu wa Makedonia, nikisema: «Kanisa la jimbo la Akaya liko tayari kusaidia tangia mwaka jana.» Hivi kwa njia ya bidii yenu mumewavuta wengi kati yao kwa kutoa vilevile. ³ Lakini sasa ninawatumia wandugu hawa kusudi kujisifu kwetu kwa ajili yenu kusioneke kuwa bure. Kwa hiyo ninataka mukuwe tayari kama vile nilivyosema. ⁴ Kwa maana kama watu wa Makedonia wanakuja pamoja nami na tusipowakuta tayari, sisi tutapata haya sana kwa kuona jinsi nilivyowaaminia, nami sisemi kitu juu ya haya ambayo ninyi mutaweza kupata. ⁵ Ni hivi niliona kuwa ni vizuri kuwashauri wandugu hawa watangulie kufika kwenu mbele yangu kusudi watayarisha vile vitu mulivyoahidi kutoa kwa mapenzi yenu. Hivi vitakuwa tayari na itaonyesha kwamba mumevitoa kwa moyo mwema, wala si kwa uchoyo. ⁶ Mukumbuke maneno haya: yule anayepanda kidogo atavuna kidogo, na yule anayepanda kwa uwingi atavuna kwa uwingi. ⁷ Basi inafaa kila mtu atoe sawa alivyokusudia moyoni, si kwa huzuni wala si kwa kulazimishwa. Kwa maana Mungu anapenda mtu yule anayetoa kwa furaha. ⁸ Na Mungu anaweza kuwajalia mema ya kila namna, kusudi siku zote mupate vyote munavyohitaji, na hivi mupate kuzidi kutoshelewa katika kutenda kazi njema. ⁹ Kama vile inavyoandikwa katika Maandiko Matakatiifu: «Ametoa kwa uwingi, amewapa wamasikini. Haki yake inadumu milele.» ¹⁰ Mungu ndiye anayemupatia mupandaji mbegu na mukate wa kukula. Kwa hiyo atawapatia ninyi mbegu yoyote munayohitaji na kuiotesha, kusudi moyo wenu wa kutoa upate kuzaa matunda mengi ya haki yenu. ¹¹ Hivi mutakuwa watajiri katika vitu vyote, kusudi siku zote muweze kuonyesha moyo wa kutoa, hata watu wengi watamushukuru Mungu kwa ajili ya musaada tunaowafikishia kutoka kwenu. ¹² Kwa maana kazi hii ya kutoa munayofanya haifai tu kwa kusaidia watu wa Mungu kusudi wapate vitu wanavyokosa, lakini vilevile kwa njia ile watu wengi wanamutolea Mungu shukrani. ¹³ Kufuatana na ushuhuda wa kazi hii, watu watamutukuza Mungu kwa kuona jinsi munavyoonyesha utii wenu katika kushika Habari Njema ya Kristo. Vilevile wanamutukuza kwa kuona moyo wa kutoa munaokuwa nao katika kushirikiana mali yenu pamoja nao na sisi. ¹⁴ Kwa hiyo watawaombea kwa upendo mwingi, kwa ajili ya neema kubwa sana Mungu aliyowajalia. ¹⁵ Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya zawadi yake inayopita kipimo!

Chapter 10

¹ Sasa mimi Paulo mwenyewe ninawaomba kwa upole na kwa wema sawa na ule wa Kristo; mimi yule ambaye wanasema juu yake kwamba ni mupole wakati ninapokuwa pamoja nanyi, lakini ni mukali wakati ninapokuwa mbali nanyi. ² Ninawasihi kwamba nitakapofika kwenu, musinisukume kuwa mukali. Kwa maana nina uhakika kwamba nitawatendea vile wale watu wote wanaozania kwamba sisi tunaishi maisha ya kimwili. ³ Kwa maana ijapokuwa tunaishi katika dunia, lakini hatufanyi vita kwa namna ya kimwili. ⁴ Silaha tunazotumia katika vita si za kimwili, lakini silaha zetu ni uwezo wa Mungu unaoweza kuharibu upango wa adui. Tunaharibu mawazo ya uongo na ⁵ kuangusha vizuizo vyote watu wanavyojivunia kwa kupinga elimu ya Mungu. Tunatawala mafikiri ya watu na kuyafanya yapate kumutii Kristo. ⁶ Sisi tuko tayari kuazibu kila kitendo cha uasi, mutakapoonyesha kwamba munatii kabisa. ⁷ Ninyi munaangalia tu namna vitu vinavyoonekana kwa inje. Mtu yeyote anayejiaminia kwamba yeye ni wa Kristo, inafaa afikiri tena yeye mwenyewe mambo haya: ikiwa yeye ni wa Kristo sisi vilevile ni wa Kristo. ⁸ Kwa maana sioni haya hata kama nimejivuna zaidi kwa ajili ya uwezo Bwana aliotupatia sisi. Kwa maana uwezo ule ni kwa ajili ya kuwajenga katika imani, lakini si wa kubomoa. ⁹ Sitaki kuonekana kwamba ninataka kuwaogopesha kwa barua zangu. ¹⁰ Kwa sababu wengi wanasema: «Barua za Paulo ni kali na zenye maneno mazito; lakini yeye mwenyewe anapokuwa katikati yetu ni muzaifu na namna yake ya kusema ni ya kuzarauliwa.» ¹¹ Inafaa mtu yule anayesema vile ajue vema kwamba hakuna tofauti kati ya maneno tunayoandika katika barua zetu wakati tunapokuwa mbali, na yale tutakayofanya wakati tutakapokuwa pamoja nanyi. ¹² Kwa kweli hatungesubutu kujifananisha au kujilinganisha na watu wale wanaojisifu wenyewe. Wao ni wapumbafu. Wanajipima kufuatana na kipimo chao wenyewe na kujilinganisha na wao wenyewe. ¹³ Sisi hatutajivuna kupita kipimo, lakini tunataka kutumia kile kipimo cha kazi ile Mungu aliyotupatia na iliyotufikisha vilevile mpaka kwenu. ¹⁴ Hatutambuki mipaka yetu sawa vile hatukufika kwenu. Kwa maana tulifika kwenu, tukiwatangazia Habari Njema ya Kristo. ¹⁵ Basi, hatujivuni kupita kipimo juu ya kazi ya watu wengine. Lakini tunatumaini kwamba imani yenu itakapokuwa ikiongezeka, tutaweza kufanya kazi kubwa zaidi kati yenu kufuatana na kipimo cha kazi tuliyopewa na Mungu. ¹⁶ Kisha tutaweza kuhubiri Habari Njema katika inchi zinazokuwa mbali kupita inchi yenu, kuliko kujisifu juu ya kazi watu wengine waliyokwisha kufanya kufuatana na kipimo walichopewa. ¹⁷ Lakini, kama Maandiko Matakatiifu yanavyosema: «Anayetaka kujivuna, ajivune kwa ajili ya Bwana.» ¹⁸ Kwa maana, mtu anayekubaliwa si yule anayejisifu mwenyewe, lakini ni yule anayesifiwa na Bwana.

Chapter 11

¹ Ingekuwa heri muvumilie kidogo masemi yangu ya upumbavu! Ninawaomba kweli munivumilie! ² Mimi ninasikia wivu kwa ajili yenu sawa vile Mungu anavyousikia vilevile. Kwa maana ninyi ni kama binti mukamilifu niliyemwowesha kwa mume mmoja, ndiye Kristo. ³ Lakini ninaogopa kwamba sawa vile nyoka alivyomudanganya Eva kwa werevu wake, mawazo yenu vilevile yasipotoshwe hata mupate kupoteza uaminifu na ukamilifu wenu kwa Kristo. ⁴ Hii inatokana na kuona jinsi munavyomukubali mtu yeyote anayekuja kwenu na kuwahubiri habari za Yesu mwingine asiye kuwa yule sisi tuliyemuhubiri. Na zaidi ya hii munakubali upesi kupokea roho ingine na ujumbe mwingine vinavyokuwa tofauti na Roho au Habari Njema muliyopokea toka kwetu. ⁵ Ninazani kwamba wale mitume wanaohesabiwa kuwa wakubwa zaidi hawanipiti kitu kabisa. ⁶ Inaonekana kuwa mimi si mtu anayeelewa kusema, lakini kwa ngambo ya elimu, mimi ninaielewa sana. Nasi tumeonyesha hayo yote kila wakati na katika mambo yote. ⁷ Mimi niliwatangazia Habari Njema ya Mungu bila kudai mushahara. Nilijinyenyekeza kusudi mupate kutukuzwa. Basi kwa kujinyenyekeza vile, nilifanya kosa? ⁸ Nilipokuwa nikitumika kati yenu nililipwa na makanisa mengine. Ni kama vile nilinyanganya mali ya makanisa yale na kuitumia kwa kuwasaidia. ⁹ Wakati nilipokuwa kwenu, sikumulemea mtu yeyote nilipohitaji kitu fulani, kwa maana wandugu waliotoka Makedonia waliniletea vitu vyote nilivyohitaji. Nilijiangalia vizuri katika mambo yote kusudi nisiwalemee, nami nitaendelea kujiangalia vema. ¹⁰ Kufuatana na vile ninavyosema ukweli kama vile Kristo, ninaapa kwamba hakuna anayeweza kunizuiza kujivuna juu ya jambo hilo katika jimbo lote la Akaya. ¹¹ Kwa sababu gani ninasema hivi? Kwa sababu siwapendi? Hapana, Mungu anajua kwamba ninawapenda. ¹² Nitaendelea kufanya sawasawa ninavyofanya kwa sasa, kusudi niwafungie njia zote wale wanaotafuta kujivuna kwamba wanatumika sawa sisi. ¹³ Watu wale ni mitume wa uongo, wanafanya kazi yao kwa udanganyifu wakijisingizia kuwa mitume wa kweli wa Kristo. ¹⁴ Na jambo hilo si la kushangaza kwa maana Shetani mwenyewe anajisingizia kuwa malaika wa mwangaza. ¹⁵ Basi si jambo la ajabu kama watumishi wake vilevile wanajigeuza kuwa watumishi wa haki. Kwa mwisho wao watalipwa kufuatana na matendo yao. ¹⁶ Mimi ninasema tena: mtu asinizanie kuwa mupumbavu. Kama si vile, basi munihesabu kama mupumbavu, kusudi nami nipate kujivuna kidogo vilevile. ¹⁷ Maneno haya ninayosema sasa hayafuatani na mapenzi ya Bwana, lakini ninayasema tu kama mupumbavu kuelekea jambo hili la kujivuna. ¹⁸ Watu wengi wanajivuna kwa namna ya kimwili, kwa sababu hiyo mimi nitajivuna vilevile. ¹⁹ Ninyi munajidai kuwa wenye hekima na ndiyo maana munapenda kuwavumilia wapumbavu! ²⁰ Munavumilia hata mtu anayewatia katika utumwa, anayeiba mali zenu, anayewagandamiza, anayewazarau na anayewapiga kofi kwenye uso. ²¹ Ninasikia haya ya kuisema: tumekuwa zaifu kwa kufanya vile! Lakini kama watu wengine wanasubutu kujivuna juu ya kitu chochote, mimi vilevile nitajivuna. Sasa ninasema kama vile mupumbavu. ²² Watu wale ni Waebrania? Mimi vilevile. Wao ni Waisraeli? Mimi vilevile. Wao ni wa uzao wa Abrahamu? Mimi vilevile. ²³ Sasa nitasema kama mwenda-wazimu: wao ni watumishi wa Kristo? Mimi ni mtumishi wake zaidi kuliko wao. Nimetumika kazi nyingi zaidi, nimefungwa mara nyingi zaidi, nimepigwa zaidi, na mara nyingi nimekuwa katika hatari ya kufa. ²⁴ Mara tano Wayuda wamenipiga viboko makumi tatu na tisa. ²⁵ Waroma wamenipiga fimbo mara tatu na mara moja walitaka kuniua kwa kunitupia mawe. Mara tatu chombo nilichosafiri nacho kilizama kwa kuvunjika. Mara moja, nilishinda ndani ya bahari kwa muda wa siku nzima. ²⁶ Katika safari zangu nyingi nimepata hatari ya mafuriko ya mito, hatari ya wanyanganyi, hatari kutoka kwa wanainchi wenzangu na kutoka kwa watu wa mataifa mengine. Nilikuwa katika hatari ndani ya miji, katika jangwa, katika bahari na kati ya wandugu za uongo. ²⁷ Nimesumbuka kwa kufanya kazi ngumu, nimepata magumu, nimekesha mara nyingi. Mara nyingi niliteswa na njaa na kiu; mara nyingi nililazimishwa kutokula. Nimeteseka na baridi na ukosefu wa nguo. ²⁸ Na bila kutaja mambo yote mengine kama hayo, kila siku ninashugulika na makanisa yote. ²⁹ Kukiwa mtu anayepatwa na uzaifu, mimi ninajisikia muzaifu vilevile. Kukiwa mtu anayeanguka katika zambi, ninasikia uchungu. ³⁰ Kama ikinipasa kujivuna nitajivuna kwa ajili ya uzaifu wangu. ³¹ Mungu Baba ya Bwana Yesu, anayetukuzwa hata milele, anajua kwamba sisemi uongo. ³² Wakati nilipokuwa Damasiki, liwali wa mfalme Areta aliweka walinzi katika mji ule kusudi wanikamate. ³³ Lakini wakanitia ndani ya kitunga na kunishusha kwenye ukuta wa mji, tokea ndani ya dirisha, nami nikapata kuponyoka.

Chapter 12

¹ Basi nitaendelea kujivuna ijapokuwa si vizuri. Lakini nitasema sasa juu ya maono na ufunuo nilivyopata toka kwa Bwana. ² Ninamujua mtu mmoja aliyeungana na Kristo, na sasa kumekwisha kupita miaka kumi na mine, mtu huyu akanyanyuliwa mpaka katika mbingu ya tatu. (Ikiwa alinyanyuliwa katika hali ya kimwili au ya kiroho mimi sijui, Mungu peke yake anajua.) ³ Nami ninajua kwamba mtu yule alinyanyuliwa mpaka katika Paradizo. (Ninasema tena ikiwa mtu yule alinyanyuliwa katika hali ya kimwili au ya kiroho mimi sijui, Mungu peke yake anajua.) ⁴ Katika Paradizo, mtu yule akasikia mambo ya ajabu na yasiyoruhusiwa kwa mwanadamu kuyaeleza. ⁵ Basi, nitajivuna kwa ajili ya mtu sawa na yule, lakini sitajivuna kwa ajili yangu mimi mwenyewe, isipokuwa tu kwa ajili ya uzaifu wangu. ⁶ Kama ningetaka kujivuna, singekuwa mupumbavu, maana ningesema tu ukweli. Lakini ninaepuka kujivuna, kusudi watu wasinihesabu kuwa mkubwa kuliko vile wanavyoona nikifanya au kunisikia nikisema. ⁷ Lakini, kusudi nisijivune kupita kipimo kwa ajili ya kupokea ufunuo wa ajabu, nilitiwa katika mwili wangu kitu kinachoniumiza kama mwiba. Kitu kile ni kama mujumbe wa Shetani kwa kunipiga na kunizuiza nisijivune kupita kipimo. ⁸ Nami nilimusih Bwana mara tatu kusudi aniondolee kitu kile. ⁹ Lakini akanijibu: «Neema yangu inakutoshelea, kwa maana uwezo wangu unatimizwa katika uzaifu.» Basi tafazali nijivunie sana uzaifu wangu kusudi nijazwe na uwezo wa Kristo. ¹⁰ Kwa sababu hii ninafurahia uzaifu, matusi, ukosefu, taabu na mateso kwa ajili ya Kristo. Kwa maana wakati ninapokuwa muzaifu, basi ndio wakati ule ninapokuwa na nguvu. ¹¹ Ninasema kama mupumbavu, lakini ni ninyi ndio mumenilazimisha kufanya vile. Kufuatana na ile, ningepaswa kusifiwa nanyi. Kwa maana hata kama mimi si kitu, wale mitume wenu wanaohesabiwa kuwa wakubwa hawanipiti kitu kabisa. ¹² Matendo yanayohakikisha kwamba mimi ni mutume yamefanyika kati yenu kwa uvumilivu wote, kwa njia ya miujiza, maajabu, na vitambulisho. ¹³ Mumpungukiwa na nini kuliko makanisa mengine, isipokuwa tu kwamba mimi sikuwalemea kwa kupata musaada toka kwenu? Munisamehe kwa kosa hili. ¹⁴ Sasa mimi niko tayari kufika kwenu kwa mara ya tatu, nami sitawalemea. Maana sihitaji mali yenu, lakini ninawahitaji ninyi. Kwa sababu si kazi ya watoto kuwawekea wazazi wao akiba, lakini ni kazi ya wazazi kuwawekea watoto wao akiba. ¹⁵ Kwa ngambo yangu, nitafurahi kutumia vyote ninavyokuwa navyo na kujitoa mimi mwenyewe, kwa ajili yenu. Ikiwa ninawapenda zaidi namna hii, hamupaswi kupungukiwa na upendo kwangu. ¹⁶ Basi mutakubali kwamba mimi sikuwalemea. Lakini watu wengine wanafikiri kwamba mimi ni mwerevu na nimewanasa kwa kuwadanganya. ¹⁷ Basi niliwaibia ninyi kwa njia ya mtu mmoja kati ya wale niliowatuma kwenu? ¹⁸ Nilimusih Tito aende kwenu na nimemutuma pamoja na ndugu mwingine. Munaweza kusema kwamba Tito amewaibia ninyi? Basi mimi pamoja naye tuliishi katika nia moja na kuwa na mwenendo mmoja. ¹⁹ Ninyi munazani kwamba kwa wakati huu wote sisi tunajitetea mbele yenu? Tunasema mambo yale mbele ya Mungu kufuatana na vile tunavyoongana na Kristo. Wandugu wapendwa, mambo yale yote ni kwa kuwajenga ninyi katika imani. ²⁰ Kwa maana ninaogopa kwamba wakati ninapokuja kwenu, sitawakuta sawa vile ninavyotaka, nanyi hamutanikuta sawa vile munavyotaka. Ninaogopa kuwakuta katika fitina, wivu, kasirani, ugomvi, masingiziano, matetano, majivuno na fujo. ²¹ Ninaogopa kwamba kwa safari yangu ingine, Mungu wangu atanifanya tena kuwa mwenye haya mbele yenu. Nami nitalia kwa ajili ya watu wengi waliofanya zambi zamani nao hawakugeuka toka katika uasherati, uzinzi na tamaa mbaya walizofanya.

Chapter 13

¹ Hii ni safari yangu ya tatu ninayotayarisha kuja kwenu. Kama Maandiko Matakatiifu yanavyosema: «Kila neno linapaswa kuhakikishwa kwa ushuhuda wa watu wawili au watatu.» ² Kwa wakati huu ninapokuwa mbali nanyi, ninarudilia kuwaambia waziwazi maneno yale niliyokuwa nimekwisha kuwaambia mbele katika safari yangu ya pili niliyofanya kwenu. Ninawaambia kwamba nitakapokuja kwenu mara tena, sitakosa kuazibu wale waliofanya zambi zamani na wengine wote. ³ Nitafanya vile kwa sababu ninyi munataka uhakikisho kwamba Kristo anasema kwa njia yangu. Kwenu Kristo si zaifu, lakini anaonyesha uwezo wake kati yenu. ⁴ Ni kweli Kristo alitundikwa juu ya musalaba katika hali ya uzaifu wa mwili, lakini sasa anaishi kwa uwezo wa Mungu. Nasi katika kuungana kwetu naye sisi vilevile tunakuwa zaifu. Lakini kwa ajili yenu tunaishi pamoja naye kwa nguvu ya Mungu. ⁵ Mujichunguze ninyi wenyewe kusudi mupate kujua kama munasimama imara katika imani. Mujipime. Si munajua kwamba Yesu Kristo anakaa kati yenu? Kama si vile ni kusema kwamba mumeshindwa. ⁶ Lakini ninatumaini kwamba ninyi mutajua kwamba sisi hatukushindwa. ⁷ Nasi tunaomba Mungu kusudi musifanye jambo lolote baya, nasi hatutaki kuonyesha kwamba tumeshinda. Lakini tunataka mutende mema hata ikionekana kuwa sisi tunashindwa. ⁸ Kwa maana hatuwezi kufanya jambo lolote linalopingana na ukweli. Jambo tunaloweza tu ni kuendelea ukweli. ⁹ Tunafurahi wakati ninyi munapokuwa na nguvu, hata ikiwa sisi ni zaifu. Nasi tunawaomba kusudi mupate kuwa wakamilifu. ¹⁰ Ni kwa hiyo ninawaandikia maneno haya nikiwa mbali nanyi, kusudi wakati nitakapokuwa kati yenu nisitende kwa ukali kadiri ya mamlaka Bwana aliyonipa. Kwa maana uwezo ule ni kwa ajili ya kuwajenga katika imani, lakini si wa kubomoa. ¹¹ Basi kwa kumaliza, wandugu zangu, kwa heri. Mujikaze kuwa wakamilifu, mufarijiane ninyi kwa ninyi, mukuwe na nia moja, muishi katika amani, na Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi. ¹² Musalimiane kwa upendo wa kikristo. Watu wote wa Mungu wanawasalimia. ¹³ Tunawatakia ninyi. ¹⁴ Wote neema kutoka kwa Bwana Yesu Kristo, na upendo wa Mungu na ushirika wa Roho Mtakatifu.

Book: Galatians

Galatians

Chapter 1

¹ Mimi Paulo mutume kupisa Yesu Kristo mwengye we na Mungu baba mwenye alimufufuata kutoka mubafu. ² Ivi nikona baandikia nyie kanisa ya kule Galati tuko na bandugu bengine. ³ Neema na amani ikue kwenu kuto ka kwa Mungu baba na bwana wetu Yesu, ⁴ mupakaliwa mwenye aliji toa ye mwenyewe ju ya makosa na zambi yetu, kusudi atu okowe mwa hezi siku za mwisho zenye zina kuwa mbaya, kupi kupitia mapenzi ya Mungu Baba ye peke. ⁵ Tuna mu rudishia sifa na mi lele. ⁶ Mina shangala sana kuona mwenye ali baitaka na hamukukua na stahili, laki ni pupitia neema ya Yesu mupakaliwa wake, sa mina shanga moyo inaluma kuona muna feuka na kufuata enjili ingine muna acha habari jema yake. ⁷ Siseme kama kuko ingine habari yenu lakin kuko batu benye biko na ba vuruga, na kutaka ku haribisha enjili ya Yesu mupakaliwa. ⁸ Lakini mutu moja ndini yetu, ao ata ni malaika mwenye ata jaribukuwa fundisha ingine enjili tafauti na habari njema ya Yesu mutakaliwa, hugo na alainiwe. ⁹ Kama vile tulisema mbele, mina rudilia tena "alainiwe" mutu mwenye ata jaribu kuwa fundisha ingine enjili tofauti na habari nje ma ya Yesu mupakaliwa. ¹⁰ Sasa nikona tafuta anipatie alama? kama nikitafuta batu sifie, siko kabisa mutumishi wa Yesu mupakaliwa wa Mungu. ¹¹ Ndugu, nataka mujie kama, habari nje ma yenye nili hubiri, hakutoka wa batu ya dunia. ¹² Haiko bo njo bali nifu hundisha nayo. Lakini bwana Yesu mwenye ali ni funuliaka nayo. ¹³ Mulisikia maisha nili kuaka nayo mu dini ya kiyahudi, gisi nili kua na tesa na kusumbuo sana kanisa la Mungu. ¹⁴ Nili kua naendelea sana mwa ile dini kushinda bote benye bali nitanguliaka. Nili kua na Juhudi kubwa sana mu mila ya ba tate yangu. ¹⁵ Lakini Mungu ye peke alinichagua kwa mapenzi yake kutoka tomoya mama yangu. Ali miita kupilia neema yake. ¹⁶ Kusudi anitambulishe mtoto wake, kusudi ni tangaze kwa mataifa sikuuliza ata mutu wala kitu. ¹⁷ Siku kimbilia kulezea benye bali ni tanguliaka katika hudu ma ya kitume, lakini nilienda mbele kwa wa harabu na nika rudia tena Dameski. ¹⁸ Na kiisha myaka tatu njo nika hika sasa Yerusaleme kusudi ni muone Petro, na nikabakia naye ya pata siku kumi na tano. ¹⁹ Lakini siku ona bengine bamitume, kama sio tu Yakobo ndugu yake na bwana. ²⁰ Ile ni kweli nawaambia siku sema bongo. ²¹ Kisha nilienda mu majumbo za suria na silisia. ²² Mekaniso za Bwana zenye zili kua kule Yudea hazi kuniju. ²³ Balikwa na ni sitia kwa jina tu na byenye nilikuwaka na fanya baka kua na shangala, na kusema, ule mwenye alikuaka na tu tesa ju ya enjili, ye peke ana hubiri ile imani ye nye alikuaka na tafuta kuzuiya. ²⁴ Maka nisa zilikuwa na shukuru Mungu.

Chapter 2

¹ Nyuma ya mpaka kumi na ine (14 ans) nili rudia tena Yerusalemu pamoja na Barnaba, na sika tela Tito pia. ² Nili pandaka ju Mungu ali niambiaka mu maana aseme niende kule niliba fasiria juya habari njema yznye nili kwaka na hubiri mu bapagani, lakini batu ya hesima, nilikua na baambilia pembeni. Nili penda ni hakikishe siku fanya kazi ya bure. ³ Kwanzi Tito mwenye tuli kua naye, sikumushurutisha ata hiriwe. ⁴ Ha takma kulikua bandugu ba bongo bali kuya kisirisiri kusudi bapeleleze gisi gani tuko muru ndani ya Yesu. Balitaka fanya batumwa ba sheria. ⁵ Hatu kubaachia hata ka wakati kadogo kusidi basi badilishe ukueli wa habari njena ndani yenu. ⁶ Lakini benye batu bote balikua naita biongozi habaku ni saidia na kitu, gisi banaishi faida kwangu. Mungu hana upendeleo. ⁷ Balitambua Mungu alinita nitangazi habari njena kwa wapagani kama vile Petro aliituwaka kuhubiri wa yahudi walio tahiriwa, ⁸ kwa sababu Mungu mwenye alitumikisha Petro kwa kuhubiri ba yahudi, alitumikisha namiye nihubiri mataiwa. ⁹ Wakati bali tambua kama niko na neema ya Mungu, Yakobo, Petro na Yohane, benye balikua biongozi waka tupatia mukono wa kuume mie na Barnaba kama alama yakutukubala kusudi twende kwa wapagani kuhubiri; nababakie kuhubiri bayahidi. ¹⁰ Baka tu ambia lukumbuke na wa wakosefu na njo ilikua niayangu sana. ¹¹ Wakati kefa alifika Antikia, nilimupiga sana wazi wazi, na nilikua na sheria ju mbele, alikuaka na kula na bapagani bakule Antiokia. ¹² Lakini wakati aliona bandugu benye Yakobo ali kuaka natuma banafika, akatumia unafiki ju ya haya na bongo mbele ya bale yahudi akaji tenga na bale bapagani ba Antikia sawa hakula nabo. ¹³ Njo bengine bote ba kiyahudi, ba kina Barnaba baka jiunga na ile bunafikiya kefa. ¹⁴ Lakini wakati nili tambua kama habatembee tena na ukweli ya habari njema, ni ka muambia kefa mbele bo «Kama weye muyahudi unaishi sawa mupagani, namuna gani uta sukuma bale bapagani baige mufono ya ba yahudi?» ¹⁵ Shiepe benye tuko bayahudi baki zalikio benye tunajitapa kama hatuko bapagani, ¹⁶ tujue kama hakuna mwenye ana shuudiwa ju ya matendo mazuri, lakini tuli shuhudiwa na imani katika Yesu mupakaliwo lakini hiko kwa matendo ya sheria. ¹⁷ Lakini wakati tuna tafula kwamba Mungu atashuhudie ndani ya Yesu Kristo tuna jikuta shipeke ni wa fanya zambi! sasa Yesu ni mutumishi wa zambi? Hakika apana. ¹⁸ Kwa sababu ni niki fanya tena zambize nye niko na kataza batu, mipeke mitena murunja haki na amri. ¹⁹ NI liji katalia bile ya masheria masheria kusudi niishi tu ju ya Mungu. ²⁰ Nili tundikwa pamoja na Yesu. Haiko mingo haishi tena lakini Kristo njo anaishi ndani yangu, ivi ningali mu mwili kwa leo, niko na ishikwa imani ndani ya Mwana wa Mungu mwenyi alinipendaka, akajitoa ye pake ju ya yangu. ²¹ Si wezi tupitia neema ya Mungu kwa sababu kama haki engekua mu masheria, halafukifo ya Yesu ku musalaba hainge kwa na maana.

Chapter 3

¹ Bagalatia bajinga, nani mwenye ali baloga? maono ni ya Yesu kristo mwenye alifufykaka njo nibaletiaka. ² Nilitakatu kuji funza kitu kimoja kwenyu, muli pataka hoho takatifu kwa matendo ya sheria ao kwa imani katika ule mwenye tuli bahubiri habari njema yake? . ³ Mungu muliakoka na mukakua batu ya Mungu , munataka tena rudie kua bapagani tena? ⁴ Ni kusema mateso yenu ilikua ya bure? . ⁵ Sasa mwenye alilimiza ile kazi ndani yenu, aliifanya kwa nja ya sharia, wala kwa kusikia na kuamimi neno? . ⁶ « Abrahamu» aliamini Mungu, akaitia mwenye haki. ⁷ Muelewe sasaa kama bote benye banaamini, ni batoto ba Abrahamu . ⁸ Bibilia ina sema kama Mungu ata shuhudia bapa gani kupitia imani yabo , Habari njema ilifikiaika Abrahamu kusema, kupitia weye mataifayote itabari kwa. ⁹ Hwi basi bote benye kua na imani, bana barikiwo pamoja na Abrahamu. ¹⁰ Bote benye kulazamia kazi za sharia baria:«Alaamiwe kila mwenye hato shika ma ayizo ya sheria». ¹¹ Sasa inaone kama wazi kama Mungu hashuhudie mutu kupitia sheria sababu«mwenye haki ataishi kwa imoni» . ¹² shiria hai tokei katika imani, mwenye ana heshimu maneno ya sheria njo anaishi na ma sheria - sheria». Shiria hai tokei katika imani,« mwenye ana heshimu manemo ya sheria njo anaishi na ma sheria sheria». ¹³ Kristo alituo kowa toka chini ya laana ya sheria wakati ali jifanya ye peke kuwa loana, ju yetu, Sababu inaandikwa «alaaniwe mwenye ata kae tundi kwa ku miti». ¹⁴ Shabaha yake ilikua kusema ile baraka yenye ika ndani ya Abrahamu, ifikie wa pagani kwa njo ya Yesu -Kristo, kusudi tu pate ile ahadi ya Roho kupitia imani. ¹⁵ Wandugu, nina sena sema kama mutu sawa vile pia mapatano yenye ili wekwa na batu, halaina mutu mwenye ana weza kutosha wala kuongaye ahadiza Mungu. ¹⁶ Sasa ahadi ilipatitiwa Abrahamuna kizazi yake« Mungu hakusema kwa vizazi, tusizame ju ya batu yote lakini Muzaliwa moja ndie Yesu-Kristo. ¹⁷ Sasa nana sema hivi, patano yenye Mungu ali kamilisha tangu mwanzo haiwezi ondoshewa na sheria yenye ilifika kisha myaka mia ine na makumi tatu. ¹⁸ Sababu inpelikua wizi ili kuyaka kupitia sheria isaka hange kua mwizi wa Abrahamu lakini Mungu yepeke alipatia ka Abraham murizi kupitia. ¹⁹ kwa nini sasa sheria ilikua? ili ongezwabababu bavinja sheriya mpaka ule muzaliwa wa Abramufike. ²⁰ Sababu mopatanishi ana kusanyaka batu batu mingi takini Mungu ni Mumoja. ²¹ Hivi sasa shiria, ina lingana na ahadi? hapana kabisa! sababu ingekua sheria ina weza leta uzima. Haki inge kua mu duma kupitia ile sheria. ²² Lakini mandiko ili kusanya bile byole chini ya mamlaka ya zamba njo ahadi ya Mungu kutu fungu la kupitia imoni katika Yesu-Kristo ika patiwa kwa wale wa nao amini ²³ La mbele ile imani katika Kristo ifike, tuli kua muma busu yenye kuchungwa na sheria mpaka wakati imani ile funuliwa. ²⁴ kwa hiyo, tu libakia mpa siku ²⁵ Yesu za Yesu zi timilike kusude, tifunguliwe kwa imani. Sasa, ivi tayari imani iko, hatu kotena chini ya ule mulinzi. ²⁶ kwa sababu muko nye bote bato ya baba Abrahamu kupitia imani katika Yesu-Kristo. ²⁷ Bate be nye bali batiziwaka katika jina la Kristo bana kua sura yake, hakuna tena tafauti kati ya batu . ²⁸ Ukabila haipashwe tena kuoneka na ndani Yesu, Mukubwa wala Mudogo, Mwanaume na mwanu muke, sababu muko umoja ndani ya Kristo. ²⁹ Kama muko batu ya Kristo, ni kusema muko rizi ile ahadi.

Chapter 4

¹ Kwa sababu hiyo, tunapaswa kushikamana zaidi na habari tuliyosikia, kusudi tusipotee mbali. ² Ujumbe wa Sheria uliotangazwa na malaika ulitimizwa, na hata kila mtu aliyekosa kuufuata na kuasi aliazibiwa sawa inavyostahili. ³ Basi, namna gani sisi tutaponyoka azabu kama hatushuguliki na wokovu mkubwa kama huu? Ni Bwana mwenyewe aliyetangaza kwanza habari za wokovu huu, na wale waliomusikia walihakikisha kwetu kwamba ni za kweli. ⁴ Mungu vilevile alihakikisha ushuhuda wao kwa njia ya maajabu, ya miujiza mbalimbali, na ya vitambulisho, na kwa njia ya zawadi za Roho Mtakatifu alizowapa watu kama anavyopenda. Mwongozi wa wokovu ⁵ Mungu hakuwapa wamalaika uwezo wa kutawala ulimwengu unaokuja, ndio ule tunaosema juu yake. ⁶ Tena maneno haya yanahakikishwa na pahali pengine katika Maandiko Matakatifu: «Mtu ni nini hata umukumbuke, mwanadamu ni nini hata umushugulikie? ⁷ Umemufanya kuwa mwenye cheo chini kidogo ya malaika. Umemujaza utukufu na heshimaa. ⁸ Umemupa mamlaka juu ya vitu vyote.» Wakati inaposemwa ya kama Mungu amemupa mtu mamlaka juu ya vitu vyote, maana yake hakuacha hata kitu kimoja. Ingawa hivi, hata sasa hatuoni kwamba amepewa mamlaka juu ya vitu vyote. ⁹ Lakini mambo tunayoona ndiyo haya: Yesu alifanywa kuwa mwenye cheo chini kidogo ya malaika kusudi kwa neema ya Mungu, Yesu akufe kwa ajili ya watu wote. Na sasa kwa njia ya kile kifo kilichomufikia, amepata utukufu na heshima. ¹⁰ Kwa hiyo ilifaa kwamba Mungu aliyeumba vitu vyote na kuvilinda imara, amufanye Yesu kuwa mukamilifu kwa njia ya mateso, kusudi awaleta watoto wengi kuwa washiriki wa utukufu wa Mungu. Kwa maana Yesu ndiye anayewaongoza watu wapate kuokoka. ¹¹ Yeye anawatakasa watu toka katika zambi, na wale wanaotakaswa naye, wote ni watoto wa Baba mmoja. Ni kwa sababu hiyo Yesu hasikii haya ya kuwaita wandugu zake. ¹² Kwa maana anasema: «Ee Mungu, nitatangaza jina lako kwa wandugu zangu, nitakusifu katikati ya mkutano. ¹³ Tena anasema: “Nitamutumainia Mungu.” Na tena anasema: “Mimi ni hapa pamoja na watoto Mungu alionipatia.”» ¹⁴ Basi kwa kuwa hao watoto ni wanadamu, wenye mwili na damu, Yesu vilevile alitwaa ile hali ya mwanadamu. Alifanya hivi kusudi kwa njia ya kufa kwake amwagamize Shetani aliyekuwa na uwezo wa kuleta lufu. ¹⁵ Vilevile aliwafungua wale wote walioishi kama watumwa katika maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa lufu. ¹⁶ Kwa maana hakika hakukuja kuwasaidia wamalaika, lakini alikuja kuwasaidia wazao wa Abrahamu. ¹⁷ Kwa hiyo ilimupasa afanane na wandugu zake katika mambo yote, kusudi apate kuwa Kuhani Mkubwa anayekuwa mwenye huruma na mwaminifu katika kazi yake mbele ya Mungu, na kwa njia hiyo zambi za watu zisamehewe. ¹⁸ Na kwa sababu yeye mwenyewe alijaribiwa na kuteswa, anaweza kuwasaidia wale wanaojaribiwa.

Chapter 3

¹ Kwa sababu hiyo, wandugu zangu, ninyi ambao mumeitwa na Mungu na kuwa watu wake kama vile sisi, mufikiri sana juu ya Yesu, anayekuwa mutume na Kuhani Mkubwa wa imani tunayotangaza. ² Yeye alikuwa mwaminifu mbele ya Mungu aliyemusimika kwa kazi ile, sawa vile Musa alivyokuwa mtumishi mwaminifu katika kazi ya nyumba yote ya Mungu. ³ Mujengaji wa nyumba anaheshimiwa zaidi kuliko nyumba yenyewe. Hivi vilevile Yesu anastahili kupewa heshima kubwa zaidi kuliko Musa. ⁴ Ni kweli kila nyumba inajengwa na mtu, lakini Mungu ndiye aliyejenga vitu vyote. ⁵ Musa alikuwa mtumishi mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu, kusudi ashuhudie maneno ambayo Mungu angesema nyuma. ⁶ Lakini Kristo ni mwaminifu kama Mwana anayesimamia nyumba ya Mungu. Na sisi ndio nyumba ile, kama tukiendelea kuwa na uhodari na kuaminia kupata mambo tunayotumainia. Mapumziko Mungu anayotayarishia watu wake ⁷ Kwa hiyo, kama vile Roho Mtakatifu anavyosema: «Leo ikiwa munasikiliza sauti ya Mungu, ⁸ musifanye mioyo yenu kuwa migumu kama babu zenu walivyofanya wakati walipomuasi Mungu, sawa siku ile walipomupima katika jangwa. ⁹ Kule babu zenu walinipima na kunijaribia, ingawa walikuwa wameona yote niliyotenda kwa muda wa miaka makumi ine. ¹⁰ Kwa sababu ile nilikasirikia kizazi chao, na kusema: Watu hao wanapotoka mioyo siku zote. Nao hawafuati njia zangu. ¹¹ Basi nikaapa kwa kasirani kwamba hawataingia kwenye mapumziko niliyowatayarishia!» ¹² Basi wandugu zangu, muangalie vizuri, kati yenu kusikuwe mtu mmoja mwenye moyo mubaya wa kutokuamini, aliyefikia hata kujitenga mbali na Mungu Mwenye Uzima. ¹³ Lakini muonyane kila siku kwa muda wote ambao lile neno leo linalotajwa lingali linatuelekea kusudi hata mmoja wenu asikuwe mugumu kwa kudanganywa na zambi. ¹⁴ Kwa maana sisi wote tunaishi katika ushirika na Kristo ikiwa tunachunga mpaka mwisho lile tumaini tulilopata kwa mwanzo. ¹⁵ Maandiko Matakatiifu yanasema: «Leo ikiwa munasikiliza sauti ya Mungu, musifanye mioyo yenu kuwa migumu kama babu zenu walivyofanya wakati walipomuasi Mungu.» ¹⁶ Ni watu gani waliosikia maneno ya Mungu na kumwasi? Si wale wote walioongozwa na Musa toka katika inchi ya Misri? ¹⁷ Tena, ni watu gani waliomukasirisha Mungu kwa muda wa miaka makumi ine? Si wale wote waliofanya zambi wakaanguka na kufa katika jangwa? ¹⁸ Tena ni watu gani Mungu aliowaapia kwamba hawataingia kwenye mapumziko aliyowatayarishia? Si wale waliokataa kumutii? ¹⁹ Basi tunaona kwamba hawakuweza kuingia kwenye mapumziko yale kwa sababu ya kutokuamini kwao.

Chapter 4

¹ Basi kwa kuwa tungali na ahadi ya kuingia kwenye mapumziko yale, basi tuogope kusudi katikati yenu kusikuwe hata mtu mmoja atakayekosa kuingia. ² Kwa maana sisi vilevile tumehubiriwa Habari Njema kama vile watu wale. Walisikia habari lakini haikuwafalia kitu, kwa maana wale walioisikia hawakuipokea kwa imani. ³ Lakini sasa sisi tulioamini, tutaingia kwenye mapumziko ambayo Mungu alitaja aliposema: «Halafu nikaapa kwa kasirani kwamba hawataingia hata kidogo kwenye mapumziko niliyowatayarishia! Mungu alisema vile ingawa alikuwa amemaliza kazi zake tangu pale alipoumba dunia. ⁴ Kwa maana imesemwa pahali fulani katika Maandiko Matakatifu juu ya siku ya saba: “Siku ya saba, Mungu akapumzika kwa maana alikuwa amemaliza kazi zake zote.” ⁵ Na tena, katika Maandiko tuliyotaja hapa juu, Mungu anasema: “Hawataingia hata kidogo kwenye mapumziko niliyowatayarishia.” ⁶ Wale waliokuwa wa kwanza kuhubiriwa Habari Njema hawakuingia kwenye mapumziko yale kwa sababu ya kutokuamini kwao. Ingawa vile ingali inawezekana kwa wengine kuingia. ⁷ Kwa sababu hii Mungu anaweka tena siku ingine inayoitwa “Leo”. Naye alisema juu ya siku ile nyuma ya miaka mingi kwa njia ya Daudi, kufuatana na Maandiko haya yaliyokwisha kutajwa mbele: “Leo kama munasikiliza sauti ya Mungu musifanye mioyo yenu kuwa migumu.”» ⁸ Kwa maana kama Yoshua angekuwa amewafikisha watu kwenye mapumziko, Mungu hangesema tena nyuma ya pale juu ya siku ingine. ⁹ Kwa hiyo kungali mapumziko ambayo Mungu anawatayarishia watu wake. ¹⁰ Kwa maana yule anayeingia kwenye mapumziko anayotayarisha, anapumzika kwa kuwa amemaliza kazi zake zote kama vile Mungu alivyopumzika alipomaliza kazi zake. ¹¹ Basi tufanye bidii ya kuingia kwenye mapumziko yale, kusudi hata mtu mmoja asianguke sawa vile wale walioasi katika jangwa. ¹² Kwa maana Neno la Mungu ni lenye uzima, na lina nguvu; ni kali kupita upanga unaokata ngambo mbili. Linapenya hata linatenga moyo na roho na hata viungo na ubongo. Nalo linatambua nia na mawazo ya mtu. ¹³ Hakuna kitu kinachoweza kufichwa mbele ya Mungu, lakini vitu vyote vinafunuliwa na viko wazi mbele ya macho yake, yeye tutakayemutolea hesabu ya maneno yetu. Yesu ni Kuhani Mkubwa zaidi ¹⁴ Basi, kwa kuwa tuko na Kuhani Mkubwa zaidi aliyeingia mbinguni, ndiye Yesu Mwana wa Mungu, tushikamane sana na imani tunayotangaza. ¹⁵ Kwa maana tuko na Kuhani Mkubwa asiyekosa kujua mwenyewe uzaifu wetu. Maana yeye alijaribiwa katika njia zote sawasawa na sisi, lakini hakufanya zambi. ¹⁶ Kwa sababu hii, tujongeele kwa uhodari kiti cha kifalme cha Mungu pahali anapowajalia watu neema kusudi apate kutuhurumia na kutujalia neema ya kutusaidia kwa wakati unaofaa.

Chapter 5

¹ Kila Kuhani Mkubwa aliyechaguliwa kati ya watu amesimikwa kwa kumutumikia Mungu kwa ajili ya watu kusudi atolee matoleo na sadaka kwa ajili ya zambi. ² Kwa kuwa yeye mwenyewe ni muzaifu, anaweza kuwavumilia wale waliopotoka bila kujua. ³ Na kwa sababu yeye mwenyewe ni muzaifu, anapaswa kutolea sadaka, si kwa sababu ya zambi za watu tu, lakini kwa sababu ya zambi zake mwenyewe vilevile. ⁴ Hakuna mtu anayejiipatia heshima hii ya kuwa Kuhani Mkubwa yeye mwenyewe. Lakini anapaswa kuitwa na Mungu, kama vile Haruni alivyoitwa. ⁵ Hivi vilevile, Kristo hakujipatia yeye mwenyewe utukufu wa kuwa Kuhani Mkubwa, lakini ni Mungu ndiye aliyemwambia: «Wewe ni mwana wangu, mimi leo nimekuwa baba yako. ⁶ Vilevile alisema pahali pengine katika Maandiko: “Wewe ni kuhani hata milele kwa mufano wa Melkisedeki.”» ⁷ Wakati Yesu alipoishi katika dunia, aliomba na kusihi kwa malalamiko makubwa pamoja na kutoa machozi kwa Mungu ambaye angeweza kumwokoa toka katika kifo. Mungu alimusikia Yesu kwa sababu yeye alimuheshimu. ⁸ Ijapokuwa alikuwa Mwana wa Mungu, alijifunza kutii kwa njia ya mateso yale aliyopata. ⁹ Na alipokwisha kufanywa kuwa mukamilifu, akawaongoza watu wote wanaomutii wapate kuokolewa kwa milele. ¹⁰ Basi, Mungu alitangaza kwamba yeye ni Kuhani Mkubwa kwa mufano wa Melkisedeki. Hatari ya kuacha imani ¹¹ Tuna maneno mengi ya kusema juu ya jambo hili, lakini ni vigumu kuyaeleza kwenu kwa sababu ninyi mumekuwa na masikio magumu. ¹² Kweli, kwa wakati huu, ninyi mungepaswa sasa kuwa walimu, lakini mungali munahitaji kufundishwa tena mafundisho ya mwanzo ya neno la Mungu. Mumegeuka tena wenye kuhitaji kunywa maziwa, wala si chakula kigumu. ¹³ Kwa maana kila mtu anayeishi kwa kunyonya maziwa tu hawezi kufahamu mafundisho ya haki, maana yeye ni mtoto muchanga. ¹⁴ Lakini chakula kigumu ni kwa ajili ya watu wazima, ndio wale waliozoeza mafikiri yao hata wapate kutambua mema na mabaya.

Chapter 6

¹ Basi kwa sababu hii, tuache mafundisho ya mwanzo juu ya Kristo. ² Tusijenge tena musingi mupya wa mambo haya: kugeuka toka katika matendo yasiyofaa, kumwamini Mungu, namna mbalimbali za ubatizo, kuwawekea watu mikono, ufufuko na hukumu ya milele. ³ Tuendele katika mafundisho makamilifu. Tutatanya hivi, Mungu akitaka. ⁴ Maana watu wanapokwisha kuangaziwa na ukweli wa Mungu na kuonja zawadi ya mbinguni, na kuishi katika ushirika na Roho Mtakatifu, ⁵ wanapokwisha kuonja wema wa Neno la Mungu na nguvu za ulimwengu utakaokuja, ⁶ kisha wakianguka, haiwezekani kuwarudisha hata wapate kugeuka mara ingine toka katika matendo yao mabaya. Kwa sababu wamemutundika wao wenyewe Mwana wa Mungu mara ya pili na kumupatisha haya mbele ya watu. ⁷ Udongo unaonyeshewa na mvua mara kwa mara na kutoa mimea inayofaa kwa walimaji, unabarikiwa na Mungu. ⁸ Lakini kama ukitoa miiba na magugu, udongo ule haufai kitu nao uko karibu ya kulaaniwa na Mungu, tena mwisho wake ni kuteketezwa. ⁹ Lakini wapendwa wangu, ijapokuwa tunasema hivi, hatuna mashaka juu yenu, tukijua kwamba munafuata njia nzuri zaidi, ile ya wokovu wenu. ¹⁰ Kwa maana Mungu ni mwenye haki. Yeye hatasahau kazi yenu na upendo mulioonyesha kwa ajili yake kwa namna mulivyowasaidia watu wake na munavyoendelea kuwasaidia. ¹¹ Lakini tunatamani sana kwamba kila mmoja kati yenu aendelee kuonyesha bidii ile mpaka mwisho, kusudi mambo yale munayotumainia yapate kutimizwa. ¹² Basi musigeuke kuwa wavivu, lakini mufuate mufano wa wale wanaoamini na kuvumilia. Kwa njia hiyo wanapokea yale Mungu aliyoahidi kuwapa. Ahadi ya Mungu ¹³ Wakati Mungu alipomupa Abrahamu ahadi, alifanya vilevile kiapo. Kwa sababu hakuna mtu mwingine mkubwa kuliko yeye kusudi ataje jina lake, akaapa kwa jina lake mwenyewe. ¹⁴ Akasema: «Hakika nitakubariki sana na nitaongeza wazao wako.» ¹⁵ Hivi kisha kungojea kwa uvumilivu, Abrahamu akapokea yale Mungu aliyomwahidi. ¹⁶ Kwa maana watu wanapofanya kiapo, wanaapa kwa jina la mtu anayekuwa mkubwa kuliko wao wenyewe, nao uhakikisho wa kiapo kile unakomesha mabishano yote kati yao. ¹⁷ Naye Mungu, kwa sababu alitaka kuonyesha wazi kwa wale watakaopokea ahadi kwamba yeye hawezi kubadilisha shauri lake hata kidogo, akaihakikisha kwa kiapo. ¹⁸ Basi kuna mambo mawili, ahadi na kiapo, yasiyoweza kubadilika, na kuelekea hayo, Mungu hawezi kusema uongo. Kwa hivi, sisi tuliomukimbilia tunatiwa moyo sana na kushika kwa nguvu tumaini tulilowekewa. ¹⁹ Tumaini hili linasimamisha imara na kulinda mioyo yetu kama vile nanga inavyosimamisha mashua imara. Nalo linapita katika pazia na kuingia katika Pahali Patakatifu Sana. ²⁰ Yesu alitangulia kuingia pahali pale kwa ajili yetu. Amekuwa Kuhani Mkubwa hata milele, kwa mufano wa Melkisedeki.

Chapter 7

¹ Huyu Melkisedeki alikuwa mfalme wa Salemu na kuhani wa Mungu Mkubwa. Abrahamu alipokuwa akirudi toka katika vita nyuma ya kuwashinda wafalme., ² Naye Abrahamu akamupa fungu moja la kumi la vitu vyote alivyoteka. Maana ya jina la Melkisedeki, kwanza ni Mfalme wa haki, tena ni mfalme wa Salemu, ni kusema Mfalme wa amani. ³ Hakuna mambo yaliyoandikwa juu ya baba ya Melkisedeki, wala mama yake, wala majina ya babu zake. Tena, habari za kuzaliwa kwake na za kufa kwake hazijulikani. Anafanana na Mwana wa Mungu. ⁴ Basi muangalie namna mtu huyu alivyokuwa mkubwa, hata babu yetu mkubwa Abrahamu alimupa fungu moja la kumi la vitu vyote alivyoteka katika vita. ⁵ Wazao wa Lawi wanaopewa kazi ya ukuhani wanaamriwa na Sheria kukongoa fungu moja la kumi la mapato toka kwa wandugu zao Waisraeli, ijapokuwa wao vilevile ni wa uzao wa Abrahamu. ⁶ Lakini huyu Melkisedeki asiyekuwa wa uzao wa Lawi, alipokea fungu moja la kumi la vitu toka kwa Abrahamu. Na zaidi ya ile akamubariki Abrahamu, ambaye Mungu alikuwa amemutolea ahadi. ⁷ Lakini bila shaka, yule anayebarikiwa ni mudogo kuliko yule anayebariki. ⁸ Wale makuhani wanaopokea fungu la kumi ni watu wanaokufa; lakini Melkisedeki aliyepokea fungu la kumi anashuhudiwa kwamba anaishi. ⁹ Basi tunaweza kusema hivi: wakati Abrahamu alipotoa fungu la kumi la mali yake, Lawi vilevile alilitoa kupitia yeye. ¹⁰ Kwa maana ingawa Lawi alikuwa hajazaliwa bado, alikuwa yuko ndani ya damu ya babu yake Abrahamu, wakati Melkisedeki alipokutana naye. ¹¹ Ukuhani ndio ulikuwa musingi wa Sheria iliyotolewa kwa Waisraeli. Basi ikiwa ukamilifu ulipatikana kwa njia ya kazi ya ukuhani wa uzao wa Lawi, hakungekuwa tena lazima kutokee kuhani mwingine anayekuwa sawa na Melkisedeki, kwa pahali pa kuhani anayekuwa sawa na Haruni. ¹² Kwa maana wakati ukuhani unapobadilika, Sheria nayo inapaswa kubadilika vilevile. ¹³ Naye Bwana wetu ambaye maneno haya yanamwelekea, alikuwa mtu wa kabila lingine, wala hakuna hata mtu mmoja wa kabila lake aliyefanya kazi ya ukuhani kwenye mazabahu. ¹⁴ Kwa maana inajulikana wazi kwamba Bwana wetu alitoka katika kabila la Yuda, na juu ya kabila lile Musa hakusema hata neno moja linaloelekea ukuhani. Kuhani mwingine anayefanana na Melkisedeki ¹⁵ Tena jambo hili linaloonyesha wazi zaidi maneno haya: kumetokea kuhani mwingine anayefanana na Melkisedeki. ¹⁶ Huyu mwingine hakuwekwa kuwa kuhani kwa amri ya kimtu kufuatana na ukoo wake, lakini kufuatana na uwezo wa uzima usiokuwa na mwisho. ¹⁷ Maana Maandiko Matakatiifu yanashuhudia: «Wewe ni kuhani kwa milele kwa mufano wa Melkisedeki.» ¹⁸ Kwa hiyo, ile amri ya zamani imevunjwa, kwa sababu ilikuwa zaifu nayo haikufaa kitu, ¹⁹ kwa maana Sheria ya Musa haikuleta ukamilifu. Lakini sasa kumeletwa tumaini nzuri zaidi, na kwa njia ya tumaini hili tunaweza kumukaribia Mungu. ²⁰ Zaidi ya hii, mambo yale yalifanyika kufuatana na kiapo cha Mungu. Wale makuhani wengine wa uzao wa Lawi waliwekwa kwa kazi yao pasipo kiapo. ²¹ Lakini Yesu amewekwa kuwa kuhani kwa njia ya kiapo, wakati Mungu alipomwambia: «Bwana ameapa, naye hatageuka: “Wewe ni kuhani kwa milele.”» ²² Kwa sababu ya kiapo hiki, Yesu amekuwa kihakikisho kwetu cha agano linalokuwa zuri zaidi. ²³ Kuna tofauti ingine vilevile: wale makuhani wengine walipaswa kuwa wengi, kwa sababu walikuwa wakikufa hawakuweza kuendelea na kudumu katika kazi yao. ²⁴ Lakini Yesu hawezi kukombolewa kwa kazi yake ya ukuhani, kwa sababu yeye anaishi kwa milele. ²⁵ Ni kwa sababu hii anaweza kuwaokoa kabisa wao wanaokuja kwa Mungu kwa njia yake, kwa maana yeye anaishi siku zote kusudi akuwe mwombezi mbele ya Mungu. ²⁶ Basi Yesu ndiye Kuhani Mkubwa anayefaa kwa ajili yetu. Yeye ni mtakatifu, hana kosa wala alama ya uchafu. Ametengwa mbali na wenye zambi, naye amenyanyuliwa juu sana mbinguni. ²⁷ Yeye hahitaji kutoa sadaka kila siku kama vile Makuhani wengine Wakubwa, kwanza kwa ajili ya zambi zake mwenyewe na kisha kwa ajili ya zambi za watu. Kwa maana amefanya vile mara moja tu wakati alipojitoa mwenyewe kufa. ²⁸ Sheria ya Musa inawaweka watu wenye uzaifu kuwa Makuhani Wakubwa, lakini kufuatana na kiapo kilichokuja nyuma ya Sheria ile, Mwana anayekuwa mukamilifu kwa milele aliwekwa kuwa Kuhani Mkubwa.

Chapter 8

¹ Jambo la lazima sana katika maneno tunayosema sasa ni hili. Tuko na Mkubwa wa namna ile, anayeikaa na mamlaka katika mbingu kwa kuume kwa Mwenyezi Mungu. ² Yeye anafanya kazi ya Kuhani Mkubwa katika Pahali Patakatifu Sana, maana yake katika hema ya kweli iliyosimikwa na Bwana, wala si mtu. ³ Kila Kuhani Mkubwa anawekwa kusudi afanye kazi ya kutoa sadaka na matoleo. Kufuatana na hiyo, ilimupasa Kuhani wetu Mkubwa Kristo akuwe na kitu cha kutoa vilevile. ⁴ Kama Kristo angekuwa katika dunia, asingekuwa kuhani hata kidogo, kwa sababu kuko makuhani wanaotoa sadaka kufuatana na maagizo ya Sheria. ⁵ Kazi wale makuhani wanayofanya ni mufano na kitambulisho kinachoonyesha jinsi mambo kamili yanavyopitika mbinguni. Maneno hayo yanalingana na yale yaliyomutokea Musa. Wakati Musa alipokuwa karibu ya kujenga Hema, Mungu alimwambia: «Ufanye angalisho kusudi upate kutengeneza kila kitu kufuatana na mufano niliokuonyesha kwa mulima.» ⁶ Lakini sasa Yesu amepewa kazi inayokuwa bora zaidi kuliko kazi ya wale makuhani, kwa maana yeye ni mupatanishi wa agano linalokuwa zuri zaidi. Sherti za agano lile zinasimamia juu ya ahadi ya Mungu inayokuwa bora zaidi. ⁷ Kama lile agano la kwanza lingekuwa kamilifu, haingekuwa lazima likombolewe na la pili. ⁸ Lakini Mungu aliwaonya watu wake, akisema: «Katika siku zinazokuja, nitafanya agano jipya na watu wa ufalme wa Israeli na wa Yuda. Ni Bwana anayesema hivyo. ⁹ Agano lile halitakuwa sawa na lile nililofanya na babu zao siku nilipowakamatia kwenye mukono na kuwaondoa toka inchi ya Misri. Kwa sababu hawakushika lile agano, kwa hiyo vilevile sikuwashugulikia. Ni Bwana wetu Mungu anayesema hivyo. ¹⁰ Sasa hili ndilo agano nitakalofanya na watu wa ufalme wa Israeli katika siku zile: nitawawezesha kuchunga sheria zangu ndani ya mafikiri yao, nikiziandika ndani ya mioyo yao. Ni Bwana wetu Mungu anayesema hivyo. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. ¹¹ Hakutakuwa tena atakayefundisha mwanainchi mwenzake, au kumwambia ndugu yake: “Umujue Bwana. Kwa maana watu wote watanijua, tangu mudogo mpaka mkubwa. ¹² Mimi nitawasamehe maovu yao, wala sitakumbuka tena zambi zao.”» ¹³ Mungu alipotangaza hilo agano kuwa jipya, jambo hilo lilisababisha lile la kwanza kuwa la zamani na lenye kuchakaa. Na kitu chochote kikiwa cha zamani na chenye kuchakaa kinafikia wakati wa kutoweka.

Chapter 9

¹ Katika agano la kwanza wanasema juu ya kanuni za ibada na juu ya nafasi ya kuabudia iliyojengwa na watu. ² Kufuatana na ile, kulikuwa Hema iliyosimikwa. Chumba chake cha kwanza kiliitwa Pahali Patakatifu. Ndani ya chumba kile kulikuwa kinara cha kuwekea taa, meza na mikate iliyotolewa kwa Mungu. ³ Na nyuma ya pazia lililotenga kile chumba cha kwanza, kulikuwa chumba kingine kilichoitwa Pahali Patakatifu Sana. ⁴ Ndani ya chumba kile kulikuwa chombo cha kufukizia ubani, kilichotengenezwa na zahabu. Na kulikuwa vilevile Sanduku la Agano lililopakaliwa zahabu pande zote. Ndani ya sanduku lile kulikuwa kopo la zahabu lenye mana, na fimbo ya Haruni iliyoota vichipukizi juu yake. Kulikuwa vilevile vibao vya mawe vyenye Maandiko ya Agano la Mungu. ⁵ Na juu ya lile sanduku kulikuwa sanamu mbili za makerubi zilizoonyesha utukufu wa Mungu. Mabawa yao yalikuwa yakinyoosha juu ya kiti cha rehema. Lakini sasa si wakati wa kueleza mambo hayo yote moja kwa moja. ⁶ Ni hivi ndivyo walivyopanga vitu vile vyote. Halafu makuhani waliingia kila siku katika kile chumba cha kwanza kwa kufanya kazi za ibada. ⁷ Lakini ni Kuhani Mkubwa peke yake ndiye aliyeingia katika kile chumba cha pili mara moja tu kila mwaka. Naye alipaswa kupeleka mule damu ya nyama anayotoa sadaka kwa ajili ya zambi zake mwenyewe na kwa ajili ya zambi watu walizofanya kwa kutokujua. ⁸ Hivi Roho Mtakatifu alikuwa akionyesha kwamba njia ya kuingia katika Pahali Patakatifu Sana ilikuwa bado kufunguliwa kwa wakati wote ile Hema ya kwanza ilipokuwa ingali ikisimikwa. ⁹ Huo ni mufano wa wakati wa sasa unaonyesha kwamba matoleo na sadaka zinazotolewa kwa Mungu haziwezi kumufanya yule anayeabudu kuwa na moyo mukamilifu. ¹⁰ Hizo ni kanuni za kimtu zinazoelekea vyakula na vinywaji pamoja na desturi mbalimbali za utakaso za kidini. Nazo zinaamuriwa kushikwa mpaka upate kutimia wakati wa kutengeneza vitu vyote upya. ¹¹ Lakini Kristo alikuja kuwa Kuhani Mkubwa anayeshugulika na mambo mema ambayo sasa yamekwisha kutokea. Yeye alipita katika hema inayokuwa bora zaidi na kamilifu. Hema hii haikutengenezwa na watu, maana yake si ya dunia hii. ¹² Aliingia mara moja tu katika Pahali Patakatifu Sana. Naye hakupeleka mule sadaka ya damu ya mbuzi na ya ngombe, lakini alipeleka damu yake mwenyewe. Na kwa njia ile akatukomboza kwa milele. ¹³ Watu waliohesabiwa kuwa wachafu kufuatana na desturi, walitakaswa uchafu wao wa kimwili kwa njia ya kunyunyizwa damu ya mbuzi na ya ngombe pamoja na majivu ya ngombe aliyeteketewa kwa moto. ¹⁴ Ikiwa ni hivi, damu ya Kristo haitakuwa na uwezo zaidi wa kututakasa? Kwa maana kwa njia ya Roho anayeishi kwa milele, Kristo alijitoka mwenyewe kwa Mungu kuwa sadaka kamilifu. Nayo damu yake ikazitakasa zamiri zetu toka katika matendo yasiyofaa, kusudi tupate kumutumikia Mungu Mwenye Uzima. ¹⁵ Kwa sababu hii, Kristo ni mupatanishi wa agano jipya. Kwa njia ya kufa kwake aliwakomboa watu toka katika makosa waliyofanya chini ya uongozi wa agano la kwanza, kusudi wale walioalikwa na Mungu wapate kupokea urizi wa milele aliowaahidia. ¹⁶ Katika mambo yenye kuelekea agano la urizi, ni lazima kuhakikisha kwamba yule aliyelifanya amekwisha kufa. ¹⁷ Agano kama hili linatimizwa nyuma ya kifo cha yule aliyelifanya, lakini si wakati angali mzima. ¹⁸ Kwa sababu hii, hata lile agano la kwanza halikuwekwa pasipo kumwangika kwa damu. ¹⁹ Kwa maana, kwanza Musa aliwatangazia watu wote amri zote za Sheria. Kisha akatwaa damu ya ngombe na mbuzi pamoja na maji, naye akavinyunyiza juu ya kitabu cha Sheria na juu ya watu wote akitumia manyoya mekundu na vitawi vya muti wa hisopo. ²⁰ Naye akasema: «Hii ndiyo damu inayohakikisha agano lile Mungu analowaamuru kutii.» ²¹ Musa akanyunyiza vilevile damu juu ya Hema na juu ya vyombo vyote vya ibada. ²² Na kufuatana na Sheria, karibu vitu vyote vinatakaswa kwa damu, nazo zambi haziwezi kusamehewa pasipo kumwangwa kwa damu. Kristo ni sadaka inayoondoa zambi. ²³ Basi ilikuwa lazima vitu vile vinavyoonyesha mufano wa mambo yanayopitika katika mbingu vitakaswe kwa njia ile. Lakini mambo kamili ya mbinguni yanahitaji kutakaswa kwa sadaka inayokuwa bora zaidi. ²⁴ Kwa maana Kristo hakuingia katika Pahali Patakatifu palipojengwa na watu, panapokuwa tu mufano wa Pahali Patakatifu kamili, lakini aliingia katika mbingu yenyewe, pahali anaposimama sasa mbele ya Mungu kwa kututetea. ²⁵ Kuhani Mkubwa wa Wayuda anaingia katika Pahali Patakatifu Sana kila mwaka, akibeba damu ya nyama. Lakini Kristo hakuingia humo kusudi ajitoe mwenyewe sadaka mara nyingi. ²⁶ Ingekuwa hivi, ingemupasa ateswe mara nyingi tangu kuumbwa kwa dunia. Lakini sasa, wakati ukikaribia kwa mwisho, yeye alitokea mara moja tu kusudi awasamehe watu zambi kwa njia ya kujitoka mwenyewe sadaka. ²⁷ Kila mtu anapaswa kufa mara moja tu, na nyuma ya kufa, anahukumiwa na Mungu. ²⁸ Hivi vilevile Kristo naye alijitoka kufa mara moja kusudi aondoe zambi za watu wengi. Naye atarudi tena, si kwa ajili ya kuondoa zambi, lakini kwa kuwaokoa wale wanaomungoja.

Chapter 10

¹ Sheria ya Kiyuda ni mufano wa mema yatakayotokea, lakini si kitambulisho kinachoonyesha mambo yale kamili. Kwa sababu hii Sheria haiwezi hata mara moja, kwa njia ya sadaka zinazotolewa mara nyingi kila mwaka, kuwafanya wakamilifu wale wanaomwendea Mungu. ² Wale wanaomwabudu Mungu kwa njia ile wangetakaswa kabisa kwa mara moja tu, nayo zamiri yao isingewahukumu tena hata kidogo juu ya zambi, basi sadaka zile hazingeacha kutolewa. ³ Lakini kwa njia ya sadaka zile, watu wanakumbushwa zambi zao kila mwaka, ⁴ kwa sababu damu ya ngombe na ya mbuzi haiwezi kuondoa zambi. ⁵ Kwa sababu hii, wakati Kristo alipokuja katika dunia alisema: «Wewe haukutaka sadaka wala matoleo. Lakini umeniumbia mwili. ⁶ Haukupendezwa na sadaka za kuteketezwa kwa moto wala sadaka za kusamehewa zambi. ⁷ Halafu nikasema: “Niko hapa, ee Mungu, nimekuja kufanya mapenzi yako, kama ilivyoandikwa juu yangu katika kitabu cha Sheria.” ⁸ Kwanza Kristo alisema: “Haukutaka wala haukupendezwa na sadaka na matoleo, wala sadaka za kuteketezwa kwa moto wala sadaka za kusamehewa zambi.” (Alisema vile ingawa sadaka hizo zote zilitolewa kufuatana na maagizo ya Sheria.) ⁹ Kisha akasema: “Mimi niko hapa, ee Mungu, nimekuja kufanya mapenzi yako.” Kwa hiyo Mungu ameondoa hizo sadaka zote za kwanza na kuzikomboa na Kristo mwenyewe kama sadaka. ¹⁰ Na kwa sababu Yesu Kristo alifanya mapenzi ya Mungu, sisi tumetakaswa zambi kwa njia ya mwili wake alioutoa sadaka kwa mara moja tu. ¹¹ Kila kuhani anasimama mbele ya Mungu kila siku kwa kufanya ibada na kutoa sadaka za namna moja mara nyingi zisizoweza hata kidogo kuondoa zambi. ¹² Lakini Kristo yeye alitoa sadaka moja tu inayofaa kwa milele kwa ajili ya usamehe wa zambi. Na kisha akaikaa na mamlaka kwa kuume kwa Mungu. ¹³ Na kule anangoja sasa mpaka waadui zake wote watiwe chini ya miguu yake. ¹⁴ Kwa maana kwa njia ya sadaka moja aliyotoa, amewafanya wale aliowatakaswa kuwa wakamilifu hata milele. ¹⁵ Naye Roho Mtakatifu anatushuhudia mambo hayo vilevile. Kwanza anasema maneno haya: ¹⁶ “Hili ndilo agano nitakalofanya nao nyuma ya siku zile. Ni Bwana wetu Mungu anayesema hivyo. Nitawawezesha kuchunga sheria zangu ndani ya mafikiri, nikiziandika ndani ya mioyo yao.” ¹⁷ Naye anaongeza kusema: «Nami sitakumbuka tena zambi wala maovu yao.» ¹⁸ Basi wakati zambi zinaposamehewa, hakuna tena hitaji la kutoa sadaka kwa ajili ya usamehe wa zambi. Tumukaribie Mungu ¹⁹ Basi wandugu, tuko na uhodari wa kuingia katika Pahali Patakatifu kwa njia ya damu ya Yesu. ²⁰ Yeye ametufungulia njia mupya ya uzima, inayopitia katika pazia, maana yake mwili wake mwenyewe. ²¹ Sisi tuko na Kuhani Mkubwa anayesimamia nyumba yote ya Mungu. ²² Basi tumwendee Mungu kwa moyo wa uaminifu, kwa imani kamilifu, kwa moyo uliosafishwa toka zamiri mbaya na mwili uliosafishwa na maji safi. ²³ Tuendeleo kuchunga lile tumaini tuliloshuhudia bila kuchoka, kwa maana Mungu aliyetupatia ahadi ni mwaminifu. ²⁴ Tena tushugulikiane kusudi tupate kuvutana sisi kwa sisi kuwa na upendo na kufanya mema. ²⁵ Tusiache kukusanyika pamoja, kama vile wamoja wanavyozoea kufanya. Lakini tuonyane, na zaidi sana kufuatana na vile munavyoona kwamba Siku ya Bwana inakaribia. ²⁶ Kwa maana tukifanya zambi kwa makusudi tukisha kutambua waziwazi ukweli, hakuna tena sadaka ingine inayoweza kutolewa kwa ajili ya usamehe wa zambi zetu. ²⁷ Lakini inayobaki tu ni kungojea kwa woga hukumu na moto mukali wa Mungu utakaowateketeza waasi. ²⁸ Mtu yeyote aliyevunja Sheria ya Musa, aliuawa bila huruma kisha ushuhuda wa watu wawili au watatu. ²⁹ Basi munazania itakuwa namna gani? Hataazibiwa vikali zaidi yule anayemuzarau Mwana wa Mungu na kuihesabu kuwa bure damu ya agano la Mungu iliyomutakasa na kumutukana Roho wa neema? ³⁰ Kwa maana tunamujua yule aliyesema: «Ni kazi yangu kulipiza kisasi. Ni mimi nitakayelipiza. Naye alisema tena: “Bwana atawahukumu watu wake.”» ³¹ Kuanguka katika mikono ya Mungu Mwenye Uzima ni jambo la kuogopa sana! ³² Mukumbuke mambo yaliyowatokea katika siku zilizopita. Ninyi mulipokwisha kuangaziwa na Mungu, mulipita katika mateso mengi lakini mulivumilia. ³³ Kwa ngambo moja mulitukanwa na kuteswa waziwazi mbele ya watu. Na kwa ngambo ingine mulishirikiana na wale waliotendewa vibaya. ³⁴ Muliwahurumia wale waliokuwa katika kifungo, nanyi mulikubali kwa furaha kunyanganywa mali zenu, kwa sababu mulijua kwamba muko na mali inayokuwa bora zaidi na yenye kudumu. ³⁵ Basi musikate tumaini, kwa maana litawaletea zawadi kubwa. ³⁶ Munapaswa kuvumilia, kusudi mutimize mapenzi ya Mungu, na kuweza hivi kupewa kile mulichoahidiwa. ³⁷ Kwa maana, kama vile Maandiko haya Matakatifu yanavyosema: «Kunabaki wakati kidogo sana, yule anayepaswa kuja, afike wala hatakawia. ³⁸ Mwenye haki mbele yangu ataishi kwa njia ya imani. Lakini kama akirudi nyuma, sitapendezwa naye.» ³⁹ Lakini sisi si watu wenye kurudi nyuma na kupotea, lakini sisi ni watu wenye imani na wenye kuokoka.

Chapter 11

³¹ Kuwa na imani ni kuwa na uhakika juu ya mambo tunayotumainia, ni kusadiki kabisa mambo tusiyoyaona. ² Ni kwa sababu ya imani yao babu zetu wameshuhudiwa vizuri na Mungu. ³ Kwa njia ya imani tunafahamu kwamba ulimwengu uliumbwa kwa amri ya Mungu, hata vitu vinavyoonekana, viliumbwa kutoka vile visivyoonekana. ⁴ Kwa njia ya imani, Abeli alimutolea Mungu sadaka nzuri zaidi kuliko ile ya Kaina. Kwa ajili ya imani yake alihihesabiwa na Mungu kuwa mwenye haki, kwa maana Mungu alishuhudia sadaka zake. Na kwa imani ile, ingawa Abeli amekwisha kufa, angali anasema. ⁵ Kwa njia ya imani, Enoki alibebwa na Mungu toka katika dunia pasipo kufa. Naye hakuonekana tena, kwa sababu Mungu alimubeba mbinguni. Maana Maandiko Matakatifu yanasema kwamba mbele ya kubebwa kwake, Enoki alishuhudiwa kwamba alimupendeza Mungu. ⁶ Basi pasipo imani, hakuna mtu anayeweza kumupendeza Mungu. Kwa maana mtu anayetaka kumwendea Mungu sherti aamini kwamba Mungu yuko, na kwamba anawapa zawadi wale wanaomutafuta. ⁷ Kwa njia ya imani, Noa alionywa na Mungu juu ya mambo yatakayotokea, yale aliyokuwa hajayaona bado. Yeye alimutii Mungu na kujenga chombo kwa kujiokoa yeye mwenyewe pamoja na jamaa yake. Kutokana na hayo yote akahukumu dunia na kupokea haki inayopatikana kwa njia ya imani. ⁸ Kwa njia ya imani, Abrahamu alitii wakati Mungu alipomwita na kwenda katika inchi ile Mungu aliyoahidi kumupatia kuwa urizi wake. Akaacha inchi yake pasipo kujua pahali anapokwenda. ⁹ Kwa njia ya imani, aliishi kama vile mugeni katika inchi ile Mungu aliyomwahidi. Yeye alikuwa akiishi katika hema kama vile Isaka na Yakobo walivyoishi. Wao vilevile walishiriki pamoja naye ahadi ile ile ya Mungu. ¹⁰ Kwa maana Abrahamu alitazamia kuona mji wenye musingi wa nguvu, mji ambao Mungu mwenyewe ndiye fundi aliyeuchapa na kuujenga. ¹¹ Kwa njia ya imani, Sara mwenyewe vilevile, ijapokuwa alikuwa muzee sana, alijaliwa uwezo wa kupata mimba kwa sababu aliamini kwamba Mungu atatimiza ahadi yake. ¹² Kwa sababu hiyo, kwa njia ya mtu mmoja aliyekuwa akingojea kufa, kukazaliwa wazao wengi sana kama nyota na kama muchanga unaokuwa kandokando ya bahari. ¹³ Watu hawa wote walikufa katika imani pasipo kupokea mambo Mungu aliyoahidi. Lakini waliyaona kwa mbali na kuyafurahia, wakikubali kwamba walikuwa wageni na wasafiri katika dunia. ¹⁴ Maana watu wanaosema maneno kama haya wanaonyesha wazi kwamba wanatafuta inchi yao wenyewe. ¹⁵ Kama wangekumbuka inchi yao walioiacha zamani, wangepewa kupata namna ya kurudia kule. ¹⁶ Lakini kwa hakika walitamani sana inchi inayokuwa bora zaidi, ndiyo inchi ya mbinguni. Kwa sababu hii Mungu hasikii haya kuitwa Mungu wao, maana amewatayarishia mji. ¹⁷ Kwa njia ya imani, Abrahamu alimutoa Isaka kama vile sadaka wakati Mungu alipopima imani yake. Abrahamu alikubali kumutoa mwana wake wa pekee, ingawa ni yeye ndiye aliyekuwa amepewa ahadi na Mungu. ¹⁸ Mungu alikuwa amemwambia: «Ni kwa njia ya Isaka utapata wazao watakaotwa wako.» ¹⁹ Abrahamu aliamini kwamba Mungu anaweza kumufufua Isaka na hivi akarudishiwa tena Isaka kama vile mwenye kufufuka. ²⁰ Kwa njia ya imani, Isaka aliwabariki Yakobo na Esau kuelekea mambo ya siku zitakazokuja. ²¹ Kwa njia ya imani, Yakobo alipokuwa karibu kufa, alibariki kila mmoja wa wana wa Yosefu; akainama kwa kumwabudu Mungu akiagemea fimbo yake. ²² Kwa njia ya imani, Yosefu alipokuwa karibu kufa, alisema juu ya habari za wakati Waisraeli watakapotoka katika inchi ya Misri, na kuwaagiza juu ya mifupa yake. ²³ Kwa njia ya imani wazazi wa Musa walimuficha kwa muda wa miezi mitatu nyuma ya kuzaliwa kwake. Kwa sababu waliona kwamba alikuwa mtoto mwenye sura nzuri, wala hawakuogopa amri ya mfalme. ²⁴ Kwa njia ya imani, Musa alipokuwa mtu mzima, alikataa kuitwa mwana wa binti wa mfalme wa Misri. ²⁵ Alifikiri kwamba ni afazali kuteswa pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika zambi kwa muda mufupi. ²⁶ Aliona kwamba kupatishwa haya kwa ajili ya Kristo kuna faida kubwa zaidi kuliko kupata utajiri wote wa inchi ya Misri, maana alikuwa anatazamia kupokea zawadi yake. ²⁷ Kwa njia ya imani, Musa alitoka katika inchi ya Misri bila kuogopa kasirani ya mfalme. Na kama vile mtu mwenye kumwona Mungu asiyeonekana, yeye hakurudi nyuma. ²⁸ Kwa njia ya imani, alianzisha sikukuu ya Pasaka, na kuamuru damu inyunyizwe, kusudi malaika mwangamizaji asiwaue wazaliwa wa kwanza wanaume wa Waisraeli. ²⁹ Kwa njia ya imani, Waisraeli walivuka bahari Nyekundu kama vile ingekuwa katika inchi kavu. Lakini wakati Wamisri walipojaribu kufanya vile, walizama na kufa ndani ya maji. ³⁰ Kwa njia ya imani, ukuta uliozunguka mji Yeriko ulianguka wakati Waisraeli walipokwisha kuuzunguka kwa muda wa siku saba. ³¹ Kwa njia ya imani, Rahaba, yule kahaba, hakuangamia pamoja na wale waliomuasi Mungu, kwa sababu aliwakaribisha wapelelezi kwa amani. ³² Basi niseme nini tena? Maana wakati hauniruhusu kueleza habari juu ya Gideoni, Baraka, Samsoni, Yefuta, Daudi, Samweli na manabii. ³³ Kwa njia ya imani hawa walishinda inchi za wafalme, walitenda mambo ya haki na kupata yale Mungu aliyowaahidi. Walifunga vinywa vya simba, ³⁴ walizimisha moto mukali, waliponyoka kuuawa kwa upanga. Walikuwa wazaifu, lakini wakupata nguvu; walikuwa shujaa katika vita na kushinda majeshi ya kigeni. ³⁵ Kwa njia ya imani, wanawake wamoja walifufuliwa na kurudishiwa wale waliofiwa nao. Wengine waliteswa mpaka

kufa, nao wakikataa kuachiliwa kusudi wapate ufufuko unaokuwa bora zaidi. ³⁶ Wengine walichekelewa na kupigwa fimbo, na wengine walifungwa minyororo na kutupwa katika kifungo. ³⁷ Wengine waliuawa kwa kutupiwa mawe, wengine walikatwa vipandevipande kwa misumeno, au kuuawa kwa upanga. Walitangatanga wakivaa ngozi za kondoo au za mbuzi, wakiishi katika umaskini, wakiteswa na kutendewa vibaya. ³⁸ Dunia haikustahili kuwa na watu kama hawa! Walitangatanga katika jangwa na katika milima, wakiishi katika mapango na mashimo ndani ya udongo. ³⁹ Watu hawa wote walishuhudiwa vizuri na Mungu kwamba wamemupendeza kwa njia ya imani yao. Lakini hawakupokea mambo yale Mungu aliyowaahidia, ⁴⁰ kwa maana Mungu alikuwa ametayarisha mambo mazuri zaidi kwa ajili yetu kusudi wao wenyewe wasipate kukamilishwa bila sisi vilevile.

Chapter 12

¹ Nasi vilevile tunazungukwa na kundi kubwa kama lile la wale walioshuhudia imani yao. Basi tutupilie mbali vitu vyote vinavyotusonga, nazo zambi zinazotufunga upesi na tukimbie kwa juhudi sana katika mashindano tunayowekewa. ² Tukaze macho yetu kuelekea Yesu mwenye kuanzisha na kukamilisha imani yetu. Kwa sababu alijua furaha atakayopata nyuma, alivumilia kufa juu ya musalaba pasipo kuona haya, na sasa anaikaa na mamlaka kwa kuume kwa Mungu kwenye kiti cha kifalme cha Mungu. ³ Kwa hiyo mumukumbuke yule aliyevumilia kutendewa na wenye zambi kwa chuki kubwa, kusudi musipate kuchoka wala kuregea. ⁴ Kwa maana katika vita munayofanya kwa kushinda zambi, hamujapigana bado mpaka kufa. ⁵ Na zaidi ya hii, mumesahau maonyo haya Mungu anayotoa kwenu kama wana wake? Mwana wangu, usizarau azabu ya Bwana wala usiregee wakati anapokukaripia. ⁶ Kwa maana, Bwana anamwazibu yule anayemupenda, yeye anamupiga kila mtu anayemukubali kuwa mtu wake. ⁷ Muvumilie maadibisho; kwa maana Mungu anawatendea ninyi kama wana wake. Tena, ni mwana gani asiyeazibiwa na baba yake? ⁸ Ikiwa hamuadibishwi na Mungu sawa vile watoto wake wote wanavyoadibishwa, basi ninyi si wana wa kweli wa Mungu, ninyi ni wana haramu. ⁹ Na ikiwa wababa zetu wa kimwili walituadibisha, nasi tuliwaheshimu, jambo hilo halionyeshi zaidi kwamba tunapaswa kumuheshimu Baba yetu wa kiroho na kupata kuishi? ¹⁰ Wababa zetu wa kimwili walituadibisha kwa siku chache kufuatana na vile walivyoona kuwa vema. Lakini Mungu anatuadibisha kwa mafaa yetu kusudi tupate kushirikiana naye katika utakatifu wake. ¹¹ Maadibisho yoyote wakati yanapotolewa yanaonekana kama ni tendo la huzuni wala si la furaha. Lakini kwa mwisho yanawaletea wale waliofundishwa nayo, maisha ya amani na ya haki. ¹² Basi muitie tena nguvu mikono yenu inayopooza, nayo magoti yenu yanayoregea. ¹³ Mujitengenezee njia zenye kunyooka, kusudi mwenye ulema wa miguu asiteguke, lakini apate kupona. ¹⁴ Mujikaze kwa kuishi katika amani na watu wote na kuishi katika utakatifu, kwa sababu hakuna mtu asiyeishi katika hali hiyo atakayemwona Bwana. ¹⁵ Muangalie vizuri, kusudi hata mtu mmoja asijikoseshe mwenyewe kupata neema ya Mungu, wala asikuwe sawa shina la mumea unaotoa matunda machungu na kuleta fujo kati yenu na kuambukiza watu wengi. ¹⁶ Vilevile muangalie vizuri, kusudi hata mtu mmoja asikuwe mwasherati au mwenye kukufuru Mungu kama vile Esau aliyeeuzisha haki yake ya muzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kidogo tu. ¹⁷ Kama munavyojua, nyuma ya pale alikataliwa wakati alipotaka kupokea baraka toka kwa baba yake. Yeye hakukuwa tena na namna ya kugeuza tendo lake ijapokuwa alitafuta baraka ile kwa machozi. ¹⁸ Ninyi hamujafikia kwenye kitu kinachoweza kuguswa kama vile Waisraeli walivyofikia kwenye mulima Sinai. Mulima ule uliwaka moto, ulifunikwa na giza nzito, nao ulikuwa na uvumi wa zoruba juu yake. ¹⁹ Vilevile juu yake kulisikilika mulio wa baragumu na ngurumo ya sauti. Nao Waisraeli waliposikia sauti ile wakasihi wasiambiwe tena neno, ²⁰ kwa sababu hawakuweza kuvumilia agizo walilotolewa: «Hata nyama akigusa mulima anapaswa kuuawa kwa kutupiwa mawe. ²¹ Na mambo yale yaliyoonekana yalikuwa ya kuogopesha sana, hata Musa akasema: «Ninaogopa na kutetemeka!» ²² Lakini ninyi mumefikia kwenye mulima Sayuni na kwenye mji wa Mungu Mwenye Uzima, ndio mji Yerusalema wa mbinguni, kunakokuwa maelfu na maelfu ya wamalaika. ²³ Lakini ninyi mumefikia kwenye mkutano wa furaha wa wazaliwa wa kwanza wa Mungu walioandikwa majina zao katika mbingu. Mumefikia vilevile karibu na Mungu, anayekuwa mwamuzi wa watu wote na kwenye nafsi kunapokuwa roho za watu wenye haki waliofanywa kuwa wakamilifu. ²⁴ Mumefikia karibu na Yesu anayekuwa mupatanishi wa agano jipya, na kwenye damu yake iliyomwangwa inayosema nasi maneno mema zaidi kuliko damu ya Abeli. ²⁵ Basi muangalie vizuri kusudi musikatae kumusikiliza yule anayesema nanyi. Wale waliokataa kusikiliza yule aliyewaonya hapa katika dunia hawakuponyoka azabu ya Mungu. Si jambo hilo linaonyesha wazi kwamba sisi hatutaweza kuponyoka kama tunamugeuzia mugongo yule anayetutolea maonyo kutoka mbinguni? ²⁶ Katika wakati ule sauti yake ilitetemeshwa dunia, lakini sasa ametuahidi hivi: «Nitatemeshwa dunia mara moja tena, wala si dunia tu, lakini mbingu vilevile.» ²⁷ Neno hili mara moja tena linaonyesha kwamba vitu vilivyoumbwa vitatikiswa na kutoweka, kusudi vile visivyoweza kutikiswa vipate kudumu. ²⁸ Basi kwa kuwa tunakubaliwa kuwa washiriki wa ufalme usioweza kutikiswa, tukuwe watu wenye shukrani. Tuonyeshe shukrani ile kwa kumwabudu Mungu kwa njia inayomupendeza kwa heshima na woga, ²⁹ kwa maana Mungu wetu ni kama moto wenye kuteketeza.

Chapter 13

¹ Muendeleee kuishi katika upendo wa kindugu. ² Musisahau kuwakaribisha wageni, maana kwa kufanya hivi wamoja wamewakaribisha wamalaika pasipo kujua. ³ Muwakumbuke wale wanaofungwa, mukijisikia sawa vile wenye kufungwa pamoja nao. Vilevile muwakumbuke wale wanaoteswa, mukijisikia sawa vile wenye kuteswa kama mwili mmoja. ⁴ Ndoa inapaswa kuheshimiwa na watu wote, mume na muke wake wanapaswa kujikinga na uchafu, kwa sababu Mungu atawahukumu wazinz na waasherati. ⁵ Musijiachilie kutawaliwa na tamaa ya mali katika maisha yenu, lakini mutoshewe na vitu munavyokuwa navyo, kwa maana Mungu mwenyewe amesema: «Sitakusahau wala kukuachilia. ⁶ Kwa sababu hii tunaweza kusema kwa uhodari: “Bwana ndiye musaidizi wangu; sitaogopa kitu. Mwanadamu ataweza kunifanya nini?”» ⁷ Muwakumbuke waongozi wenu waliowatangazia neno la Mungu. Muangalie vizuri namna walivyoishi na kufa. Mufuate imani yao. ⁸ Yesu Kristo ni yule yule, jana, leo na hata milele. ⁹ Musidanganywe na mafundisho mengine ya kigeni ya kila namna. Kwa maana mioyo yetu inapaswa kutiwa nguvu kwa njia ya neema ya Mungu, wala si kwa njia ya kushika kanuni zinazoagizwa juu ya vyakula. Kanuni hizo haziwafalii kitu wale wanaozishika. ¹⁰ Sisi tuko na mazabahu yetu, nao makuhani Wayuda wanaotumika katika Pahali Patakatifu hawana ruhusa ya kula sehemu ya vitu vinavyotolewa sadaka juu ya mazabahu ile. ¹¹ Kuhani Mkubwa anapeleka damu ya nyama ndani ya Pahali Patakatifu Sana kwa ajili ya kuitoa kuwa sadaka ya kusamehewa zambi lakini viungo vyote vya nyama wale vinateketezwa kwa moto mbali na kambi. ¹² Kwa sababu hii Yesu vilevile aliua mbali na mji kusudi awatakase watu wake kwa njia ya damu yake mwenyewe. ¹³ Basi tumwendee mbali na kambi, tukikubali kuzarauliwa kama vile yeye alivyozarauliwa. ¹⁴ Kwa maana hapa katika dunia hatuna mji unaodumu, lakini tunatazamia mji ule unaokuja. ¹⁵ 1 Basi kwa njia ya Yesu, tumutolee Mungu sadaka za kumusifu siku zote, maana yake kutangaza kwamba tunaaminia jina lake. ¹⁶ Tena, musisahau kutenda mema na kusaidiana, maana sadaka za namna hii zinamupendeza Mungu. ¹⁷ Mutii waongozi wenu na kushika maagizo yao. Kwa maana wao wanashugulika kila mara kwa ajili ya roho zenu, na wao wanapaswa kutoa habari ya kazi yao mbele ya Mungu. Kwa kufanya vile mutawaruhusu kufanya kazi yao kwa furaha wala si kwa huzuni, kwa maana haitawafalia kitu kama wakitumika katika huzuni. ¹⁸ Muzidi kutuombea. Tuna uhakika kwamba tuko na zamiri safi, kwa maana tunataka kuwa na mwenendo mwema katika mambo yote. ¹⁹ Ninawasihi sana kuomba Mungu, kusudi nipate kurudishwa kwenu upesi. ²⁰ Mungu wa amani, aliyemufufua Bwana wetu Yesu ambaye ni Mchungaji mkubwa wa kondoo kwa njia ya kumwanga damu yake inayohakikisha agano la milele, ²¹ awakamilishe katika kila tendo jema kusudi mupate kutimiza mapenzi yake; yeye atimize ndani yetu yale yanayomupendeza, kwa njia ya Yesu Kristo. Yesu atukuzwe milele na milele. Amina. ²² Wandugu, ninawasihi kupokea kwa uvumilivu haya maonyo ninayowatolea kwa maana nimewaandikia kwa kifupi. ²³ Ninapenda kuwajulisha kwamba ndugu yetu Timoteo amekwisha kufunguliwa. Kama akikuja upesi, nitafika kuwaona pamoja naye. ²⁴ Muwasalimie waongozi wenu wote na watu wote wa Mungu. Wandugu wa Italia wanawasalimia. ²⁵ Tunawatakia ninyi wote neema ya Mungu.

Book: James

James

Chapter 1

¹ Yakobo mutumishi wa Mungu na bwa Yesu kwa makabila kumi na mbili wenye katika mu ta awanyiko: amujambu. ² Muwa kubali wote kama msingi wa furaha, wandugu, wakati munapita kuvipimo mbali mbali. ³ Mukijua kwamba mutihani wa imani yenu inatowa nguvu. ⁴ Uhudari umeleta mzao, kwa gisi muwe wenye ku endelea na ji eneza, na gisi musikose cho cho te. ⁵ Mu moja kati yenu aki wa na lazima ya hekima, aombe kwa Mungu, mwenye kumupa yoyote kwa uzuri bila kosa kwa wote wenye kuomba, na ata mupatia. ⁶ Lakini hombe kwa imani, asi hofu kitu kwani yeyote ahofia yuko kama mabimbi ndani ya bahaki kuu yenye inatembazwa na pepo yenyi kuvukika ngambo zote. ⁷ Kwa ni mtu huyo na wezi kuwazia kupatakitu kwa bwana. ⁸ Mutu kama nuyu iko asio ku ji uzuru, ha kamilike ku ma nfia yake yote. ⁹ Kwa ndugu maskini aji sifu na gisi ya muinoko wake. ¹⁰ Lakini mtafiri na namna yake ya yakushuka, kwani ataoita kama vile tunda ya pori ndnai ya majani. ¹¹ Kwani jua ikitoka na vukutu kali na ikikaukasha majani. uwa li ka anguka na uzuri wake uka haribika. namna moja kwa mtafiri ata konda safarini. ¹² Heri mutu mwenye ku vumulia majaribu. kwani kalisha kushinda majaribu, atapokea taji la maisha, yenyi ilihadiwa lwa wale wenye kupenda Mungu. ¹³ Ye yote asiseme wakati anapo jaribuwa: «Nimejaribi wa na Mungu.» Kwa sababu Mungu hawezi kujaribiwa kwa ubaya, wala hajaribu mutu. ¹⁴ Lakini kula mutu kajaribiwa na vitendo viake vibaya, njo inamuba na ku mugeuza akili. Kisha, wakati unaunda wazo mbaya, inazaa zambi. ¹⁵ Na kwisha zambi kukomaa anazaa kifo. ¹⁶ Musidanginyike, wandu wa penzi. ¹⁷ Zawa yote nzuri na yenye kuka mili ka juu. Imeshuka kwa Baba wa nuru, na kwake haku na mubadiko ao kiziwizi chakinyume. ¹⁸ Mungu alichangua kutu zaa kwa no la kweli, kwa ajili tuwe kama vile ma zao ya kwanza kati ya vitu yote aliye umba. ¹⁹ Mume jua haya, wandugu wapenzi : kwa kila mutu awe mwepesi kwa kisikia, na mzito kwa kusema, na hasirike kwa wepesi. ²⁰ Kwa kisirani kia mwana adam, haionyeshe hukumu ya Mungu. ²¹ Sasa muhache mambo yote ya uchafu na ya wingi wa ubaya. Kwa kujishusha, pokeeni neno lenyi nguvu, na yenyi ya weza kuponyesha nafsi zenu ²² Muwe wenye kutumikisha neno, sio weye kusikiatu. Mukidanganya wenye. ²³ Kama uko mutu mwenye kusikia neno bure lakini si mutumishi. iko kama mutu kajia angalia bure ku kio. ²⁴ ikijiangalia peke yake na kwisha akiyenda na akisahabu pale pale gisi alijifana. ²⁵ Lakini mutu akiangalia saana ndani ya amri nzuri na yenyi kuokowa, na zidi kuwa musikaji bure na akisahabu, mutu huyu ata narikiwa kwa yote ata kaye tenda. ²⁶ Mutu aki zani wakioni lakini hachu nguze masemi yake, akidanganya moyo wake, na dini yake naina manufaa. ²⁷ Kanisa nzuri na safi mbele ya Mungu Baba ni hii: Kusaidia mayatima na wa jane ndani ya mateso yao, ku ji chungu vizuri na hui dunia.

Chapter 2

¹ Wa ndugu musiki changanisha amani ya Bwana Yesu Kristo, Bwana wa utukufu na ubaguzi ya batu bengine. ² Kwa mufano mkuu aniki ingiya ndani ya nkuardi yenu ana vala kikomo ya oa na manguo muzuri, na maskini ana ingiya na manguo ya buchafu. ³ Kama una angaliya ule ana vala manguwo muzuri na kusema: samani, ikala kwa iyi fasi ya heshima! Lakini una ambiya maskini: weye, simama pale, ao «Ikalala ku mangula yangu» ⁴ Ha ufanye ubagizi we peke? Ha mukuwe na kabula na mawazo yenu? ⁵ Ba ndugu bapenzi, Mungu ka changula ba maskini ya dunia kuwa batajini ndani ya imani, na kuwa warizi ndani ya ufalame ali lake benye bana mupenda? ⁶ Lakini mu na oneya wa maskini! haiko batajiri benye ku bateso? haiko njo abo bana babebaka kwenye chimba ya wa a mzi? ⁷ Na watukane njina nzuri yenu? ⁸ Njo kwa mana kama una timiza cheria ya maandiko: «uta penda mwezako kama wewe mwenyewe» una fanya muzuri. ⁹ Lakini kama una pendeleya batu bengine una fanya zambi na una umju shiria. ¹⁰ Sbabu yeyote anaye heshimiya sheria yetu, lakini akianguka kidogo ana haribisha sheria yote, ana pashwa ku hukumiwa. ¹¹ Sababu nani alisema: «Hauta fanya busharati» aka sema tena «Hauta uwa» kama hausharatike lakini una uwa, una vuja sheria. ¹² Hivi kusema na kutenda kwenu iwe kama ya batu bata sambishiwa ku fatana na sheria ya uhura. ¹³ Sababu Mungu hata sikiya uruma kwa ule ana kosa uruma juu uruma ni ya lazima kuliko kusambiswa. ¹⁴ Ndugu yangu nini ya muhimu kwa mutu akisema iko na imani bila matendo? ile imani yaweza ku muokowa? ¹⁵ Kama ndugu ana kosa manguo na chakwa. ¹⁶ Mfane moja wenu ana mwambiya: «wende na amani vala koti na kula ushibe.» Lakini Haumu leteye bila ana kosa juu ya mulili yake, ile ni muzuri kwa nini? ¹⁷ Namuna moja kwa imani, kama haina mapendo, ni yenyi kufa. ¹⁸ Ijapakuwa mwengine akisema: « uko na imani na niko na bitendo.» Ni oneshe imani yako bila matendo na miye nikuoneshe imani yangu kwa bitendo. ¹⁹ Una amini kama Mungu iko, una fanya muzuri. Lakini hata mapepo chafu wana amini na ku teteleke. ²⁰ We mjinga una penda niku oneshe kama imani bila matendo ni bure? ²¹ Tate yetu Ibrahimu haku pata sheria ju ya matendo kwku mtowa mtote yake isaka kwenyi mazahubu? ²² Una ona kama na matendo ina tembeya njiya moja, na kwa matendo, imani yake ika zidi. ²³ Ivi maandiko iko timilika : «Ibrahimu aka amini Mungu na Mungu aka mufanya kuwa mwenyi laki», kwahivi Ibrahimu aka itwa rafiki yake.» ²⁴ Una ona kama ni kwa matendo mutu ana pata haki, na laiko tu kwa imani. ²⁵ Kwa namna moja piya, rahabu kahaba hakupata haki kupitiya matendo wakati ali karibisha wa jumbe, na akawa toroshe kwa njia yingine? ²⁶ Juu vile mwili ina kosa nafsi niya kufa, imani matendo nayo ni ya kufa

Chapter 3

